JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

# TAARIFA YA MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA ZOTE KWA KIPINDI CHA MWAKA 2020 HADI 2025



IMEANDALIWA NA OFISI YA WAZIRI MKUU
(SERA, BUNGE NA URATIBU)

MEI, 2025

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

# TAARIFA YA MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA KATIKA SEKTA ZOTE KWA KIPINDI CHA MWAKA 2020 HADI 2025

IMEANDALIWA NA OFISI YA WAZIRI MKUU
(SERA, BUNGE NA URATIBU)

MEI, 2025

# YALIYOMO


SURA YA KWANZA ........ 3

1. UTANGULIZI ........ 3

SURA YA PILI ........ 8

2. HALI YA UCHUMI ........ 8

SURA YA TATU ........ 19

3. SEKTA ZA HUDUMA YA JAMII ........ 19

SURA YA NNE ........ 38

4. SEKTA ZA UZALISHAJI ........ 38

SURA YA TANO ........ 65

5. UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO ........ 65

SURA YA SITA ........ 86

6. UTUMISHI NA UTAWALA BORA ........ 86

SURA YA SABA ........ 94

7. ULINZI NA USALAMA ........ 94

SURA YA NANE ........ 101

8. USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA 101

SURA YA TISA ........ 104

9. URATIBU WA MASUALA MBALIMBALI ........ 104

HITIMISHO ........ 120

# SURA YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliingia madarakani tarehe 19 Machi, 2021 kutokana na kifo cha aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kilichotokea tarehe 17 Machi, 2021. Mabadiliko ya uongozi yalizingatia Ibara ya 5 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inayoeleza kuwa: "*Endapo kiti cha Rais kitakuwa wazi kutokana na Rais kufariki dunia, kujiuzulu, kupoteza sifa za uchaguzi au kutomudu kazi zake kutokana na maradhi ya mwili au kushindwa kutekeleza kazi na shughuli za Rais, basi Makamu wa Rais ataapishwa na atakuwa Rais kwa muda uliobaki katika kipindi cha miaka mitano na kwa masharti yaliyoelezwa katika ibara ya 40, kisha baada ya kushauriana na chama cha siasa anachotoka, Rais atapendekeza jina la mtu atakayekuwa Makamu wa Rais na uteuzi huo utathibitishwa na Bunge kwa kura zisizopungua asilimia hamsini ya Wabunge wote*".

Mara baada ya kuingia madarakani, Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alianzisha falsafa ya 4R ambayo ni Maridhiano (*Reconciliation*), Ustahimilivu (*Resiliency*), Mabadiliko (*Reform*) na Kujenga upya (*Rebuilding*). Falsafa hiyo ni dira ya kisera iliyolenga kuijenga upya Tanzania yenye mshikamano, haki na maendeleo endelevu kwa misingi ya demokrasia na ushirikishwaji wa wananchi. Falsafa ya 4R imekuwa nguzo muhimu katika maendeleo endelevu na demokrasia jumuishi ya nchi ya Tanzania pamoja na kuimarisha demokrasia na ushirikishwaji wa wananchi katika masuala ya msingi ya Taifa.

Wakati akilihutubia Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 22 Aprili, 2021 Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliahidi kuimarisha demokrasia, utawala bora na haki za binadamu; kuboresha huduma za jamii hususan elimu, afya na maji; kuendeleza miundombinu ya usafiri na nishati; kuimarisha mazingira ya uwekezaji na biashara; kukuza uchumi wa viwanda na matumizi ya teknolojia; na kuimarisha uhusiano wa kikanda na kimataifa. Vilevile, iliahidi kudumisha mazuri ya Awamu zilizopita, kuyaendeleza mema yaliyopo na kuleta mengine mapya; pamoja na kudumisha Tunu za Taifa yaani amani, umoja na mshikamano, uhuru wa nchi yetu, Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar pamoja na Muungano.

Ahadi alizozitoa zimetekelezwa kwa mafanikio makubwa kupitia Sera, Mipango na Mikakati mbalimbali ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya Mwaka 2020; Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025; Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/2022 - 2025/2026); Ajenda 2030 ya Malengo ya Maendeleo Endelevu: na Ajenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika. Vilevile, uhamasishaji kupitia kauli mbiu ya ***Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Kazi iendelee.***

Katika kipindi cha utawala wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi mahiri wa Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, nchi imeendelea kuwa na amani, umoja na mshikamano pamoja na kuendelea kulinda Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar na kudumisha Muungano wa Tanzania. Vilevile, Serikali imeendelea kuimarisha demokrasia, utawala bora na haki za binadamu kwa kufanya marekebisho ya sheria mbalimbali, kuondoa zuio la mikutano ya hadhara ya vyama vya siasa, na kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari ili kuwezesha wananchi wengi zaidi kupata habari kwa wakati.

Kwa upande wa utoaji wa huduma za kijamii, Serikali imechukua hatua mbalimbali ili kuimarisha upatikanaji wa huduma hizo ikiwemo elimu, afya, na maji. Katika sekta ya elimu, Serikali imeendelea kutoa fedha za kugharamia mpango wa elimu bila ada katika ngazi ya shule za msingi na sekondari; kujenga na kukarabati miundombinu ya shule nchini; kuongeza bajeti ya mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya juu; kuanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya vyuo vya kati pamoja na kuhuisha mitaala mbalimbali ya elimu. Vilevile, kwa upande wa sekta ya afya, Serikali imejenga majengo ya kutolea huduma za afya; kuimarisha hali ya upatikanaji wa dawa, vitendanishi, vifaa, vifaa tiba na mitambo ya kisasa ya uchunguzi na ugunduzi wa magonjwa; pamoja na kuboresha huduma za ubingwa na ubingwa bobezi. Aidha, kwa upande wa sekta ya maji, Serikali imesimamia utekelezaji wa miradi ya maji ambayo imeimarisha hali ya upatikanaji wa maji na kupunguza adha zilizokuwepo katika kutafuta huduma hiyo; kuendeleza tafiti za teknolojia bora zinazotumika katika kutoa huduma ya maji na kusimamia matumizi endelevu ya rasilimali za maji.

Vilevile, Serikali imeboresha miundombinu na huduma za usafiri na usafirishaji ikiwemo kuendelea na ujenzi wa reli ya kati kwa kiwango cha kimataifa (SGR) ambayo imeanza kutoa huduma kwa sehemu ya Dar es Salaam – Morogoro - Dodoma; kuboresha miundombinu ya Bandari za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara; Kuimarisha kampuni ya ndege; na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege na miundombinu ya barabara. Hatua hiyo imechangia kuimarisha huduma za usafirishaji wa abiria na mizigo ndani na nje ya nchi na hivyo kuimarisha uchumi wa nchi. Aidha, kwa upande wa nishati, Serikali imekamilisha miradi mbalimbali ya uzalishaji wa umeme ikiwemo Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere na mradi wa kuzalisha umeme wa Rusumo kwa kutumia maporomoko ya maji ya Mto Kagera ambayo imeongeza umeme katika gridi

ya Taifa. Pia, imeimarisha miundombinu ya kusafirisha umeme katika maeneo mbalimbali nchini.

Katika kuimarisha mahusiano ya kikanda na kimataifa hasa katika kukuza diplomasia ya kiuchumi, Serikali iliratibu ziara na mikutano ya viongozi wa kitaifa nje ya nchi na viongozi wa mataifa mengine nchini. Kutokana na ziara hizo, Tanzania imenufaika na uwekezaji na mikopo yenye masharti nafuu kwa ajili ya ugharamiaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo katika sekta za nishati; kilimo; maji; mazingira na hali ya hewa; usafiri na usafirishaji; afya; elimu; mawasiliano na teknologia ya Habari; na viwanda na biashara. Katika hatua nyingine, Serikali imeendelea kutambua umuhimu wa upatikanaji wa ajira hususan kwa kundi la vijana ambao ndio nguvukazi kubwa ya Taifa hili ili kuendelea kukuza uchumi. Kutokana na umuhimu huo, Serikali ilibuni na kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuzalisha fursa za ajira nchini kupitia uwekezaji katika sekta mbalimbali na utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati. Kupitia juhudi hizo na kwa kushirikiana na sekta binafsi, jumla ya ajira 8,084,204 zilizalishwa katika sekta za umma na binafsi katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025.

Kutokana na utekelezaji wa vipaumbele, pamoja na uwekezaji mkubwa uliofanywa na Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi Pato la Taifa lilikua kutoka asilimia 4.8 mwaka 2020 hadi asilimia 5.5 mwaka 2024 na mfumuko wa bei kuendelea kuwa himilivu na kubaki ndani ya lengo la nchi ambalo ni chini ya asilimia 5 na malengo ya nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC). Vilevile, wastani wa Pato la mtu Mmoja Mmoja *(GDP per Capita)* umeongezeka kutoka shilingi 2,468,241 mwaka 2020 hadi shilingi 3,204,244 mwaka 2024.

Taarifa hii imeainisha kwa kina Mafanikio ya Serikali ya Awamu ya Sita katika sura tisa (9). Sura ya kwanza ni utangulizi kuhusu

mafanikio; Sura ya pili ni hali ya uchumi; Sura ya tatu ni sekta za huduma ya jamii; Sura ya nne ni sekta za uzalishaji; Sura ya tano ni sekta ya ujenzi, uchukuzi, mawasiliano na nishati; Sura ya sita sekta ya utumishi na utawala bora; Sura ya saba ni ulinzi na usalama; Sura ya nane ushirikiano wa kikanda na kimataifa; na Sura ya tisa inabainisha mafanikio yaliyopatikana katika masuala mbalimbali.

# SURA YA PILI

## 2. HALI YA UCHUMI

### 2.1 Usimamizi wa Uchumi Jumla

Ukuaji wa uchumi wa nchi yoyote duniani unategemea utekelezaji madhubuti wa sera, programu na mikakati mbalimbali ya nchi. Kipindi cha Awamu ya Sita kilikumbwa na misukosuko mbalimbali ikiwemo janga la UVIKO 19 pamoja na migogoro ya Kimataifa ambayo iliathiri uchumi wa nchi mbalimbali ikiwemo Tanzania. Kutokana na hali hiyo, Serikali ilitekeleza Mikakati mbalimbali ya kisera, kiutawala na uwekezaji katika miundombinu ya sekta za usafirishaji, nishati, elimu, maji na afya ili kukabiliana na changamoto hizo. Mikakati hiyo imewezesha kupata mafanikio yafuatayo:

i. Kuongezeka kwa ukuaji wa uchumi kutoka asilimia 4.8 mwaka 2020 hadi asilimia 5.5 mwaka 2024;

ii. Kuongezeka kwa Wastani wa pato la mtu mmoja mmoja (*GDP per Capita*) kutoka shilingi 2,468,241 mwaka 2020 hadi shilingi 3,204,244 mwaka 2024;

iii. Kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya ndani kutoka shilingi trilioni 20.59 mwaka 2020/2021 hadi shilingi trilioni 28.83 mwaka 2023/2024. Aidha, kwa kipindi cha mwaka 2024/2025, kuanzia Julai, 2024 hadi Machi, 2025 jumla ya shilingi trilioni 25.67 zimekusanywa. Vilevile, katika kipindi cha Novemba, 2020 hadi Machi, 2025 jumla ya shilingi trilioni 120.16 zilikusanywa kutoka katika vyanzo vya ndani. Kati ya fedha hizo, shilingi trilioni 103.87 ni mapato yaliyokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania na

shilingi trilioni 16.29 ni mapato yaliyokusanywa na Wizara, Wakala za Serikali, Mashirika na Taasisi za Umma pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, mapato ya ndani yaliyokusanywa kwa mwezi yameongezeka kutoka shilingi trilioni 1.51 Novemba, 2020 hadi shilingi trilioni 3.09 Machi, 2025. Mapato hayo yameiwezesha Serikali kuendelea kuboresha hali ya maisha ya wananchi kwa kuimarisha upatikanaji wa huduma za jamii (afya, elimu na maji) na uimarishaji wa miundombinu wezeshi ya uwekezaji na biashara ikiwemo nishati na uchukuzi;

iv. Mfumuko wa bei kuendelea kuwa himilivu na kubaki ndani ya lengo la nchi (chini ya asilimia 5) na vilevile Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Wastani huo wa mfumuko wa bei umeendelea kulinda pato la mwananchi mmoja mmoja na kumwezesha kununua bidhaa zaidi na hivyo kuchangia kuboresha maisha. Aidha, kwa upande wa wawekezaji na wazalishaji, hali hiyo imeondoa wasiwasi wa mabadiliko ya bei na hivyo kuchangia kuongeza uwekezaji;

v. Kukua kwa biashara ya nje kutokana na kuboreshwa kwa mazingira ya biashara na uwekezaji ambapo mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi yaliongezeka kutoka Dola za Marekani bilioni 8.83 kwa kipindi cha miezi 12 iliyoishia Novemba, 2020 hadi Dola za Marekani bilioni 16.5 kwa kipindi kilichoishia Machi, 2025. Aidha, ongezeko hilo lilichagizwa kwa sehemu kubwa na mauzo ya bidhaa za madini, hususan dhahabu; zao la korosho; na kuimarika kwa shughuli za utalii kulikochangiwa na utangazaji wa filamu za *The Royal Tour* na *Amazing Tanzania* ambazo zimekuwa na mchango mkubwa katika kuvutia utalii nchini;

vi. Kuongezeka kwa thamani ya bidhaa na huduma zilizoagizwa kutoka nje ya nchi kutoka Dola za Marekani bilioni 8.96 kwa miezi 12 iliyoishia Novemba, 2020 hadi Dola za Marekani bilioni 17.06 katika kipindi kama hicho kilichoishia Machi, 2025; na

vii. Kuongezeka kwa Bajeti ya Serikali kutoka shilingi trilioni 34.88 mwaka 2020/21 hadi shilingi trilioni 57.04 mwaka 2025/26 na hivyo kuwezesha kuboresha huduma na miundombinu katika sekta mbalimbali zikiwemo afya, maji, elimu, nishati, ujenzi wa barabara, madaraja na treni ya kisasa ya SGR, pamoja na ununuzi na usambazaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

## 2.2 Uendelezaji wa Sekta ya Fedha, Huduma za Kibenki na Bima

Serikali imeendelea kusimamia utekelezaji wa sera na sheria za uendelezaji wa sekta ya fedha, huduma za kibenki na bima. Katika kipindi cha Novemba, 2020 hadi Aprili, 2025 Serikali ilifanya Marejeo ya Kanuni za Fedha za Kigeni za Mwaka 2022 kwa lengo la kuimarisha usimamizi na upatikanaji wa fedha za kigeni nchini. Vilevile, ilifanya mapitio ya Sheria ya Benki Kuu ya Tanzania, Sura 197, sehemu ya 26 ili kuhakikisha sarafu ya shilingi ya Tanzania inatumika katika upangaji wa bei na malipo ya bidhaa na huduma mbalimbali ndani ya nchi. Kutokana na jitihada hizo mafanikio mbambali yamepatikana ikiwemo:

i. Kiwango cha fedha za kigeni kuendelea kubaki ndani ya lengo la nchi la kutosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4 ambapo hadi Machi, 2025 akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani bilioni 5.69. Kiwango hicho kinatosheleza uagizaji wa bidhaa na huduma nje ya nchi kwa muda wa miezi 4.6 ikilinganishwa dola za Marekani bilioni 4.76 mwishoni mwa mwaka 2020. Aidha,

katika kuimarisha akiba ya fedha za kigeni na kupunguza changamoto zinazojitokeza kutokana na uhaba wa dola ya Marekani, Serikali imeendelea kubuni mikakati mipya ya kuongeza wigo wa vyanzo vya akiba ya fedha za kigeni ikiwemo kufanya marejeo ya sheria ya ongezeko la thamani kwa kufuta tozo ya kodi ya ongezeko la thamani kwenye madini ya dhahabu yatakayouzwa kwa Benki Kuu.

Vilevile, imeanzisha programu ya ununuzi wa dhahabu ndani ya nchi kwa kutumia shilingi ambapo hadi Machi, 2025 takribani tani 3.42 za dhahabu yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 342.64 zimenunuliwa na kuhifadhiwa. Lengo ni kuendelea kununua dhahabu hadi kufikia tani sita (6) ifikapo 2030. Ununuzi wa dhahabu ndani ya nchi, umewezesha uwepo wa soko la uhakika la dhahabu kwa wachimbaji wadogo waliojirasimisha pamoja na kuongeza wigo wa akiba ya nchi na hivyo kuilinda nchi na misukosuko ya kiuchumi;

ii. Kuongezeka kwa mikopo ya kigeni kwa sekta binafsi kutoka Dola za Marekani bilioni 5.34 Novemba, 2020 hadi Dola za Marekani bilioni 7.38 Machi, 2025 ambazo zimewekezwa na sekta binafsi katika shughuli mbalimbali za kiuchumi. Kuongezeka kwa mikopo hiyo, kumewezesha sekta binafsi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kiuchumi hususan sekta za uchimbaji wa madini, fedha na bima, viwanda, usafirishaji na mawasiliano, hivyo kuongeza ajira na kipato kwa wananchi;

iii. Kulipwa kwa madeni yaliyohakikiwa ya shilingi trilioni 4.40 kwa wakandarasi, watumishi, watoa huduma na wazabuni na hivyo kuchangia katika kuongeza mitaji, shughuli za kiuchumi, kijamii, ajira na kipato cha mwananchi; na

iv. Kuimarika kwa sekta ya bima kwa kuongezeka kwa idadi ya watoa huduma za bima kutoka 993 mwaka 2021 hadi 2,208 mwaka 2024; kampuni za bima mtawanyo nchini kutoka kampuni moja (1) mwaka 2021 hadi kampuni nne (4) mwaka 2024; wanufaika wa huduma za bima kutoka milioni 14.2 mwaka 2021 hadi milioni 25.9 mwaka 2024; ajira rasmi katika soko la bima kutoka 3,527 mwaka 2021 hadi 6,916 mwaka 2024; thamani ya mali katika soko la bima kutoka shilingi trilioni 1.277 mwaka 2021 hadi shilingi trilioni 2.340 mwaka 2024; na kuimarika kwa thamani ya mitaji katika soko la bima kutoka shilingi bilioni 416.0 hadi shilingi bilioni 847.3.

## 2.3 Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi

### 2.3.1 Kukuza uwezeshaji kiuchumi

Serikali imeendelea kuchukua juhudi za maksudi ili kuwawezesha wananchi kuimarisha ushiriki wao katika shughuli za kiuchumi. Juhudi hizo zilijumuisha utekelezaji wa Sera, Sheria, mikakati, programu na huduma mbalimbali za uwezeshaji. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

(i) Kuongezeka kwa mikopo iliyotolewa kupitia mifuko na programu za uwezeshaji wananchi kiuchumi kutoka shilingi billioni 904.25 mwaka 2021 hadi trilioni 3.5 mwaka 2024;

(ii) Kuongezeka kwa wananchi waliopata mikopo kupitia mifuko na programu za uwezeshaji kutoka wanufaika 3,562,810 mwaka 2021 hadi wanufaika 6,183,835 mwaka 2024;

(iii) Kuongezeka wananchi waliojengewa uwezo wa uzalishaji na urasimishaji wa biashara katika sekta mbalimbali kutoka wananchi 3,829,412 mwaka 2021 hadi wanufaika 5,493,580 mwaka 2024;

(iv) Kuongezeka kwa marejesho ya mikopo kutoka mifuko na programu za uwezeshaji kutoka marejesho ya shilingi 501.73 bilioni mwaka 2021 hadi kufikia marejesho ya shilingi 2.17 trilioni mwaka 2024; na

(v) Kuongezeka kwa vituo vya uwezeshaji wananchi kiuchumi kutoka vituo 11 hadi vituo 29 mwaka 2025.

### 2.3.2 Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini

Serikali iliendelea kutekeleza Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini Awamu ya Tatu kwa maeneo yote ya Tanzania Bara na Zanzibar. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuongezeka kwa kaya za walengwa kutoka 876,440 waliopata shilingi bilioni 34.9 mwaka 2021 hadi walengwa 1,371,916 waliopata Shilingi trilioni 1.12 mwaka 2025. Aidha, kaya za walengwa zimeboresha maisha yao kwa kuanzisha shughuli za kujipatia kipato kupitia kilimo, ufugaji, uvuvi na biashara ndogondogo; na

ii. Kutekeleza jumla ya miradi 27,863 yenye thamani ya shilingi bilioni 291.7 kwa kaya 909,440 mwaka 2025 ikilinganishwa na miradi 3,185 yenye thamani ya shilingi bilioni 38.6 kwa kaya 197,110 mwaka 2020. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa malambo, barabara za vijijini, mifereji ya umwagiliaji na makinga tuta; uanzishwaji wa vitalu vya miche; na uhifadhi wa mazingira na misitu kupitia upandaji wa miti.

## 2.4 Mwenendo wa Uwekezaji katika Sekta Binafsi

Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuvutia uwekezaji wa ndani na nje ya nchi. Mikakati hiyo ililenga kuweka mazingira yatakayomwezesha mwekezaji kufikia malengo yake kulingana

na Mipango ya Kitaifa. Utekelezaji wa Mikakati huyo umeleta mafanikio mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

i. Kusajili jumla ya miradi 2,175 inayotarajiwa kuzalisha ajira 650,674 na uwekezaji wa jumla ya mtaji wa Dola za Marekani bilioni 25.53 katika kipindi cha mwaka 2021 hadi 2024. Aidha, idadi ya miradi iliongezeka kutoka 256 mwaka 2021 hadi 901 mwaka 2024 ambapo kiwango cha mitaji kilipanda kutoka Dola za Marekani bilioni 3.74 mwaka 2021 hadi Dola za Marekani bilioni 9.31 mwaka 2024; na

ii. Kusajili miradi 45 katika maeneo mbalimbali nchini kupitia leseni za Eneo Maalum la Uwekezaji (EPZ) na Ukanda Maalum wa Kiuchumi (SEZ). Miradi hiyo imeleta mitaji ya jumla ya Dola za Marekani bilioni 1.17 na kuongeza ukuaji wa mauzo ya nje yenye thamani ya Dola za Marekani milioni 397.64 na ajira zipatazo 20,674.

### 2.5 Mapato yasiyo ya Kodi na thamani ya uwekezaji

Serikali imeendelea kukusanya mapato yasiyo ya kodi ambayo yanajumuisha Gawio, Michango ya asilimia 15 ya Mapato ghafi na mapato mengineyo. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuongezeka kwa mapato yasiyo ya kikodi kutoka shilingi billioni 637.66 mwaka 2021 hadi shilingi trilioni 1.008 mwaka 2023; na

ii. Kuongezeka kwa thamani ya uwekezaji wa katika taasisi, mashirika ya Umma na Wakala za Serikali kutoka shilingi trilioni 67.01 mwaka 2020 hadi shilingi trilioni 85.4 mwaka 2024. Aidha, uwekezaji wa Serikali nje ya nchi ulifikia shilingi bilioni 846.22 kutoka shilingi bilioni 722.94 mwaka 2020/21.

## 2.6 Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050

Serikali imeendelea kuratibu maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050 ambapo rasimu ilizinduliwa tarehe 11 Desemba, 2024 na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi. Maandalizi ya rasimu hiyo yalikuwa jumuishi na shirikishi ambapo jumla ya washiriki 1,172,106 kutoka Tanzania Bara na Zanzibar walitoa maoni yao. Aidha, Serikali imeendelea na uandaaji wa Mpango Elekezi wa Muda Mrefu (LTPP) ambao utatumika kama mwongozo wa maandalizi ya Mipango ya Muda wa Kati na Muda Mfupi ya Utekelezaji wa Dira 2050.

## 2.7 Sensa ya Watu na Makazi

Serikali iliendesha zoezi la Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 ambayo ilibainisha uwepo wa idadi ya watu 61,741,120 ambapo kati yao, watu 59,851,347 wanatoka Tanzania Bara na 1,889,773 wanatoka Tanzania Zanzibar. Sensa hiyo imekusanya taarifa mbalimbali zikiwemo taarifa za kidemografia, shughuli za kiuchumi, hali ya ulemavu, uhamaji, huduma za kijamii, majengo na anwani ya makazi. Matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022 yamekuwa na matumizi makubwa katika kuandaa mipango jumuishi ya maendeleo endelevu ya nchi na kwa kuzingatia idadi ya watu katika ngazi zote za utawala.

## 2.8 Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji

Serikali imeendelea na utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji Nchini (MKUMBI) unaolenga kuondoa changamoto mbalimbali katika taratibu za uwekezaji na ufanyaji biashara. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kupitia na kurekebisha sheria na kanuni 66 kwa lengo la kupunguza ushuru, kurahisisha upatikanaji wa ardhi kwa

wawekezaji husussan katika sekta za viwanda na biashara, kilimo, ufugaji, afya pamoja na maliasili na utalii;

ii. Kufuta na kupunguza tozo, ada na faini mbalimbali zipatazo 383 zilizobainishwa kuwa kero katika ufanyaji biashara. Mathalan, Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) ilifuta ada 14 na kupunguza kiasi cha ada 9, Bodi ya Sukari Tanzania (SBT) ilifuta ada 16; na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA) ilifuta ada 12;

iii. Kuondoa na kuunganisha majukumu ya mamlaka za udhibiti ambayo yanafanana. Mathalan, majukumu ya kutoa vibali vya kusafirisha kemikali vilivyokuwa vinatolewa na Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba Tanzania (TMDA), Wakala ya Barabara Tanzania (TANROAD) na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA) hivi sasa vinatolewa na Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali pekee; na

iv. Kukamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Kuhudumia Wawekezaji (Tanzania Electronic Investment Window - TeIW) kwa awamu ya kwanza ambao umeunganisha huduma 7 kutoka taasisi 6. Mfumo huo unawawezesha wawekezaji kuomba na kupatiwa cheti cha uwekezaji, vibali vya kazi na ukaazi, cheti cha mlipa kodi (TIN), vivutio vya kikodi, kitambulisho cha taifa (NIDA) na usajili wa makampuni kwenye dawati moja.

### 2.9 Usimamizi wa Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa Tanzania

Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali za kukuza soko la mitaji nchini kwa kuboresha mifumo ya kidigitali inayowezesha kununua na kuuza bidhaa kwa teknolojia ya habari na mawasiliano, husussan simu za kiganjani. Aidha,

mifumo ya *Sim Invest* na Hisa Kiganjani inatumika katika kuuza na kununua dhamana za masoko ya mitaji. Jitihada hizo zimewezesha utoaji wa Hatifungani saba (7) ambazo ni:

i. Hatifungani ya kijani, inayoitwa "*CRDB Kijani Bond"* kwa ajili ya kutekeleza miradi rafiki kwa mazingira, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 171.8 kimepatikana;

ii. Hatifungani yenye mguso na matokeo chanya kwa jamii, inayoitwa *"NMB Jamii Bond*" kwa ajili ya kuendeleza biashara na shughuli za miradi endelevu inayomilikiwa na kuendeshwa na vijana na watu wenye mahitaji maalumu, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 212.9 kimepatikana;

iii. Hatifungani yenye mguso wa jinsia, iliyoitwa "*NMB Jasiri Bond"* kwa ajili ya kutoa mikopo ya kuendeleza biashara ndogo na za kati zinazomilikiwa na kuendeshwa na wanawake, pamoja na zile zinazomilikiwa na wanaume lakini bidhaa na huduma zake zina matokeo chanya kwa mwanamke, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 74.2 kimepatikana;

iv. Hatifungani ya Miundombinu ya miaka mitano iitwayo *Samia Infrastructure Bond* kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya Barabara vijijini na mijini, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 323.1 kimepatikana;

v. Hatifungani ya Miaka 10 ya Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira ya Jiji la Tanga kwa ajili ya kupata fedha za kutekeleza miradi ya ujenzi wa miundombinu ya huduma endelevu za maji na utunzaji wa mazingira katika Jiji la Tanga, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 54.7 kimepatikana;

vi. Hatifungani inayokidhi misingi ya Shariah inayoitwa "*KCB Fursa Sukuk"* kwa ajili ya kupata fedha za kuwekeza katika

biashara ndogo na za kati zinazokidhi misingi ya Shariah, ambapo kiasi cha shilingi bilioni 11 kimepatikana; na

vii. Hatifungani inayokidhi misingi ya Shariah kwa ajili ya kupata fedha za kutekeleza shughuli za kuboresha miundombinu ya kituo cha afya na shule iliyotolewa na shule ya Sekondari ya Wasichana *Premier* ambapo kiasi cha shilingi bilioni 1.9 kimepatikana.

### 2.10 Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Serikali imeimarisha uratibu na usimamizi wa ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi ambapo pamoja na masuala mengine imeanzisha Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Maboresho hayo yameimarisha uratibu na usimamizi wa miradi ya ubia ambapo jumla ya miradi 105 ilitambuliwa katika mikoa 13. Kati ya hiyo miradi 80 ilichambuliwa ambapo, miradi mitatu (3) ya ubia imetekelezwa, minne (4) ipo katika hatua ya mashauriano, miwili (2) ipo katika hatua ya ununuzi, 39 ipo katika hatua mbalimbali za upembuzi yakinifu na 32 ipo katika hatua ya andiko dhana. Uwepo wa miradi hiyo umewezesha Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi kupeleka huduma bora kwa wananchi pamoja na kuongeza kipato kwa wananchi. Kwa mfano, mradi wa *Dar es Salaam Development Corporation - DDC* umezalisha ajira 400 kwa wananchi.

# SURA YA TATU

## 3. SEKTA ZA HUDUMA YA JAMII

### 3.1 Elimu

Serikali imefanya mapitio ya Sera ya Elimu na Mafunzo ya Mwaka 2014, Toleo la Mwaka 2023 na Mitaala ya elimu ngazi ya awali, msingi, sekondari na elimu ya ualimu ili kuimarisha utoaji wa elimu nchini. Sera na mitaala iliyoboreshwa inalenga kuwa na wahitimu wenye maarifa, maadili na ujuzi ili waweze kujiajiri na kukidhi mahitaji ya soko la ajira. Katika uimarishaji huo mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwemo:

#### 3.1.1 Elimu Awali, Msingi na Sekondari

**Miundombinu**

i. Kuimarisha miundombinu ya elimu kwa kujenga shule 26 za Kitaifa za sayansi za wasichana kwa kila mkoa na shule 7 za wavulana kila kanda; kuongeza vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari kutoka madarasa 191,708 mwaka 2020 hadi madarasa 254,393 mwaka 2025; kuboresha shule 274 za michepuo ya kilimo na shule 28 za michepuo ya biashara; kujenga shule za sekondari 1,031, kutoka 3,863 hadi shule 4,894 mwaka 2025; kujenga shule mpya za msingi kutoka 16,406 mwaka 2020 hadi 17,986 mwaka 2025; kutoa vifaa vya kisasa katika shule 28 za mchepuo wa elimu ya amali; kuongeza nyumba za walimu kutoka 58,637 mwaka 2020 hadi 60,429 mwaka 2025; maabara 8,072 mwaka 2020 hadi 8,710 mwaka 2025; maktaba 1,537 mwaka 2020 hadi 2,665 mwaka 2025; mabwalo 871 mwaka

2020 hadi 1,004 mwaka 2025; kukamilisha ukarabati wa shule za sekondari 74 na shule za msingi 794 pamoja na kuendelea na ujenzi wa shule 29 za amali za mikoa. Aidha, miundombinu hiyo imeongeza fursa za elimu kwa wanafunzi na kupunguza muda na umbali wa wanafunzi kwenda na kurudi shuleni.

### 3.1.1.1 Elimu Bila Ada

i. Kuendelea kutekeleza Mpango wa Elimu Bila Ada kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha sita kwa kuongeza fedha za kugharamia mpango huo kutoka shilingi bilioni 249.66 mwaka 2020 hadi shilingi bilioni 484.27 mwaka 2025 na hivyo kuchangia kuongeza wanafunzi wanaonufaika kutoka 14,940,925 mwaka 2020 hadi 16,155,281 mwaka 2024; na

ii. Kurejesha wanafunzi 3,402 wa shule za msingi na 14,945 wa shule za sekondari waliokatiza masomo kwa sababu mbalimbali. Aidha, urejeshaji huo ni hatua muhimu katika kuhakikisha kila mtanzania anapata fursa ya kupata elimu bora kwa ajili ya maendeleo binafsi na Taifa.

### 3.1.1.2 Walimu, Vitabu, Vitendea Kazi na Mafunzo

i. Kuongeza idadi ya walimu kutoka walimu 262,736 mwaka 2020 hadi 314,040 mwaka 2025 wakiwemo walimu 447 wa elimu maalum;

ii. Kuongeza idadi ya vitabu kwa wanafunzi wa shule za msingi kutoka nakala 24,268,715 mwaka 2020 hadi nakala 32,049,668 mwaka 2025. Kuongeza nakala za vitabu kwa wanafunzi wa shule za sekondari kutoka nakala 1,078,517 mwaka 2020 hadi 8,643,643 mwaka 2025. Ongezeko hilo limesababisha kuwa na wastani wa uwiano wa 1:3 kwa kitabu kwa mwanafunzi shule za msingi na sekondani; na

iii. Kuongeza idadi ya walimu waliopata mafunzo ya utekelezaji wa mitaala kutoka walimu 1,250 wa shule za msingi na sekondari mwaka 2021 hadi 252,434 mwaka 2025, ambapo wa shule za msingi ni 185,180 na sekondari 67,254.

Juhudi hizo za kuongeza walimu na mafunzo, ununuzi na usambazaji wa vitabu pamoja na vitendea kazi umechangia katika kuinua ubora wa elimu ikiwemo ongezeko la ufaulu wa wahitimu wa ngazi ya elimu ya msingi kutoka asilimia 79.62 mwaka 2021 hadi ufaulu wa asilimia 80.87 mwaka 2024. Aidha, ufaulu wa Mtihani wa Kidato cha nne umeongezeka kutoka asilimia 87.30 mwaka 2021 hadi asilimia 92.37 mwaka 2024.

### 3.1.2 Elimu ya Ualimu

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kujenga vyuo vya Ualimu vya Sumbawanga, Dakawa, Mhonda, Kabanga na Ngorongoro;

ii. Kujenga miundombinu ya madarasa 41, kumbi za mihadhara tatu (3) na mabweni 15 katika vyuo 23 vya ualimu pamoja na kukarabati miundombinu katika Vyuo vya Ualimu vya Songea, Tarime, Mamire, Katoke, Singachini, Vikindu, Bunda, Mtwara (Ufundi), Mtwara (Kawaida), Monduli, Bustani, Butimba, Kasulu, Kleruu, Patandi, Mpwapwa, Korogwe na Morogoro;

iii. Kuongeza udahili wa wanachuo wa vyuo vya ualimu hadi 20,261 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 17 ikilinganishwa na wanachuo 17,260 waliosajiliwa mwaka 2020. Aidha, idadi ya wanachuo waliohitimu mafunzo ya ualimu katika ngazi ya stashahada na astashahada imeongezeka hadi wanachuo 7,918 mwaka 2024

ikilinganishwa na wanachuo 6,773 waliohitimu mwaka 2021;

iv. Kuwajengea uwezo wakufunzi 1,334 wa vyuo vya ualimu kuhusu ufundishaji wa masomo ya sayansi, michezo, muziki, sanaa za maonesho na ufundi, biashara na stadi nyingine za ufundishaji; na

v. Kuunganisha vyuo 25 vya ualimu katika Mkongo wa Taifa ili kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika kufundisha na kujifunza na kununua vifaa vya TEHAMA.

Uboreshaji wa miundombinu, huduma na uimarishaji wa matumizi ya TEHAMA katika vyuo vya ualimu umechangia kuimarisha ubora wa mafunzo ikiwemo kuongeza ufaulu wa wahitimu hadi asilimia 99.8 mwaka 2024 ikilinganishwa na ufaulu wa asilimia 96.9 mwaka 2021

### 3.1.3 Elimu Maalum

i. Kukamilika kwa ujenzi wa shule jumuishi ya mfano ya Lukuledi iliyopo Mkoani Mtwara yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 620; Shule Maalum ya Sekondari Patandi Mkoani Arusha yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 360; na Shule Jumuishi ya Mfano ya Awali, Msingi na Sekondari Mbuye Mkoani Geita yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 800; na

ii. Kuboresha mazingira ya utoaji wa elimu jumuishi na uongezaji wa nafasi za mafunzo kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum katika shule ili kutekeleza falsafa ya *No one is left behind* kwa kuandaa Mkakati wa Taifa wa Elimu Jumuishi wa Mwaka 2021/2022 - 2025/2026; Mwongozo wa Shule ya Nyumbani; Mwongozo wa Ubainishaji na Upimaji wa Kielimu kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum na Mwongozo wa Uanzishaji na Uendeshaji wa Elimu kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum.

### 3.1.4 Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi

i. Kuongeza vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi kutoka 662 (Sekta ya umma 108 na Sekta binafsi 554) mwaka 2020 hadi 860 (Sekta ya umma 162 na sekta binafsi 698) mwaka 2024;

ii. Kuongeza vyuo vya elimu ya ufundi kutoka vyuo ufundi 441 mwaka 2020 hadi 512 mwaka 2025;

iii. Kuanza kutoa mikopo kwa wanafunzi wa ngazi ya stashahada wanaosoma fani za kipaumbele ikiwemo Afya, Sayansi na Ufundi ambapo shilingi bilioni 19.95 zimetolewa kwa wanafunzi 7,534 kwa mwaka 2024/25;

iv. Kuanzisha vituo vya umahiri hususan katika sekta za nishati, kilimo na usindikaji, usafirishaji, TEHAMA na viwanda vya uzalishaji vilivyo katika mikoa ya Arusha, Dar es Salaam na Mwanza. Vituo hivyo vipo katika Chuo cha Ufundi Arusha (Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Nishati Jadidifu cha Kikuletwa); Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya Taaluma za Anga na Operesheni za Usafirishaji):Taasisi ya Teknolojia Kampasi ya Dar es Salaam (Kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya TEHAMA); na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam Kampasi ya Mwanza (Kituo cha umahiri cha Uchakataji Ngozi);

v. Kukamilisha ujenzi wa vyuo 29 vya mafunzo ya ufundi stadi ambavyo vimeanza kutoa mafunzo pamoja na kuendelea na ujenzi wa vyuo 65;

vi. Kukamilisha ukarabati wa vyuo 10 vya VETA vya Ileje, Urambo, Nkasi, Newala, Muleba, Itilima, Babati, Kilindi, Ngorongoro na Kasulu; na ukarabati wa vyuo sita (6) vya ufundi stadi na huduma za utengano wa Watu Wenye Ulemavu katika mikoa ya Tanga (Masiwani), Tabora

(Luanzari), Singida (Sabasaba), Dar es Salaam (Yombo) na Mtwara (Mtapika);

vii. Kununua vifaa na mitambo ya kisasa ya kufundishia na kujifunzia kwa vyuo 38 vya elimu ya mafunzo ya ufundi na vyuo 54 vya Maendeleo ya Wananchi; na

viii. Kuwezesha programu ya kuwatambua na kuwarasimisha watu wenye ujuzi katika fani za ufundi na ufundi stadi kupitia vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi VETA ambapo jumla ya watu 13,879 wenye ujuzi uliopatikana nje ya mfumo rasmi wa utoaji elimu wametambuliwa na kurasimishwa.

Maboresho hayo yameongeza udahili wa wanafunzi katika vyuo vya mafunzo ya ufundi stadi kutoka 344,815 mwaka 2020 hadi 446,251 mwaka 2024; na kuongeza udahili katika vyuo vya elimu ya ufundi kutoka wanafunzi 157,420 mwaka 2020 hadi wanafunzi 206,617 mwaka 2024. Aidha, ongezeko la fursa za elimu ya ufundi na mafunzo ya ufundi stadi na kuimarisha mafunzo katika ngazi hiyo kunawezesha Taifa kuwa na vijana wenye ujuzi unaohitajika katika kuchangia maendeleo ya Taifa

### 3.1.5 Elimu ya Juu

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na;

i. Kuongeza Bajeti ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu kutoka Shilingi bilioni 464 mwaka 2020 hadi Shilingi bilioni 787.4 mwaka 2025 na hivyo kuongeza idadi ya wanufaika wa mikopo kutoka wanafunzi 142,170 mwaka 2020 hadi 248,332 mwaka 2024;

ii. Kuanzisha programu ya ufadhili wa Mama Samia (SAMIA Scholarship) ili kuongeza wahitimu wa fani za sayansi katika Elimu ya Juu iliyoanzishwa mwaka 2022 ambapo

wanafunzi 1,343 wamenufaika na ufadhili huo wenye thamani ya Shilingi bilioni 18.7; na

iii. Kuondoa tozo ya asilimia 6 ya kulinda thamani ya fedha katika urejeshaji wa mkopo iliyokuwa inatozwa kwa wanufaika wa Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na tozo ya adhabu ya **asilimia 10** ya mkopo ambayo inatozwa kwa wanufaika waliochelewa kulipa mikopo hiyo.

Utoaji wa mikopo ya elimu ya juu umeongeza idadi ya wanafunzi wanaodahili katika taasisi za elimu ya juu kutoka wanafunzi 206,305 mwaka 2020 hadi 334,854 mwaka 2024. Kuongezeka kwa fursa za elimu ya juu kumeongeza idadi ya wahitimu wenye ujuzi na stadi za maisha za kukuza uchumi na hali za maisha ya jamii; kupunguza ombwe la ukosefu wa ajira litokanalo na kuwa na idadi kubwa ya vijana wasio na ujuzi, stadi na maarifa yanayotakiwa katika soko la ajira. Aidha, kuondolewa kwa tozo kwenye mikopo ya elimu ya juu kumeimarisha urejeshaji wa mikopo iliyoiva kwa hiari na kupunguza gharama ya mikopo kwa wanufaika ambayo ilikuwa inaongezeka kila mwaka**.**

### 3.1.6 Sayansi, Teknolojia na Ubunifu

Sayansi, Teknolojia na Ubunifu ni nyenzo muhimu katika kutatua changamoto mbalimbali za maendeleo hususan katika kuwezesha matumizi ya rasilimali kwa ufanisi zaidi. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuhimiza matumizi ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini. Katika kipindi cha utekelezaji mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwa ni pamoja na:

i. Kuendeleza bunifu 464 zilizotokana na mashindano ya Kitaifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (MAKISATU)

kupitia Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji wa Sayansi na Teknolojia (MTUSATE) ili kufikia hatua ya kubiasharishwa. Aidha, bunifu 64 kati ya hizo zimeendelezwa na kuingia sokoni;

ii. Kuanzisha Mfuko wa Bunifu ujulikanao kwa jina la *SAMIA Innovation Fund* ambao utawezesha upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wabunifu ili kuanzisha kampuni na kuingiza bidhaa sokoni;

iii. Kuleta nchini wataalamu wabobezi 44 ili kuhawilisha maarifa na teknolojia kwa ajili ya maendeleo ya Taifa; na

iv. Kuanzisha vituo 12 katika vyuo vya maendeleo ya wananchi ili kukuza na kuendeleza wabunifu nchini. Aidha, takribani ajira 600 zilizalishwa kutokana na kuimarishwa kwa vituo atamizi kwa ajili ya kukuza na kuendeleza wabunifu.

## 3.2 Afya

Sekta ya Afya ni muhimu katika kuhakikisha wananchi wanashiriki kikamilifu katika shughuli za maendeleo na kuchangia kuongezeka kwa kipato cha mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kujenga na kukarabati miundombinu ya kutolea huduma za afya, kuweka mazingira wezeshi kwa sekta binafsi kutoa huduma, kuongeza dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya pamoja na kuimarisha huduma za ubingwa na ubingwa bobezi. Jitihada hizo zimewezesha kupata mafanikio mbalimbali ikiwemo:

### 3.2.1 Miundombinu ya Kutolea Huduma za Afya

i. Kuongeza vituo vya kutolea huduma za afya kutoka 8,783 mwaka 2020 na hadi 12,846 mwaka 2025 sawa na ongezeko la vituo 4,063 ambapo kwa Zahanati

zimeongezeka kutoka 7,242 hadi 8,328; Vituo vya Afya kutoka 1,205 hadi 1,254; Hospitali zenye hadhi ya ngazi ya Wilaya kutoka 148 hadi 361; Hospitali zenye hadhi ya Mkoa kutoka 23 hadi 76; Hospitali zenye hadhi ya Kanda 18; Hospitali Maalumu 6 na Hospitali ya Taifa moja (1). Aidha, vituo vingine ni kliniki 1,013, Maabara Binafsi 1,676 na vituo vinginevyo 113. Kuongezeka kwa vituo hivyo nchini kumeiwezesha Serikali kusogeza huduma za afya karibu zaidi na wananchi ambapo hivi sasa asilimia 75 - 85 ya wananchi wanapata huduma za afya ndani ya kilomita 5 ya maeneo wanayoishi;

ii. Kukamilika kwa ujenzi wa Hospitali za Kanda ya Kusini Mtwara na Chato. Vilevile, majengo mapya yamejengwa katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda ya Kaskazini - KCMC (Banka za kusimika mitambo ya kutibu Saratani), Hospitali ya Kanda Mbeya na Hospitali ya Benjamin Mkapa - Dodoma (Jengo la kutolea huduma za Saratani) na Hospitali ya Kanda ya Bugando (Wodi ya wagonjwa wa Saratani);

iii. Kukamilika kwa ujenzi wa Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Katavi, Njombe, Songwe, Simiyu, Geita, Ruvuma, Shinyanga, Singida, Mara na Lindi. Hospitali hizi zimeanza kutoa huduma mbalimbali zikiwemo Huduma za Dharura (EMD), Mahututi (ICU), Mama na Mtoto (Maternity Ward), Upasuaji (Surgical), Magonjwa ya Ndani (Internal Medicine), Wagonjwa wa Huduma za Nje (OPD) na Huduma za Kusafisha Figo (Dialysis);

iv. Kukamilika kwa ukarabati na ujenzi wa majengo mapya ya kutolea huduma za afya katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ya Mtwara (Ligula), Mwanza (Sekoutoure), Kigoma (Maweni), Rukwa (Sumbawanga), Tabora (Kitete) na Mwanza (Ukerewe);

v. Kukamilika kwa ujenzi wa Hospitali mpya 135 za Halmashauri, Vituo vya Afya 390, maboma ya Zahanati 980, mitambo 21 ya kuzalisha hewa tiba ya oksijeni kwa ajili ya wagonjwa mahututi na Wagonjwa wa dharura, nyumba za Watumishi 270 na ukarabati wa Hospitali Kongwe 50 za Halmashauri;

vi. Kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya kutoa huduma za afya ya Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Kanda-Meta iliyopo katika Jiji la Mbeya na Hospitali za Rufaa za Mikoa ambazo ni Sekou Toure (Mwanza), Geita, Simiyu, Mawenzi, Njombe na Songwe;

vii. Kuongeza hospitali zenye majengo ya kutolea Huduma za Dharura (EMD) kutoka 7 hadi 125 mwaka 2025 (Ngazi ya Msingi EMD 87 na Ngazi ya Rufaa EMD 31). Ujenzi huo umechangia kupunguza vifo na kuokoa maisha kwa wagonjwa wa dharura na ajali; na

viii. Kuongeza zahanati binafisi kutoka 2,106 mwaka 2020 hadi 2,272 mwaka 2025, vituo vya afya binafsi kutoka 323 hadi 349; na hospitali binafsi kutoka 173 hadi 212.

### 3.2.2 Huduma za Mama na Mtoto

i. Kuongeza idadi ya vituo vyenye uwezo wa kutoa huduma za upasuaji wa dharura wa kumtoa mtoto tumboni (CEmONC) kutoka vituo 340 mwaka 2020 hadi 577 na wodi/vyumba maalum kwa ajili ya Huduma za Watoto Wachanga Wagonjwa (NICU) kutoka 80 mwaka 2020 hadi 362 mwaka 2025. Kuimarika kwa huduma za uzazi, mama na mtoto kumesaidia kupunguza vifo vya kinamama vitokanavyo na uzazi kwa kiwango kikubwa kutoka vifo 556 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2020 hadi 104 kwa kila vizazi hai 100,000 mwaka 2025;

ii. Kuongeza vituo vya kutolea huduma za afya vyenye majengo ya mama na mtoto kutoka 6,081 mwaka 2020 hadi 7,397 mwaka 2025. Pia, vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano vimepungua kutoka 67 mwaka 2020 hadi 43 mwaka 2025;

iii. Kuanzisha mfumo wa *National Emergency Medical Services (NEMS)* kwa ajili ya kuhudumia na kusafirisha dharura za uzazi na watoto, majeruhi wa ajali na dharura nyingine za afya kwa kutumia magari ya wagonjwa *(ambulance)* yaliyounganishwa katika mfumo wa kielektoniki. Mfumo huu unahakikisha magari ya wagonjwa yanapatikana kwa haraka wakati wa ajali za barabarani au dharura nyingine za afya ikiwemo wajawazito na watoto, magonjwa ya moyo na Kiharusi yanayoweza kutokea katika jamii na kuhudumiwa na watoa huduma wenye ujuzi wakati wa kusafirishwa. Aidha, hadi kufikia mwaka, 2025 wanufaika wa huduma za dharura za rufaa za mama na mtoto kupitia mfumo wa m-mama wameongezeka kutoka 46,941 mwaka 2023 hadi 144,237 mwaka 2025, ambapo kati ya hao akina mama walikuwa 117,690 ikilinganishwa na akina mama 38,560 mwaka 2023, watoto wachanga 26,272 ikilinganishwa na 8,273 mwaka 2023 na mama pamoja na mtoto, kwa pamoja walikuwa 275 ikilinganishwa na 108 mwaka 2023; na

iv. Kuongeza vituo vya kutolea huduma jumuishi kwa manusura wa vitendo vya ukatili wa Kijinsia na Ukatili dhidi ya watoto katika ngazi mbalimbali za vituo vya kutolea huduma za afya nchini kutoka vituo 4 mwaka 2020 hadi 31 mwaka 2025.

### 3.2.3 Dawa, Vifaa na Vifaa Tiba

i. Kuongeza vitanda vya wagonjwa katika vituo vya kutolea huduma za afya nchini kutoka vitanda 104,687 mwaka

2021 hadi 153,683 Aprili, 2025. Ongezeko la vitanda vya wagonjwa limesaidia kuongeza ubora na ufanisi wa huduma za afya hususani huduma za afya ya mama na mtoto. Vilevile, idadi ya vitanda katika vituo vya umma kwa ajili ya wagonjwa mahututi (ICU) imeongezeka kutoka vitanda 185 vya mwaka 2021 hadi 1,362 mwaka 2025. Ongezeko hili limejumuisha vitanda vya wodi za watoto wachanga (NICU);

ii. Kuongeza upatikanaji wa vifaa tiba ikiwemo MRI kutoka 7 hadi 13, CT Scan 13 hadi 45, Mini Angio Suite 4 hadi 5, Fluoroscopy 9 hadi 13, Digital X-Ray 147 hadi 559, Ultrasound 476 hadi 970 na Oxygen Plant 25; na

iii. Kuimarika kwa hali ya upatikanaji wa dawa na bidhaa za Afya aina 382 katika vituo vya kutolea huduma za afya vya umma kutoka asilimia 73 mwaka 2020 hadi asilimia 86.2 Aprili 2025. Upatikanaji wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi umewezesha wananchi kupata mahitaji yote muhimu ya msingi ya kimatibabu pale anapoenda kupata huduma katika vituo vya kutolea huduma za afya.

### 3.2.4 Huduma za Kibingwa na Ubingwa Bobezi

i. Kuimarika kwa huduma za kibingwa na ubingwa bobezi ambapo hivi sasa huduma nane zinapatikana hadi ngazi ya hospitali za rufaa za mikoa ambazo awali zilikuwa zinapatikana katika ngazi ya kanda. Huduma hizo ni afya ya uzazi na magonjwa ya wanawake, afya ya watoto, magonjwa ya ndani, upasuaji, upasuaji mifupa na ajali, huduma za dharura, huduma za mionzi, huduma za ganzi na dawa za usingizi. Hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi vya kisasa na bidhaa za afya imeimarika kutoka asilimia 73 mwaka 2020 hadi asilimia 89.3 mwaka 2025;

ii. Kuboresha huduma za ubingwa na ubingwa bobezi katika Hospitali ya Taifa, Hospitali Maalum, Hospitali za Kanda na Hospitali za Rufaa za Mikoa umewezesha wagonjwa 12,684 kupata huduma hizo. Huduma hizo ni pamoja na uwekaji wa vifaa vya usikivu kwa watoto; upandikizaji wa figo; kuwekewa puto tumboni; upasuaji mgumu wa moyo bila kufungua kifua; upasuaji wa moyo kwa kufungua kifua; Upasuaji ubongo; Upasuaji wa uti wa mgongo; Upandikizaji wa nyonga bandia; Tiba ya saratani za mlango wa kizazi, matiti, umio, ngozi na tezi dume; upasuaji wa goti bandia; upasuaji wa ubongo kwa njia ya matundu; upasuaji wa vichwa vikubwa na mgongo wazi; upasuaji wa kiuno; na upasuaji wa magoti kwa njia ya matundu;

iii. Kuvutia wagonjwa mbalimbali kutoka nje ya nchi (Tiba utalii) ambapo wagonjwa hao waliongezeka kutoka 5,705 hadi 12,180 mwaka 2025 kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanyika katika kuboresha huduma za kibigwa na ubingwa bobezi nchini. Wagonjwa hao walitoka katika nchi za Comoro, Malawi, Burundi, Zambia, Congo DRC, Uganda, Zimbabwe na Kenya. Aidha, Wagonjwa hao walihudumiwa katika Hospitali 6 ambazo ni Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Taasisi ya Saratani ya Ocean Road, Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete, Taasisi ya Mifupa MOI, Aga khan na Saifee.

## 3.3 Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

Serikali imewezesha utekelezaji wa afua mbalimbali zinazohusu ustawi na maendeleo ya jamii ili kuleta maendeleo jumuishi na endelevu. Katika kutekeleza afua hizo, yafuatayo ni mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2020 hadi mwaka 2025:

i. Kuongeza miradi ya maendeleo yenye ushiriki wa wananchi kutoka miradi 1,257 hadi miradi 72,911 mwaka 2025. Miradi ambayo wananchi walishiriki ni pamoja na ujenzi wa madarasa ya awali na shule za msingi 45,162, ujenzi wa madarasa ya sekondari 18,762 na ujenzi wa Zahanati na vituo vya afya 8,987. Ongezeko hili ni matokeo ya utekelezaji wa Kampeni ya "Amsha Ari" katika kutekeleza Mpango wa Taifa wa Kuhamasisha na Kusimamia Maendeleo Ngazi ya Msingi wa Mwaka 2022/2023 – 2025/2026 uliojikita katika kuwezesha jamii kushiriki kwenye miradi ya maendeleo;

ii. Kuongeza ujenzi wa nyumba bora na gharama nafuu katika maeneo yenye makazi duni kutoka nyumba 5,002 mwaka 2020 hadi nyumba 14,352 mwaka 2025. Ongezeko hilo limetokana na kampeni endelevu ya ujenzi wa nyumba bora iliyobebwa na kauli mbiu "Piga Kazi, Boresha Makazi". Ujenzi wa makazi bora unasaidia kuimarisha afya na kuboresha uchumi wa kaya;

iii. Kuongeza Mabaraza ya Watoto kutoka 171 mwaka 2020 hadi 1,460 mwaka 2025. Mabaraza hayo yanalenga kuwashirikisha watoto katika masuala yanayowahusu ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa haki ya mtoto. Kupitia mabaraza hayo watoto wameshiriki mambo mbalimbali ikiwemo kutoa maoni katika uandaaji wa Rasimu Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2050;

iv. Kuongeza vikundi vya malezi chanya vyenye lengo la kuwafikia wazazi/ walezi kutoka 3,567 mwaka 2020 hadi 4,063 mwaka 2025. Katika kuimarisha matunzo kwa watoto, elimu ya malezi na matunzo imetolewa kwa wazazi na walezi 35,860 mwaka 2025 ikilinganishwa na wazazi 920 mwaka 2020. Mafunzo hayo yanasaidia kuimarisha ulinzi, makuzi na maendeleo ya mtoto;

v. Kuongeza madawati ya ulinzi na usalama wa mtoto katika shule za msingi na sekondari kutoka madawati 100 mwaka 2020 hadi 4,082 mwaka 2025. Madawati hayo yamesaidia watoto kutoa taarifa zenye viashiria vya ukatili na ukatili dhidi yao ndani na nje ya shule;

vi. Kuongeza utoaji taarifa za matukio kwa jamii dhidi ya vitendo vya ukatili kwa watoto kutoka 2,396 mwaka 2020 hadi 32,735 mwaka 2025. Ongezeko hilo limetokana na kuimarishwa kwa mifumo ya utoaji taarifa na uelewa wa jamii juu ya aina zote za madhara ya ukatili ili kufikisha mashauri hayo katika vyombo vya Sheria na kupatiwa ufumbuzi;

vii. Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003, Toleo la Mwaka 2024 ambayo imelenga kuimarisha upatikanaji wa huduma za matunzo, ustawi na ulinzi kwa wazee katika jamii na taasisi mbalimbali;

viii. Kuongezeka kwa watoto wanaopatiwa huduma ya malezi ya kambo kutoka 67 mwaka 2020 hadi 217 mwaka 2025. Ongezeko hilo limetokana na utoaji wa elimu pamoja na kuwapata walezi wa kambo wa kuaminika na watoto kuunganishwa na familia zao;

ix. Kuongeza utambuzi wa watoto walio katika mazingira hatarishi na kupatiwa huduma kutoka 703,695 mwaka 2020 hadi 1,941,848 mwaka 2025. Utambuzi huo umewezesha watoto kupata huduma za msingi ikiwa ni pamoja na afya, elimu, malazi na chakula;

x. Kuongeza madawati ya kushughulikia masuala ya jinsia kutoka matano (5) mwaka 2020 hadi 600 mwaka 2025.

Kati ya hayo, madawati 362 yameanzishwa katika taasisi za elimu ya juu na elimu ya kati na madawati

238 yameanzishwa katika maeneo ya Umma hususan sokoni katika mikoa 16. Madawati hayo yametoa elimu ya masuala ya jinsia, ulinzi wa wahanga wa ukatili wa kijinsia pamoja na kushughulikia mashauri mbalimbali ya vitendo vya ukatili wa kijinsia kwa kushirikiana na vyombo husika; na

xi. Kuongeza usajili wa Mashirika Yasiyo ya Kiserikali kutoka 1,003 mwaka 2020 hadi 10,767 mwaka 2025. Kati ya hayo, mashirika ya kimataifa ni 660, kitaifa ni 9,070, mkoa ni 452 na wilaya ni mashirika 585. Mashirika hayo yameongeza mchango katika maendeleo ya Taifa kutoka shilingi trilioni 1.1 mwaka 2020 hadi shilingi trilioni 7.46 mwaka 2025 uliowezesha kutekeleza afua mbalimbali zikiwemo afya, hifadhi ya jamii, uwezeshaji wa jamii, kilimo, elimu, utawala bora, mazingira, maji, jinsia na haki za binadamu. Mchango huo umezalisha takriban ajira 37,490 kwa wananchi.

## 3.4 Maji

Serikali imeendelea kusimamia rasilimali za maji kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa kutekeleza mikakati na programu mbalimbali. Vilevile, imeendelea kujumuisha wadau mbalimbali katika kuboresha huduma za upatikanaji wa maji mijini na vijijini. Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha mwaka 2020 hadi mwaka 2025 ni pamoja na:

i. Kutekeleza jumla ya miradi 2,331 ya usambazaji wa maji mijini na vijijini ikiwemo:

    a) Mradi wa majisafi na usafi wa mazingira Arusha uliogharimu zaidi ya shilingi bilioni 520. Mradi huu umeongeza uzalishaji wa maji kutoka lita milioni 40 hadi lita milioni 200 kwa siku na hivyo kuwezesha huduma maji safi kupatikana kwa asilimia 100. Vilevile, kuongeza huduma ya uondoaji wa majitaka

kutoka asilimia 7.6 hadi asilimia 30;

b) Mradi wa kutoa maji Ziwa Victoria kupeleka Miji ya Tinde na Shelui kwa gharama ya shilingi bilioni 24.75. Mradi huo, unanufaisha wananchi wapatao 86,980 wa miji hiyo;

c) Mradi wa ujenzi wa chujio la Butimba kwa gharama ya Euro 31,172,568.93 ambao umeboresha hali ya upatikanaji wa huduma za maji kwa wakazi wapatao 450,000 Jijini Mwanza;

d) Mradi wa Maji Same – Mwanga - Korogwe ambao umeanza kutoa huduma ya maji katika Miji ya Same na Mwanga pamoja na vijiji 43 vya Wilaya za Same, Mwanga na Korogwe ambapo zaidi ya wananchi 456,930 wanapata huduma ya majisafi;

e) Mradi wa Maji wa Mugango – Kiabakari – Butiama kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 30.69. Mradi huo unahudumia maeneo ya Mugango, Kiabakari, Butiama pamoja na vijiji vilivyopo ndani ya kilomita 12 ambao utanufaisha wananchi wapatao 100,000;

f) Mradi wa maji wa Orkesumet kwa gharama ya shilingi bilioni 38.11 ambapo wakazi wapatao 52,000 pamoja na mifugo yao wananufaika na huduma ya majisafi;

g) Kukamilika kwa uchimbaji wa visima 1,749 na mabwawa 16 kujengwa kwa ajili ya kutoa huduma ya maji katika maeneo mbalimbali nchini;

h) Kununua seti 25 za mitambo ya uchimbaji wa visima, seti tano (5) za mitambo ya ujenzi wa mabwawa na seti nne (4) za utafiti wa maji chini ya ardhi;

i) Kuendelea na utekelezaji wa mradi wa maji wa miji 28 unaogharimu shilingi trilioni 1.6 ambao

ukikamilika utakuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao 5,985,500;

j) Kuendelea na ujenzi wa Bwawa la Kidunda linalogharimu Shilingi bilioni 329.47 kwa ajili ya kuimarisha huduma ya maji katika Mkoa wa Dar es Salaam na baadhi ya maeneo ya Mkoa wa Pwani ambao ukikamilika utakuwa na uwezo wa kuhudumia wananchi wapatao 11,387,700;

k) Kuendelea na ujenzi wa mradi wa maji wa Tunduma - Vwawa kwa gharama ya shilingi bilioni 119.95 ambao ukikamilika utahudumia wananchi wapatao 219,300 wa miji ya Tunduma, Vwawa na Mlowo;

l) Kuendelea na ujenzi wa Mradi wa Maji Ruangwa, Lindi hadi Nachingwea wenye thamani ya Shilingi bilioni 107 utakaohudumia vijiji 34 na kunufaisha wananchi wapatao 35,000;

m) Kuendelea na ujenzi wa mradi wa maji kutoka Kahama kwenda Halmashauri ya Ushetu wenye thamani ya Shilingi bilioni 42 utakaohudumia vijiji 57 na kunufaisha wananchi wapatao 234,455;

n) Kuendelea na ujenzi wa mradi wa maji kutoka Dambia kwenda Hydom Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu wenye thamani ya Shilingi bilioni 41 utakaohudumia vijiji 21 na kuwanufaisha wananchi 52,000; na

o) Kuendelea na ujenzi wa Mradi wa Maji Ukirigulu, Koromije hadi Sumve wenye thamani ya Shilingi bilioni 32 utakaonufaisha vijiji 19 na kuhudumia wananchi 85,468.

ii. Kutekeleza programu ya malipo kwa matokeo katika sekta ya maji kwa kuongeza fedha za utekelezaji wa miradi ya

maji na usafi wa mazingira vijijini kutoka Dola za Marekani milioni 350 mwaka 2020 hadi Dola za Marekani milioni 654 mwaka 2025 na hivyo kunufaisha jumla ya vijiji 1,347;

iii. Kuongeza maeneo ya vyanzo vya hifadhi ya maji vilivyotangazwa kutoka vyanzo 18 mwaka 2020 hadi 68 mwaka 2025. Kutangazwa kwa maeneo ya vyanzo hivyo kumeimarisha uwekaji wa mipaka na uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji nchini;

iv. Kuongeza maabara za ubora wa maji nchini zenye hadhi ya ithibati ya kimataifa kutoka maabara moja (1) mwaka 2021 hadi saba (7) ambazo zipo katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mwanza, Singida, Shinyanga, Musoma, Kigoma na Kagera. Hadhi hiyo, inadhihirisha kuwa matokeo yanayotolewa na maabara hizo yanakubalika kimataifa pamoja kuongeza wigo wa uchunguzi wa viashiria vya ubora wa maji; na

v. Kukamilika kwa maandalizi ya Sera ya Taifa ya Maji ya Mwaka 2002,Toleo la Mwaka 2025. Sera hiyo imelenga kuongeza upatikanaji wa maji, kuimarisha ulinzi wa vyanzo vya maji na kutambua umuhimu wa sekta binafsi katika ulinzi na upatikanaji wa maji.

Kutokana na jitihada mbalimbali zilizochukuliwa katika sekta ya maji, hali ya upatikanaji wa maji imeimarika kutoka wastani wa asilimia 70.1 mwaka 2020 hadi asimilia 83 mwaka 2025 kwa maeneo ya vijijini na wastani wa asilimia 84 mwaka 2020 hadi asilimia 91.6 mwaka 2025 katika maeneo ya mijini. Pia, upatikanaji wa maji safi na salama umesaidia kuongeza shughuli za uzalishaji na kupunguza magonjwa ya mlipuko.

# SURA YA NNE

## 4. SEKTA ZA UZALISHAJI

### 4.1 Kilimo

Sekta ya kilimo nchini ni muhimu sana kwa uchumi na maisha ya watanzania kutokana na mchango wake katika uzalishaji wa ajira na mazao ya chakula, biashara na malighafi za viwandani. Sekta hii inachangia zaidi ya asilimia 26.2 ya Pato la Taifa (GDP) na inaajiri zaidi ya asilimia 65 ya nguvu kazi yote. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imeendelea kuboresha sekta hii kupitia mipango mbalimbali kama vile kuongeza matumizi ya teknolojia, kuboresha miundombinu, na kutoa mikopo kwa wakulima ili kuwa na kilimo chenye tija na endelevu. Katika Awamu ya Sita, Serikali imeongeza bajeti ya kilimo kutoka shilingi bilioni 294 mwaka 2021/2022 hadi shilingi trilioni 1.24 mwaka 2024/2025. Kuongezeka kwa bajeti kumewezesha kutekeleza mikakati ya uendelezaji wa kilimo na kufikia mafanikio mbalimbali ikiwemo:

#### 4.1.1 Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II)

Kukamilika kwa mapitio na uhuishaji wa Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II) kwa muhula wa mwisho utakaokamilika mwaka 2030. Katika mapitio hayo, masuala mbalimbali yalibainika ikiwemo kufikiwa kwa malengo ya awali kwa asilimia 66 na kuongezeka kwa bajeti ya maendeleo.

#### 4.1.2 Uzalishaji wa Mazao ya Chakula na Biashara

Serikali katika uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara nchini imepata mafanikio yafuatayo:

i. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula kutoka tani 17,148,290 mwaka 2021 hadi tani 22,803,316 mwaka 2024. Ongezeko hilo limewezesha kuongeza utoshelevu wa chakula nchini kufikia asilimia 128 ikilinganishwa na utoshelevu wa asilimia 125 mwaka 2021;

ii. Kuongeza tija ya uzalishaji wa zao la mahindi kutoka tani 1.7 mwaka 2020 hadi tani 2 mwaka 2024, mpunga kutoka tani 3 mwaka 2020 hadi tani 4 mwaka 2024 na maharage kutoka tani 1.1 hadi tani 1.6 kwa hekta mwaka 2024. Ongezeko hili linatokana na matumizi ya pembejeo bora za kilimo na kuimarika kwa huduma za ugani;

iii. Kuongeza uzalishaji wa mazao asilia ya biashara kutoka tani 983,177 mwaka 2021 hadi tani 1,443,629.4 mwaka 2024. Mathalan, uzalishaji wa korosho umeongezeka kutoka tani 240,158 mwaka 2021 hadi tani 528,263.82 mwaka 2024;

iv. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya mbegu za mafuta kutoka tani 1,713,178 mwaka 2021 hadi tani 2,143,098.70 mwaka 2024. Kwa mfano, uzalishaji wa alizeti umeongezeka kutoka tani 425,653.1 mwaka 2021 hadi tani 1,217,025.51 mwaka 2024; na

v. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya bustani kutoka tani 7,304,722.5 mwaka 2021 hadi tani 7,513,026.83 mwaka 2024. Mathalan, uzalishaji wa parachichi zinazouzwa nje ya nchi umeongezeka kutoka tani 17,711.49 mwaka 2021 hadi tani 35,627.02 mwaka 2024.

### 4.1.3 Upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo

Katika uboreshaji na upatikanaji wa pembejeo bora za kilimo ili kuhakikisha kilimo chenye tija, Serikali imepata mafanikio yafuatayo:

i. Kuongezeka kwa upatikanaji wa mbegu bora kutoka tani 50,747 mwaka 2021 hadi tani 72,031.89 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 41.9. Aidha, uzalishaji wa mbegu bora ndani ya nchi umeongezeka kutoka tani 34,797 mwaka 2021 hadi tani 56,114 mwaka 2024;

ii. Kuwezesha maabara ya mbegu ya Taasisi ya Kudhibiti Ubora wa Mbegu (TOSCI) kupata ithibati ya kimataifa ya uzalishaji mbegu. Hatua hii imewezesha uzalishaji wa mbegu bora unaoleta tija kwa wakulima;

iii. Kutoa ruzuku ya mbegu za mazao ya alizeti tani 2,197 na ngano tani 2,421.55 pamoja na kusambaza miche ya chikichi 4,710,351 kupitia mpango wa ruzuku;

iv. Kuongezeka kwa upatikanaji wa mbolea kutoka tani 678,017 mwaka 2021 hadi tani 1,213,729 mwaka 2025. Aidha, ruzuku ya mbolea yenye thamani ya shilingi bilioni 300 ilitolewa kwa mazao yote. Upatikanaji wa mbolea umewezesha uzalishaji wenye tija kwa mazao ya biashara na chakula, kuihakikishia nchi usalama wa chakula pamoja na fedha za kigeni kutokana na uuzaji wa mazao ya biashara;

v. Kuwezesha uanzishaji wa kiwanda cha kuchanganya mbolea cha ITRACOM chenye uwezo wa kuchanganya tani 1,000,000 kwa mwaka. Vilevile, imeiwezesha Kampuni ya Mbolea Tanzania (Tanzania Fertilizer Company – TFC) mtaji wa shilingi bilioni 116 kwa ajili ya kununua na kusambaza mbolea na hivyo kusaidia kupunguza changamoto ya upungufu wa mbolea nchini;

vi. Kuanzisha vituo 45 vyenye jumla ya matrekta 500 vya kutoa huduma ya zana za kilimo kwa wakulima wadogo kwa gharama nafuu katika mikoa 15 (Dodoma, Singida, Tabora, Shinyanga, Simiyu, Mara, Mwanza, Kigoma,

Geita, Katavi, Mbeya, Ruvuma, Njombe, Morogoro na Tanga). Hatua hiyo imewezesha kupunguza gharama za uzalishaji na kuchangia katika kuongeza tija ya uzalishaji katika mnyororo mzima wa uzalishaji mazao; na

vii. Kujenga Maabara ya Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania kwa ajili ya kupima ubora wa mbolea, Maabara ya kuzalisha miche kwa njia ya chupa (Tissue Culture) kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa miche bora ya Mkonge na kukarabati maabara ya udongo ya TARI Mlingano kwa ajili ya kupima afya ya udongo.

### 4.1.4 Masoko ya Mazao ya Kilimo

Serikali imeendelea kuweka mazingira wezeshi kwa ajili ya kuhakikisha masoko ya mazao yanapatikana ndani na nje ya nchi na kuwanufaisha wakulima. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya mazao ya kilimo nje ya nchi kutoka Dola za Marekani bilioni 2.1 mwaka 2021 hadi Dola za Marekani bilioni 3.5 mwaka 2024. Hatua hiyo imeongeza mchango wa Sekta ya Kilimo katika fedha za kigeni kutoka asilimia 25 mwaka 2021 hadi asilimia 30 mwaka 2025;

ii. Kuimarisha mifumo ya masoko ya mazao ya kilimo ikiwemo kufanya minada kidigitali kupitia Soko la bidhaa Tanzania (Tanzania Mercantile Exchange – TMX), kuuza katika soko la moja kwa moja na kilimo cha mikataba. Hatua hii imeimarisha bei za mazao ya kilimo na kuleta manufaa kwa wakulima. Bei zilizoongezeka ni pamoja na zao la korosho ambayo imeongezeka kutoka shilingi 1,750 kwa kilo mwaka 2020 hadi shilingi 4,195 kwa kilo mwaka 2024; Kahawa aina ya Arabica kutoka shilingi 4,500 kwa kilo mwaka 2020 hadi shilingi 8,500 kwa kilo

mwaka 2024; na Tumbaku kutoka shilingi 4,475 kwa kilo mwaka 2020 hadi shilingi 6,183 kwa kilo mwaka 2024; na

iii. Kufungua masoko 10 kwa ajili ya mazao ya nafaka, bustani, mikunde na Tumbaku ambapo hati za ufikiaji wa masoko ya mazao ya kilimo tisa (9) zimekabidhiwa balozi 13 za China (vanila na nanasi); India (vanila na nanasi); Indonesia (karafuu) Singapore (karafuu); Israeli (parachichi); Malaysia (parachichi); Canada (pilipili manga); Uturuki (nanasi); Brazili (nanasi); Marekani (kakao); Afrika Kusini (ndizi); Zambia (viazi mviringo); Pakistan (tumbaku).

### 4.1.5 Kuimarisha Huduma za Ugani

Serikali imeimarisha utoaji wa huduma za ugani kwa kununua na kusambaza pikipiki 6,444, vishikwambi 5,443, visanduku vya ugani 1,000, na *Soil scanner* 143 kwa Maafisa Ugani. Aidha, nyumba 50 kwa ajili ya makazi ya Maafisa Ugani zimejengwa ili kuwawezesha Maafisa hao kuwa karibu na wakulima. Hatua hii imeongeza tija na uzalishaji wa mazao nchini.

### 4.1.6 Uzalishaji wa Sukari

Serikali imeimarisha upatikanaji wa sukari nchini kwa kuratibu ujenzi wa kiwanda cha sukari cha Bagamoyo chenye uwezo wa kuzalisha sukari tani 35,000; ujenzi wa kiwanda cha sukari cha Mkulazi chenye uwezo wa kuzalisha sukari tani 50,000; upanuzi wa mashamba ya Mtibwa (hekta 4,700) na Kagera (hekta 9,071); na upanuzi wa kiwanda cha Kilombero kitakachozalisha tani 271,000. Hatua hii, imeongeza uzalishaji wa sukari kutoka tani 311,358 mwaka 2020 hadi tani 392,724 mwaka 2024.

### 4.1.7 Miundombinu ya Uhifadhi wa Chakula

Katika kuimarisha uwekezaji wa miundombinu ya uhifadhi wa chakula mafanikio yafuatayo yamepatikana:

i. Kukamilika kwa ujenzi wa maghala 46 na vihenge 20 vyenye uwezo wa kuhifadhi mazao tani 219,921 na hivyo kuchangia juhudi za Serikali za kupunguza upotevu wa mazao baada ya mavuno; na

ii. Kuanzisha mfumo wa usajili wa maghala na wanunuzi wa mazao ya kilimo *(Crop Stock Dynamics System – CSDS)* kwa ajili ya kutambua idadi ya maghala na hifadhi ya chakula iliyopo nchini. Lengo la usajili huo ni kutambua idadi ya maghala ya sekta za umma na binafsi na kiasi cha mazao kilichohifadhiwa kwa lengo la kuimarisha usalama wa chakula na lishe.

### 4.1.8 Kilimo cha Umwagiliaji

Kwa upande wa kilimo cha umwagiliaji, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuongeza kwa eneo la umwagiliaji kutoka hekta 694,715 mwaka 2020 hadi hekta 983,466.06 mwaka 2024, kulikochangiwa na ongezeko la miradi ya umwagiliaji kutoka 13 mwaka 2020 hadi 780 mwaka 2025;

ii. Kuongeza tija ya uzalishaji wa mazao katika maeneo ya umwagiliaji mathalan tija ya uzalishaji wa mpunga imeongezeka kutoka wastani wa tani 1.8 - 2.0 kwa hekta hadi kufikia wastani wa tani 4.0 – 5.0 kwa hekta, mahindi kutoka tani 1.5 hadi tani 3.7- 5.0 kwa hekta, vitunguu kutoka tani 13 hadi 26 kwa hekta, na nyanya kutoka tani 5 hadi 18 kwa hekta;

iii. Kuongezeka kwa vyama vya umwagiliaji vilivyosajiliwa kutoka 175 mwaka 2020 hadi 898 mwaka 2025 na hivyo kuimarisha tasnia ya umwagiliaji katika kusimamia na kutunza miundombinu ya umwagiliaji ili kuhakikisha uendelevu wa miundombinu ya umwagiliaji; na

iv. Kununua mitambo 30 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa miradi ya umwagiliaji, kununua mitambo 17 kwa ajili ya uchimbaji wa visima virefu na vya kati kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji, na kununua magari 66 na pikipiki 23 kwa ajili ya usimamizi wa shughuli mbalimbali za umwagiliaji.

### 4.1.9 Ushirika

Serikali imeimarisha ushirika nchini na kupata mafanikio yafuatayo:

i. Kuanzisha Benki ya Taifa ya Ushirika kwa mtaji wa shilingi bilioni 58. Benki hiyo itawezesha vyama vya ushirika kufanya biashara, kupata mikopo yenye riba nafuu, kujiendesha kibiashara na kuwalinda wanaushirika wakiwemo wakulima kutokana na Taasisi za Fedha kutoa mikopo yenye riba kubwa;

ii. Kuongezeka kwa ajira katika vyama vya ushirika ambapo wananchi walioajiriwa katika vyama hivyo wamefikia 155,106 mwaka 2025 ikilinganishwa na wananchi 100,100 waliopata ajira katika mwaka 2020;

iii. Kuongezeka kwa viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika kutoka 267 mwaka 2021 hadi 331 mwaka 2025. Shughuli zinazofanywa na viwanda hivi ni uchambuaji wa pamba; ukoboaji wa mpunga, kahawa na mahindi; usindikaji wa maziwa; ukamuaji wa mafuta ya pamba, alizeti, karanga na ufuta; na ubanguaji wa korosho;

iv. Kuongezeka kwa mauzo ya mazao kutoka tani 591,268.122 zenye thamani ya shilingi trilioni 1.1 mwaka 2021 hadi tani 2,225,397.56 zenye thamani ya shilingi trilioni 4.2 mwaka 2025. Mafanikio hayo yametokana na kuimarika kwa matumizi ya mifumo rasmi ya masoko ya mazao ya wakulima kupitia vyama vya ushirika;

v. Kuongezeka kwa akiba na mikopo katika SACCOS kutoka shilingi bilioni 576.0 mwaka 2021 kufikia shilingi bilioni 966.9 mwaka 2024, na hivyo kuongeza mikopo iliyotolewa kwa wanachama wa SACCOS kutoka shilingi bilioni 798.0 mwaka 2021 hadi shilingi trilioni 1.1 mwaka 2024;

vi. Kuongezeka kwa vyama vya ushirika vilivyopata Hati safi kutoka 339 mwaka 2021 hadi 631 mwaka 2024. Hali hii inaashiria kuwa utendaji wa vyama vya ushirika inaendelea kuimarika; na

vii. Kuanzisha Mfumo wa Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (MUVU) ambao umeunganishwa na Mifumo ya Taasisi tisa (9) ambayo ni Mfumo Mkuu Unganishi wa Serikali (GovESB), Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimali (ERMS), Mfumo wa Ukusanyaji wa Malipo ya Serikali Kielektroniki (GePG), Mfumo wa Wizara ya Kilimo (e-Kilimo), Mfumo wa Mizani ya Kidigitali (Mkulima Hub), Mfumo wa Mfuko wa Bima ya Afya (NHIF), Mfumo wa Bodi ya Sukari (CANGROWERS-MIS), Mfumo wa ELCT ND SACCOS na Mfumo wa Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA). Aidha, mpaka sasa Vyama 6,634 vimesajiliwa kwenye MUVU ambapo Vyama vya msingi ni 6,117, Vyama vya Upili ni 75, vyama vya Awali ni 441 na Shirikisho ni kimoja (1)

### 4.1.10 Programu ya Jenga Kesho Iliyobora (*Building Better Tomorrow – BBT)*

Programu hii ilizinduliwa mwaka 2023 kwa lengo la kuzalisha ajira zenye staha; kuongeza uzalishaji na tija; kuimarisha usalama wa chakula nchini; kuongeza mchango wa sekta ya kilimo kwenye Pato la Taifa (GDP); na kuimarisha hali ya maisha ya jamii ya Watanzania kwa ujumla. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kutenga mashamba yenye ukubwa wa ekari 340,244.98 na kuendeleza mashamba mawili yaliyopo Dodoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino (Chinangali na Ndogowe);

ii. Kutoa mafunzo kwa vijana na wanawake 686 kuhusu mbinu bora za kilimo na biashara pamoja na upatikanaji wa mitaji na masoko;

iii. Kuanzisha vituo 16 vya BBT pamoja na kusambaza matrekta 100 na vifaa vyake ili kuongeza tija katika uzalishaji katika maeneo ya Mwanza (Ukiriguru); Tabora (Tumbi na Nzega); Morogoro (Kilosa na Ifakara); Tanga (Mheza na Korogwe); Njombe (Lugenge); Dodoma (Mtanana na Ndogowe/Mlazo); Mbeya (Mbarali); Simiyu (Itilima); Ruvuma (Madaba);

iv. Kuanzisha BBT – *Agricultural Extension Enterpreneurship Scheme* (BBT – Ugani) ambayo inalenga kukuza ujuzi wa vijana wahitimu wa vyuo vya kilimo kwa kutumika kutoa ushauri wa kitaalam (huduma za ugani) kwa wakulima ambapo jumla ya vijana 1,240 wamenufaika. Aidha, Serikali imeajiri vijana 740 na kusambazwa katika kata 250 zinazozalisha zao la Pamba kwenye Mikoa ya Shinyanga, Tabora, Simiyu, Mara, Mwanza na Pwani kwa ajili ya kutoa huduma za ugani kwa wakulima wa Pamba; na

v. Kuzalisha ajira 120,111 kupitia Programu ya Jenga Kesho Iliyobora – BBT katika ya mwaka 2023 hadi 2025.

### 4.1.11 Kukabiliana na Milipuko ya Visumbufu vya Mazao

Serikali imeendelea kuimarisha uwezo wa ndani wa kukabiliana na milipuko ya visumbufu vya mimea na mazao ambapo mafanikio yafuatayo yamepatikana:

i. Kununua ndege moja maalum ya kunyunyizia viuatilifu na ndege nyuki 41 kwa ajili ya uchunguzi na udhibiti wa visumbufu vya mimea na mazao; na

ii. Kupata Ithibati ya Kimataifa kwa Maabara ya Mamlaka ya Mimea na Viuatilifu Tanzania (TPHPA) ambayo imewezesha mazao yanayozalishwa Tanzania kupimwa na maabara hiyo kwa kuzingatia matakwa ya soko la Kimataifa.

#### 4.1.12 Mikopo ya Kilimo

Katika utoaji wa mikopo ya kilimo mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwemo yafuatayo:

i. Kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo nafuu kwa wakulima kupitia Benki ya Maendeleo ya Kilimo (TADB) ambapo dhamana ya mikopo imeongezeka kutoka shilingi bilioni 63 mwaka 2020 hadi shilingi bilioni 418.3 mwaka 2025 ambayo imeongeza wakulima walionufaika kutoka 8,327 hadi 28,788. Mikopo hiyo ni kwa ajili ya utekelezaji miradi iliyo katika mnyororo wa thamani wa kilimo ikiwemo ununuzi wa mazao na uchakataji, usambazaji wa pembejeo za kilimo na ununuzi wa zana za kilimo kama matrekta na mitambo ya kuvuna mazao;

ii. Kuanzisha utaratibu wa kutoa mikopo yenye riba nafuu ya asilimia 4.5 kwa vijana na wanawake kupitia Mfuko wa Pembejeo za Kilimo *(Agricultural Input Trust Fund - AGITF)* ambapo mikopo iliyotolewa kwa kipindi cha 2020 hadi 2025 ni shilingi bilioni 5.49;

iii. Taasisi za fedha kupunguza riba kutoka asilimia 22 hadi asilimia 9 ili kuwawezesha wakulima kupata mitaji yenye riba nafuu. Hatua hii imewezesha mikopo yenye riba nafuu kwa vijana na wanawake waliopo kwenye shughuli

za kilimo na uongezaji thamani mazao kutoka shilingi bilioni 2 mwaka 2023 hadi shilingi bilioni 5 mwaka 2025; na

iv. Kuanzisha Mfuko wa Maendeleo ya Kilimo kwa ajili ya kuendeleza kilimo kwa kupunguza ukali wa bei za mazao zinaposhuka, kutoa ruzuku ya pembejeo za kilimo, kuimarisha miundombinu ya uhifadhi, utafiti na uongezaji wa thamani.

## 4.2 Mifugo na Uvuvi

Sekta ya Mifugo na Uvuvi ni moja ya nguzo muhimu za uchumi na maendeleo ya kijamii nchini Tanzania. Sekta hii inahusisha uzalishaji, usafirishaji, uchakataji na uuzaji wa bidhaa zitokanazo na wanyama na viumbe vya majini. Sekta hizi kwa pamoja zina mchango mkubwa katika lishe bora, ajira, mapato ya kaya, na pato la Taifa. Vilevile, zinatoa malighafi kwa ajili ya viwanda kama vile vya kuchakata nyama, maziwa, ngozi na bidhaa za samaki. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imetekeleza maeneo manne ya vipaumbele ambayo ni kuongeza uzalishaji, masoko na thamani ya mazao ya mifugo na uvuvi; kuimarisha ulinzi na usimamizi wa rasilimali za mifugo na uvuvi; kuhamasisha uwekezaji katika sekta za mifugo na uvuvi; na kuimarisha utafiti, mafunzo na huduma. Utekelezaji wa vipaumbele hivi umewezesha Sekta kupata mafanikio katika maeneo mbalimbali ikiwemo:

### 4.2.1 Mifugo

Mafanikio yaliyopatikana katika sekta ndogo ya mifugo ni pamoja na;

i. Kuongeza uzalishaji wa vyakula vya mifugo vilivyosindikwa kutoka tani 1,380,000 mwaka 2020 hadi tani 2,600,000 mwaka 2025;

ii. Kuzalisha na kusambaza jumla ya dozi za chanjo 4,517,731,302 mwaka 2025 ikilinganishwa na dozi za chanjo 1,131,575,874 zilizozalishwa na kusambazwa mwaka 2021;

iii. Kuongeza maeneo ya malisho ya mifugo kutoka hekta 2,788,901.17 mwaka 2020 hadi hekta 3,489,701.13 mwaka 2025. Hatua hiyo, imeongeza maeneo ya malisho na kupunguza migogoro baina ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi;

iv. Kuongezeka kwa mauzo ya biashara ya nyama nje ya nchi kutoka tani 1,774, zenye thamani ya Dola za Marekani 4,290,000 mwaka 2020 na tani 9,863.41, zenye thamani ya Dola za Marekani 44,070,000 mwaka 2025;

v. Kuongeza viwanda vya nyama vyenye ithibati ya kuuza nyama nje ya nchi kutoka viwanda vitatu (3) mwaka 2020 hadi viwanda saba (7) mwaka 2025. Viwanda hivyo ni pamoja na kiwanda cha *Tan Choice Ltd* kilichopo Soga; Kibaha Mkoani Pwani chenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 1,500 na mbuzi/ kondoo 4,500 kwa awamu na kuzalisha ajira za moja kwa moja 397; kiwanda cha *Eliya Food Oversea* kilichopo Namanga Mkoani Arusha chenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 1,000 na mbuzi/ kondoo 1,500 na kuzalisha ajira za moja kwa moja 251; na kiwanda cha Nyama cha *Union* kilichopo Ruvu Mkoani Pwani chenye uwezo wa kuchinja ng'ombe 500 na mbuzi/ kondoo 3,000 kwa awamu na kuzalisha ajira za moja kwa moja 117;

vi. Kuongeza mikopo kwa wafugaji na vikundi vya wafugaji wadogowadogo, kupitia Benki ya TADB kutoka shilingi bilioni 2.19 mwaka 2021 hadi shilingi bilioni 267.09 mwaka 2025 ambapo jumla ya wafugaji 22,163 wamenufaika na mikopo hiyo;

vii. Kuimarisha shughuli za ugani kwa kutoa jumla ya pikipiki 2,253 na hivyo kurahisisha utoaji wa huduma za ugani kwa wananchi; na

viii. Kuwezesha ununuzi wa madume bora ya mbegu aina ya Boran 566 yaliyosambazwa katika Halmashauri 18 nchini. Aidha, Mitamba 1,560 imenunuliwa na kusambazwa katika mashamba matano (5) ya Serikali ya kuzalisha mifugo. Pia, jumla ng'ombe 254,173 wamehimilishwa katika mikoa 26 ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa mkakati wa kuboresha mbari za mifugo nchini.

### 4.2.2 Uvuvi

Mafanikio yaliyopatikana katika sekta ndogo ya uvuvi ni pamoja na;

i. Kuwezesha ongezeko la utoaji wa mikopo kwa wavuvi na vikundi vya wavuvi wadogowadogo kupitia Benki ya TADB kutoka shilingi bilioni 11.29 mwaka 2022 hadi shilingi bilioni 397.8 mwaka 2025. Mikopo hiyo imewasaidia wavuvi wadogo na vikundi vya wavuvi wapatao 502 kunufaika na usimikaji wa vizimba, ununuzi wa boti na ujenzi wa mabwawa ya samaki;

ii. Kuongeza uzalishaji wa samaki na mazao ya uvuvi kutoka tani 477,018.48 zenye thamani ya shilingi 2,775,798,531.30 katika mwaka 2021 hadi kufikia tani 543,598.91 zenye thamani ya shilingi 3,043,687,679,851 mwaka 2025 na hivyo kufanya uzalishaji wa samaki na mazao ya uvuvi kufikia jumla ya tani 2,494,895.24 zenye thamani ya shilingi 3,057,335,184,349.08;

iii. Katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025, vimeongezeka viwanda sita (6) na hivyo kufanya idadi ya viwanda vya kuchakata mazao ya uvuvi kufikia 64. Viwanda hivyo

ni pamoja na kiwanda cha *Taifa Food Limited* Mwanza chenye uwezo wa kuchakata tani 20 za minofu ya samaki kwa siku na kuzalisha ajira 100, *Lake Star* cha Ilemela, Mwanza chenye uwezo wa kuchakata samaki tani 20 kwa siku na ajira 100 na kiwanda cha *Pride of Nile Perch* kilichopo Kagera chenye uwezo wa kuchakata tani 20 kwa siku na kuzalisha ajira 80. Viwanda hivyo 64 vya kuchakata mazao ya uvuvi vimegawanyika katika maeneo matatu ambayo ni viwanda vya kuchakata samaki (24); viwanda vya mabondo (18); na viwanda vya samaki hai-Kaa, kamba koche na samaki wa mapambo (22);

iv. Kuongeza biashara ya mazao ya uvuvi katika soko la ndani na nje ya nchi kutoka tani 42,302.03 zenye thamani ya Shilingi 412,125,228,477.75 mwaka 2021 hadi tani 59,746.41 zenye thamani ya Shilingi 675,326,729,879.96 mwaka 2024. Pia mauzo ya samaki wa mapambo yameongezeka kutoka samaki 181,268 wenye thamani ya shilingi 2,107,401,016.08 mwaka 2021 hadi samaki 173,377 wenye thamani ya shilingi 2,225,304,861.11 mwaka 2024. Mauzo hayo yamesaidia kuongeza kipato kwa wananchi na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa Taifa;

v. Kuendelea na mradi wa ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko wenye thamani ya shilingi bilioni 279.5 ambao hadi Aprili, 2025 umefikia asilimia 81.9;

vi. Kujenga miundombinu ya uvuvi na ukuzaji viumbe maji ikiwa ni pamoja na kukamilisha na kuendelea na ujenzi wa masoko saba (7) na mialo saba (7) ya kupokelea samaki yenye thamani ya shilingi bilioni 15.29;

vii. Kuongeza uzalishaji wa mazao ya ukuzaji viumbe maji kutoka tani 44,735.32 mwaka 2020 hadi tani 124,024.224 mwaka 2025 wenye thamani ya shilingi 314,409,468,850;

viii. Kuongeza uzalishaji wa vifaranga vya samaki kutoka vifaranga 24,204,514 mwaka 2020 hadi vifaranga 110,771,956 mwaka 2025;

ix. Kuongeza uzalishaji wa chakula cha samaki nchini kutoka tani 1,182.47 mwaka 2020 hadi tani 13,859 kwa mwaka 2025;

x. Kuongeza uzalishaji wa zao la mwani kutoka tani 24,380.00 zenye thamani ya shilingi 2,559,900,000 mwaka 2020 hadi tani 88,615.20 zenye thamani ya shilingi 9,304,596,315 mwaka 2025; na

xi. Kusambaza Boti za Uvuvi 160 katika Ukanda wa Pwani 88, Ziwa Victoria 55, Ziwa Tanganyika 11, Ziwa Nyasa 4 na Ziwa Rukwa 2 na kuzalisha ajira za moja kwa moja 3,163 kwa wavuvi na wakuzaji viumbe kati.

### 4.3 Madini

Serikali kwa kutambua umuhimu wa sekta ya madini katika kuimarisha mapato na ajira kwa watanzania, imeendelea kubuni, kuandaa na kusimamia sera, mikakati na mipango ya kuendeleza sekta hiyo ili kuhakikisha mchango wa sekta hiyo katika pato la Taifa unaongezeka. Katika kutekeleza mikakati hiyo mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwemo:

i. Kuongezeka kwa mchango wa sekta kwenye pato la Taifa kutoka asilimia 6.8 mwaka 2020 hadi asilimia 10.1 mwaka 2025;

ii. Kuongezeka kwa kiwango cha makusanyo ya maduhuli ya Serikali kutoka shilingi bilioni 624.61 mwaka 2021 hadi shilingi bilioni 788.82 mwaka 2025;

iii. Kuongezeka kwa mchango wa sekta katika kuliingizia Taifa fedha za kigeni ambapo mauzo ya madini yameendelea

kuongezeka kutoka Dola za Marekeni Bilioni 3.1 mwaka 2021 hadi bilioni 3.55 mwaka 2023;

iv. Kuongezeka kwa masoko na vituo vya ununuzi wa madini kutoka masoko 41 mwaka 2021 hadi 43 mwaka 2025 na vituo vya ununuzi 61 mwaka 2021 hadi 109 mwaka 2025;

v. Kununua mitambo 15 ya uchorongaji kwa ajili ya wachimbaji wadogo katika maeneo mbalimbali ikiwemo Tambi — Mpwapwa, Nyawa — Bariadi, Matondo, Makongolosi na Matundasi — Chunya, Lwamgasa, Nyaruyeye, Nyamalimbe na Nyakagwe — Geita, Mavota — Biharamulo, Endabash — Karatu, Mwakitolyo — Shinyanga na Mbangala – Songwe na hivyo kusaidia katika upatikanaji wa taarifa za kijiolojia na kuongeza tija katika shughuli za uchimbaji;

vi. Kutoa leseni za uchimbaji wa madini mbalimbali ikiwemo:
   a) Leseni ya uchimbaji mkubwa wa madini ya Kinywe kwa mradi wa Epanko Graphite Wilayani Mahenge - Morogoro;
   b) Leseni ya uchimbaji mkubwa wa madini ya Nikeli kwa Kampuni ya Tembo Nickel Wilayani Kabanga - Kagera;
   c) Leseni mbili (2) za uchimbaji wa madini ya *Heavy Mineral Sands* kwa Kampuni ya *Nyati Mineral Sands Ltd* Wilayani Pangani Mkoani Tanga na Fungoni - Kigamboni;
   d) Leseni ya uchimbaji wa madini ya kinywe kwa Kampuni Faru *Graphite Corporation Limited* Wilayani Mahenge - Morogoro;
   e) Leseni ya uchimbaji wa madini ya Rare Earth Elements - REE kwa Kampuni ya *Mamba Minerals Corporation Limited* katika eneo la Ngualla - Songwe; na

f) Leseni moja (1) ya usafishaji madini kwa kampuni ya Tembo Nickel *Refining Company Limited* iliyopo Wilaya ya Ngara — Kagera.

### 4.4 Viwanda na Biashara

Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji katika viwanda na ufanyaji wa biashara nchini kwa kuboresha mifumo ya uratibu na usimamizi wa utekelezaji wa Mipango, Mikakati na Programu mbalimbali za kisekta. Lengo pamoja na masuala mengine ni kujenga uchumi shindani wa viwanda. Mafanikio yaliyopatikana katika sekta hiyo ni pamoja na:

i. Kuanzisha jumla ya viwanda 47,063 nchini. Kati ya viwanda hivyo, viwanda .428 ni vikubwa, 1,393 ni vya kati viwanda, 11,847 ni viwanda vidogo na 33,395 ni viwanda vidogo sana. Viwanda hivyo vinajumuisha kiwanda cha *Wild Flower and Grains Ltd*; Chokaa cha Maweni (Huaxin Cement Co Ltd); Viwanda vya kuunganisha magari (Kiwanda cha GF Trucks and Equipment Ltd na Kiwanda cha Saturn Corporation Limited); Kiwanda cha kutengeneza vioo (Sapphire Float Glass (Tanzania) Company Limited); Kiwanda cha Sukari cha Kilombero; Kiwanda cha Sukari cha Mkulazi; Kiwanda cha Sukari Kagera; kiwanda cha sukari cha Bagamoyo; kongani za viwanda ikiwemo kongani ya Kwala Pwani ambapo viwanda viwili vya nguo na vipodozi vimejengwa na kuendelea na ujenzi wa kongani ya kisasa katika eneo la Kikongo Wilaya ya Chalinze Mkoa wa Pwani; na kiwanda cha kuunganisha na kutengeneza ndege cha kampuni ya *Airplanes Africa Limited* kilichopo Morogoro ambapo ndege za kubeba abiria wawili mpaka wanne zinatengenezwa;

ii. Kusajili makampuni 58,637, majina ya biashara 109,292,

na alama za biashara na huduma 13,153. Vilevile, kutoa leseni za biashara kundi ‘A’ 65,442 na leseni za viwanda 1,002;

iii. Kuongezeka kwa mazao yanayouzwa kwa kutumia mfumo wa stabadhi za ghala ambapo, mazao yanayotumia mfumo wa stakabadhi za ghala yaliongezeka kutoka mazao 11 hadi 16. Mazao hayo ni Ufuta, Kakao, Asali, Maharage, Mihogo, Dengu, Choroko, Vitunguu swaumu, Mahindi, Mpunga, Mbaazi, Korosho, Chai, Mchele, Soya na Kahawa. Aidha, jumla ya tani 654,928.06 za mazao ziliuzwa kupitia mfumo huo na kuwezesha upatikanaji wa shilingi trilioni 4.9 kwa wakulima na kutengeneza ajira 6,983;

iv. Kuimarisha upatikanaji wa huduma za kifedha kwa wajasiriamali kupitia Mfuko wa Taifa wa Kuendeleza Wajasiriamali (NEDF). Hadi Aprili 2025, mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati 10,113 yenye thamani ya shilingi Billioni 26.225 imetolewa na kuwezesha upatikanaji wa ajira 23,535;

v. Kuongeza mauzo ya bidhaa nje ya nchi ambapo, mauzo katika soko la Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) yaliongezeka kutoka Dola za Marekani milioni 1,161.2 mwaka 2021 hadi 1,163.8 mwaka 2024;

vi. Kuongezeka kwa mauzo katika soko la Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kutoka Dola za Marekani milioni 1,303.4 mwaka 2021 hadi kufikia Dola za Marekani milioni 2968 mwaka 2024;

vii. Kuendelea kunufaika na Mpango wa AGOA ambapo mauzo yameongezeka kutoka Dola za Marekani Milioni 33.06 mwaka 2021 hadi Dola za Marekani milioni 85.4 mwaka 2023. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni nguo na

mavazi, Kahawa, Mbogamboga na madini. Baadhi ya viwanda vilivyouza bidhaa katika soko hilo ni pamoja na *Mazava Fabrics and Production E.A L, Tanzania Tooku Garments Co. Ltd, Red Earth Co. Ltd* na *21st Century Textiles Ltd*;

viii. Kuongeza mauzo ya bidhaa katika soko za Nchi Wanachama wa Umoja wa Ulaya kutoka Dola za Marekani Milioni 891.5 mwaka 2021 hadi Dola za Marekani Milioni 1,234.3 mwaka 2024. Bidhaa zilizouzwa kwa wingi ni pamoja na Maharage, Tumbaku, Samaki, Parachichi, Kahawa, Kokoa, Asali, Mafuta ya Alizeti, Madini, Chai (black tea), Maua, Matunda, Pamba Gafi, Mbogamboga, Ngozi na Madini ya Tanzanite; na

ix. Kutengeneza mitaa ya viwanda katika mikoa 23 ya Tanzania Bara ambayo ina miundombinu muhimu kwa ajili ya kuwasaidia wajasiriamali kuanzisha na kuendeleza viwanda vidogo na vya kati ambapo majengo mapya ya viwanda yamejengwa katika Mikoa ya Manyara, Morogoro, Katavi, Mtwara, Mwanza, Tanga, Singida na Geita – Chato.

### 4.5 Maliasili na Utalii

Sekta ya maliasili na utalii ina mchango mkubwa katika ukuaji wa uchumi na kuwaongezea wananchi kipato na fursa za ajira. Ili kuimarisha mchango wa sekta hiyo katika uchumi, Serikali imeendelea kutekeleza na kusimamia ipasavyo mikakati ya kukuza vivutio mbalimbali vya utalii ikiwemo hifadhi za wanyama, misitu ya mazingira asilia, utamaduni, fukwe na malikale. Vilevile, kutunza maliasili za nchi na mazao yatokanayo na maliasili, hususan wanyamapori, misitu na nyuki ili kuchangia kikamilifu katika ukuaji wa uchumi nchini. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuongezeka kwa idadi ya watalii kutoka 1,711,625 mwaka 2021 hadi 5,360,247 mwaka 2024. Kati yao, watalii wa kimataifa waliongezeka kutoka 922,692 mwaka 2021 hadi 2,141,895 mwaka 2024 na idadi ya watalii wa ndani iliongezeka kutoka watalii 788,933 mwaka 2021 hadi 3,218,352 mwaka 2024. Ongezeko hilo limechangia kuongeza ajira na kipato kwa wananchi wanaojishughulisha na shughuli za utalii;

ii. Kuongeza mapato yatokanayo na shughuli za utalii kutoka Dola za Marekani milioni 700 mwaka 2020 hadi Dola za Marekani bilioni 3.9 mwaka 2024 kwa watalii wa kimataifa. Aidha, mapato yatokanayo na utalii wa ndani yameongezeka kutoka Shilingi bilioni 46.3 mwaka 2021 hadi Shilingi bilioni 209.8 mwaka 2024. Hatua hiyo imeifanya Tanzania kuwa nafasi ya tisa (9) duniani na kushika nafasi ya tatu (3) Barani Afrika kwa ongezeko la mapato;

iii. Kuendelea kutambulika na kung'ara Kimataifa ambapo nchi imepata Tuzo za Kimataifa zikiwemo: Eneo linalovutia zaidi kiutalii (Africa's Leading Destination, 2024); eneo linaloongoza kwa utalii wa safari (World's Leading Safari Destination, 2024); Hifadhi ya Taifa Serengeti kuendelea kuwa bora Duniani kwa miaka mitano (5) mfululizo na kutambuliwa kama eneo la pili bora zaidi duniani kwa safari na utalii (World Travel Awards); na Mlima Kilimanjaro kushinda Tuzo ya kivutio bora cha utalii barani Afrika (African Leading Tourism Attraction, 2024). Mafanikio haya yametokana na jitihada mbalimbali za Serikali ikiwemo kuandaa filamu ya Tanzania - The Royal Tour na Amazing Tanzania ambapo Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wameshiriki kama wahusika wakuu;

iv. Kuongezeka kwa idadi ya wakala wa biashara za utalii kutoka 2,885 mwaka 2020 hadi 3,735 mwaka 2025 na kuongezeka kwa idadi ya waongoza watalii kutoka 5,076 mwaka 2020 hadi 7,862 mwaka 2025. Mafanikio hayo yamechangiwa na maboresho yaliyofanywa ya Kanuni ya Ada na Tozo ya Utalii ya Mwaka 2015. Hatua hii imewezesha vijana wengi wa kitanzania kupata ajira za moja kwa moja kwa kufungua kampuni binafsi na kujiajiri kama waongoza watalii;

v. Kuimarika kwa Utalii wa Mikutano na Matukio ambapo Tanzania imefanikiwa kuwa mwenyeji wa matukio mbalimbali ya Kimataifa ikiwemo Jukwaa la Pili la Utalii wa Chakula Duniani (Second UN Tourism Gastronomy) kwa Kanda ya Afrika linaloandaliwa na Shirika la Utalii Duniani (UN Tourism) lililofanyika kuanzia tarehe 23 – 25 Aprili, 2025 Jijini Arusha; Mkutano wa Nishati wa Wakuu wa Nchi za Afrika uliofanyika Januari, 2025 Jijini Dar es Salaam na hivyo kuwezesha nchi kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini kupitia matukio hayo;

vi. Kuimarika kwa biashara ya mazao ya misitu na nyuki ambapo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

a) Kuongeza kiwango cha uzalishaji wa malighafi mbao katika mashamba ya Serikali kutoka mita za ujazo 1,108,791 mwaka 2020 hadi 1,264,535 mwaka 2025. Vilevile, viwanda vya kuongeza thamani mazao ya misitu vimeongezeka kutoka 636 mwaka 2020 hadi 1,125 mwaka 2025. Sambamba na hilo, thamani ya mauzo ya mazao ya misitu nje ya nchi imeongezeka kutoka shilingi 105,689,957,500 mwaka 2020 hadi shilingi 458,474,543,027.45 mwaka 2025; na

b) Kuwezesha ujenzi wa viwanda vya kati na vikubwa vya kuchakata na kuongeza thamani mazao ya

nyuki kutoka kiwanda kimoja (1) mwaka 2020 hadi nane (8) mwaka 2025. Viwanda hivyo vipo katika Mikoa ya Tabora, Kigoma, Singida, Iringa, Katavi na Geita. Hatua hii imewezesha ongezeko la uzalishaji wa asali kutoka tani 31,179 mwaka 2020 hadi 33,861 mwaka 2024 na kuongeza ubora na thamani ya mazao ya nyuki kabla ya kuuzwa katika soko la ndani na nje ya nchi.

vii. Kuongeza upandaji miti kutoka miche 20,689,369 mwaka 2020 hadi 34,126,916 mwaka 2025 na hivyo kuchangia kuongeza uhifadhi wa ardhi, bioanuai za mimea na wanyama; kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi; na kuhakikisha upatikanaji wa mazao ya misitu.

## 4.6 Ardhi

Sekta ya ardhi imeendelea kuwa na mchango mkubwa katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, mageuzi makubwa yamefanyika katika usimamizi wa ardhi ikiwa ni pamoja na maboresho ya kisera, matumizi ya TEHAMA na mikakati ya kuongeza uwazi na ufanisi katika utoaji huduma za ardhi. Mafaniko yaliyopatikana ni pamoja na:

### 4.6.1 Upimaji na Umilikishaji wa Ardhi

i. Kupima viwanja 1,427,005 na mashamba 11,699; na kuhakiki mipaka ya vijiji 974 katika wilaya mbalimbali nchini. Vilevile, kusajili na kumilikisha Hatimilki 356,642 na nyaraka nyingine za kisheria 444,447 pamoja na kuandaa na kusajili Hatimilki za kimila 318,868 katika vijiji 236 vya Wilaya 6 za Songwe, Chamwino, Mufindi, Mbinga, Maswa na Tanganyika;

ii. Kuidhinishwa kwa maombi 719 ya ardhi ya uwekezaji yenye ukubwa wa hekta 146,363,240 kwa ajili ya uwekezaji. Kati

ya hayo, maombi 258 ni ya raia wa Tanzania na 461 ni ya wawekezaji kutoka nje ya nchi ambao walikuwa na mtaji wenye thamani ya shilingi trilioni 15.41;

iii. Kusimikwa kwa alama za Msingi za Upimaji 710 katika Halmashauri mbalimbali nchini na hivyo kuwa na jumla ya alama za upimaji 1,545 katika maeneo mbalimbali. Pia, mpaka wa Kimataifa kati ya Tanzania na Kenya wenye jumla ya kilomita 268 umeimarishwa pamoja na kufanya ukaguzi wa mpaka wa Tanzania na Kenya, Tanzania na Zambia, Tanzania na Burundi na Tanzania na Msumbiji;

iv. Kuidhinishwa kwa vijiji 448 kati ya 975 vilivyobainishwa kuanzishwa ndani ya Hifadhi ambapo ardhi yenye jumla ya ekari 2,402,581.32 imerejeshwa kwa wananchi ikijumuisha ekari milioni 1.65 kutoka kwenye maeneo ya hifadhi, ranchi na mashamba ya Serikali; ekari 707,962 kutoka kwenye Mapori Tengefu 12 na ekari 46,715 kutoka kwenye Hifadhi za Misitu saba (7);

v. Kuimarisha usimamizi wa mipaka ya Hifadhi kwa kusimika vigingi 32,838 na kuchonga mkuza kuzunguka maeneo ya Hifadhi za Taifa 21 na Mapori ya Akiba 29 na Hifadhi za Misitu 416 pamoja na kufanya uthamini wa kawaida 97,340 wenye majedwali yenye wananchi wa kufidiwa 153,358;

vi. Kuanzisha mabaraza ya Ardhi na Nyumba ya Wilaya 67 na kufanya kuwa na Mabaraza 115 yanayotoa huduma kati ya Mabaraza 139 yanayotakiwa kuwepo. Vilevile, mashauri 98,880 yalitolewa maamuzi kati ya mashauri 110,784 yaliyokuwa yanashughulikiwa;

vii. Kuunganisha Mfumo wa e-Ardhi na utunzaji wa kumbukumbu za ardhi kidijiti katika maeneo mbalimbali nchini. Mfumo unatumika katika Halmashauri 46 za Mikoa

11 ya Arusha (7), Dodoma (8), Mbeya (7), Shinyanga (2), Mtwara (1), Pwani (1), Tanga (11), Mwanza (6), Ruvuma (1), Kigoma (1) na Tabora (1) ambako kazi ya kubadili nyaraka za taarifa za kijiografia na umiliki wa ardhi kutoka analojia kwenda kidijiti imekamilika. Jumla ya kumbukumbu za wamiliki wa ardhi 957,407 zimehuishwa; na

viii. Kukamilisha maandalizi ya Sera ya Taifa ya Ardhi ya Mwaka 1995, Toleo la Mwaka 2023 ambayo itasaidia kuwepo kwa mfumo madhubuti wa umiliki wa ardhi, usawa katika upatikanaji ardhi, usimamizi na matumizi ya ardhi kwa maendeleo endelevu.

### 4.6.2 Upangaji wa Matumizi ya Ardhi

i. Kuhakiki mipaka ya kiutawala na kutatua migogoro katika vijiji 514. Aidha, vijiji 2,160 vimeandaliwa mipango ya matumizi bora ya ardhi, pamoja na kuandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya wilaya 11, mikoa mitatu (3) na mpango wa kanda mmoja (1) *(Mara Lowland Zone)*;

ii. Kuandaa Mipangokina ya vijiji 123 katika Halmashauri za Wilaya 31 na kuwezesha utoaji wa Hati za Hakimiliki za Kimila 38,243 katika maeneo ya vitovu vya vijiji na maeneo ya mashamba. Hati hizi zimewezesha kuongeza usalama wa milki za ardhi, thamani ya ardhi, kupunguza migogoro ya ardhi, kulinda maeneo ya huduma za jamii na kuimarisha uwekezaji mbalimbali;

iii. Kutenga maeneo yenye ukubwa wa hekta 528,438.1 kwa ajili ya matumizi mbalimbali ikiwemo kilimo (hekta 379,437), uwekezaji (hekta 5578.2), Hifadhi ya Misitu ya Kijiji (hekta 39,982.3), makazi (hekta 66,582.2), vyanzo vya maji (hekta 15,470.7) na malisho (hekta 21,387.7).

Mipango hiyo imesaidia kuibua fursa zinazotokana na shughuli za utalii, kilimo, mifugo, viwanda na uwekezaji; na

iv. Kujenga uwezo kwa Mamlaka za Upangaji za Wilaya 99, Mamlaka za vijiji 2,591 wa kuandaa, kusimamia na kutekeleza mipango ya matumizi ya ardhi.

### 4.6.3 Mipango Miji na Vijiji

i. Kutekeleza Programu Maalum ya Uendelezaji Upya wa Maeneo Chakavu katika miji mbalimbali nchini ambapo jumla ya maeneo 111 yenye ukubwa wa hekta 24,309.3 yameainishwa katika mikoa 24 kwa ajili ya kupangwa na kuendelezwa upya ili kuyafanya kuwa na tija kiuchumi na kijamii. Vilevile, Mipango saba (7) imeidhinishwa katika Majiji ya Mbeya na Tanga; Manispaa za Lindi, Morogoro, Mpanda na Moshi; na Mji wa Bagamoyo;

ii. Kuidhinisha Mipango Kabambe 15 ya Jiji la Mbeya, Dar es salaam, Tanga, Halmashauri ya Manispaa ya Mpanda, Lindi, Moshi, Morogoro, Sumbawanga, Kigoma, Shinyanga na Bukoba na Mji wa Tunduma, Geita, Njombe na Bagamoyo. Aidha, mipango minne (4) ya Manispaa ya Kahama, Mji wa Mafinga, Mji wa Vwawa (Mbozi) na Kwala (Kibaha) ipo katika hatua mbalimbali; na

iii. Kuidhinisha michoro ya mipangomiji 10,192 yenye jumla ya viwanja 1,516,309, mabadiliko ya matumizi ya ardhi 2,070 na kurasimisha makazi 1,710,920 katika Halmashauri mbalimbali nchini. Lengo la urasimishaji makazi yasiyopangwa ni kuhakikisha usalama wa milki, kutatua changamoto za migogoro ya ardhi na kuwezesha upatikanaji wa maeneo kwa ajili ya huduma za kijamii na miundombinu ya msingi.

### 4.6.4 Nyumba na Makazi

Kwa upande wa nyumba na makazi mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 1.98 kwa watumishi wa Serikali 166 kupitia Mfuko wa Mikopo ya Nyumba kwa Watumishi wa Serikali. Aidha, kwa kutambua umuhimu wa nyumba kwa watumishi wa umma, kiwango cha mkopo kimeongezeka kutoka shilingi milioni 20 hadi shilingi milioni 40 ili kukidhi ongezeko la gharama za ujenzi wa nyumba na uhalisia wa sasa wa bei za vifaa vya ujenzi;

ii. Kutoa mikopo ya shilingi bilioni 659.3 kupitia taasisi za fedha kwa ajili ya ujenzi wa nyumba. Aidha, ujenzi wa nyumba kutoka taasisi za fedha na benki za biashara zinazotoa mikopo kwa ajili ya ujenzi wa nyumba zimefikia 31;

iii. Kufanikiwa kuingiza kwenye kanzidata nyumba 14,358,372 zilizobainika kupitia Sensa ya Makazi ya Mwaka 2022 kwa ajili ya kuwezesha maendeleo na mipango ya kitaifa; na

iv. Kukamilisha miradi mitatu mikubwa iliyopo Jijini Dar es Salaam ukiwemo mradi wa *Morocco Square* wenye thamani ya shilingi bilioni 137. Aidha, ujenzi wa mradi wa Kawe 711 wenye thamani ya shilingi bilioni 169 umefikia asilimia 70 na mradi wa *"Samia Housing Scheme"* unaendelea katika mikoa ya Dar es Salaam na Dodoma.

# SURA YA TANO

## 5. UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

### 5.1 Ujenzi

Sekta ya ujenzi imeendelea kuwa muhimu katika ukuaji wa uchumi kwa kuwezesha usafiri na usafirishaji kupitia ujenzi na kukarabati miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikiwemo barabara na madaraja, viwanja vya ndege na majengo mbalimbali. Kutokana na uwekezaji uliofanyika, miundombinu hiyo imewezesha usafiri na usafirishaji wa bidhaa kwa wakati kutoka maeneo ya uzalishaji hadi kwenye masoko. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuongezeka kwa mtandao wa barabara kwa kiwango cha lami kutoka kilomita 38,086.95 mwaka 2020 hadi 40,902.434 mwaka 2025 na mtandao wa barabara za changarawe kutoka kilomita 24,493 mwaka 2020 hadi 44,372.21 mwaka 2025. Aidha, upembuzi yakinifu na usanifu wa kina kwa ajili ya ujenzi kwa barabara zenye urefu wa jumla ya kilomita 3,848.13 umekamilika;

ii. Kukamilisha ujenzi wa madaraja kumi (10) ya Gerezani (Dar es Salaam), Tanzanite (Dar es Salaam), Wami (Pwani), Kitengule (Kagera), Kiyegeya (Morogoro), Ruaha (Morogoro), Ruhuhu (Ruvuma), Mpwapwa (Dodoma), Msingi (Singida) na JP Magufuli (Kigongo – Busisi). Madaraja yaliyokamilika yamerahisisha utekelezaji wa shughuli za kiuchumi na ufikiwaji wa huduma za kijamii kwa haraka kwa kupunguza foleni na muda wa usafiri;

iii. Kukamilika kwa awamu ya pili kilomita 20.3 ya mradi wa ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka

(BRT) (Mbagala - Mzunguko wa Bandari (Bendera Tatu), Bendera Tatu – Kariakoo, Sokoine – Zanaki, Barabara ya Kawawa – Barabara ya Morogoro (Magomeni) pamoja na kuendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tatu, kilomita 23.3 kutoka katikati ya Jiji hadi Gongo la Mboto ambao umefikia asilimia 80 na awamu ya nne, kilomita 30.1 kutoka katikati ya Jiji hadi Tegeta ambao umefikia asilimia 22. Ujenzi wa barabara hizo utasaidia kupunguza msongamano wa magari katika Jiji la Dar es Salaam;

iv. Kuendelea na ujenzi wa barabara ya kiwango cha lami ya Mzunguko wa Nje (*Outer Ring Road*) katika Jiji la Dodoma ambapo ujenzi wa sehemu ya kwanza ya Nala – Veyula – Mtumba – Ihumwa Bandari Kavu (km 52.3) umefikia asilimia 86 na sehemu ya pili ya Ihumwa Bandari Kavu – Matumbulu – Nala (km 62) imefikia asilimia 82. Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kupunguza msongamano wa magari katikati ya Jiji la Dodoma;

v. Kuendelea na upanuzi wa Barabara Kuu ya TANZAM sehemu ya Uyole – Ifisi – Songwe Airport Jijini Mbeya yenye urefu wa kilomita 36 kutoka njia mbili kuwa njia nne ambapo ujenzi umefikia asilimia 23.5;

vi. Kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Iringa uliohusisha ukarabati na uboreshaji wa barabara ya kuruka na kutua ndege (Runway), ujenzi wa maegesho ya ndege (Apron), barabara za viungio (taxiway), jengo la zimamoto, jengo la kuongozea ndege na usimikaji wa taa za kuongozea ndege na taa za usalama. Aidha, awamu ya pili ya ujenzi wa uwanja huo inayohusisha ujenzi wa jengo la kudumia abiria pamoja na miundombinu upo katika hatua ya awali ya ujenzi;

vii. Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vya ndege ambapo ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Tabora umefikia asilimia 93, Kiwanja cha Ndege cha Kigoma asilimia 20 na Kiwanja cha Ndege cha Geita asilimia 80. Vilevile, ukarabati wa Kiwanja cha Ndege cha Musoma umefikia asilimia 58, Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga asilimia 60, Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga asilimia 80 na kukamilisha ukarabati wa viwanja vya ndege vya Arusha, Songea, Mpanda, Kahama na Mtwara;

viii. Kuendelea na ujenzi wa Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato – Dodoma ambapo utekelezaji wake umegawanyika katika sehemu mbili. Sehemu ya kwanza inayohusisha ujenzi wa barabara ya kuruka na kutua Ndege (*runway*), Barabara za maungio (*Taxiways*), Maegesho ya Ndege (*Aprons*), Uzio wa usalama, Barabara ya kuingia na kutoka Kiwanjani, Maegesho ya Magari na Usimikaji wa Taa za kuongozea Ndege ambapo utekelezaji umefikia asilimia 87. Aidha, sehemu ya pili inayohusisha ujenzi wa jengo la abiria, jengo la kuongozea ndege, Kituo cha Zimamoto, Kituo cha Hali ya Hewa na vituo vidogo nane (8) vya kufua umeme ambapo utekelezaji umefikia asilimia 53.22;

ix. Kuendelea na ujenzi wa vivuko vipya sita (6) ambao umefikia hatua zifuatazo: Mafia – Nyamisati (asilimia 35), Bwiro – Bukondo (asilimia 87), Kisorya – Rugezi (asilimia 82), Ijinga – Kahangala (asilimia 90), Nyakaliro – Kome (asilimia 83) na Buyagu – Mbalika (asilimia 80);

x. Kukamilika kwa ukarabati wa boti MV Tangazo iliyopo Tanga pamoja na matengenezo ya Boti Mv Mkongo iliyopo Pwani ambazo zimeanza kutoa huduma katika maeneo hayo. Vilevile, kuendelea na ukarabati wa vivuko ambao umefikia hatua zifuatazo: MV Kilombero II (asilimia

90), MV Nyerere (asilimia 81), MV Ukara I (asilimia 20), MV Kigamboni, MV Magogoni (asilimia 55) na MV Old Ruvuvu (asilimia 80);

xi. Kukamilika kwa awamu ya pili ya ujenzi wa ghorofa za makazi (Jengo B) katika eneo la Magomeni Kota. Aidha, ujenzi unaendelea kwa jengo C ambapo utekelezaji umefikia asilimia 40 na jengo D ujenzi asilimia 25; na

xii. Kuendelea na ujenzi wa nyumba za makazi za watumishi na viongozi ambao upo katika hatua mbalimbali kama ifuatavyo; Ghorofa la Makazi kwa Watumishi wa Umma eneo la Ghana Kota Jijini Mwanza (asilima 25) na ujenzi wa nyumba 150 za watumishi wa Umma katika eneo la Nzuguni Jijini Dodoma (asilimia 40).

### 5.2 Uchukuzi

Sekta ya uchukuzi imeendelea kuwa kiungo muhimu katika kuchangia ukuaji wa uchumi hususan kwa kuimarisha huduma za uchukuzi. Miradi katika sekta hii inajumuisha ujenzi wa reli ya kisasa *(Standard Gauge Railway - SGR)*, uboreshaji wa bandari kuu na kwenye maziwa makuu, ununuzi wa meli na ndege, ujenzi wa viwanja vya ndege, ununuzi wa rada za hali ya hewa pamoja na ujenzi wa vituo vya utafutaji na uokozi kwenye Maziwa Makuu ikiwa ni sehemu ya juhudi za kuimarisha sekta ya uchukuzi. Utekelezaji wa miradi hiyo, umerahisisha usafirishaji wa watu na mizigo na hivyo kusaidia kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza fursa za ajira. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

#### 5.2.1 Usafiri wa Anga

i. Ununuzi wa ndege saba ambapo ndege sita ni za abiria na ndege moja ni ya mizigo kwa gharama ya shilingi trilioni 1.49 katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025. Ununuzi wa ndege hizo umelifanya Shirika kuwa na jumla ya ndege

16 ambazo zimeimarisha na kuongeza safari za ndege za ndani na nje ya nchi. Uboreshaji wa miundombinu ya ATCL umeongeza idadi ya abiria wanaohudumiwa kutoka 822,232 mwaka 2021 hadi 4,291,990 Aprili, 2025; mizigo kutoka tani 2,567 mwaka 2021 hadi tani 20,098.32 Aprili, 2025. Kadhalika, mapato yameongezeka kutoka shilingi bilioni 254 mwaka 2021 hadi shilingi trilioni 1.7 Aprili, 2025;

ii. Kuongezeka kwa ajira za moja kwa moja kutoka 595 hadi 858;

iii. Kujenga uwezo wa ufundi na matengenezo ya ndege kwa kuiwezesha ATCL kufanya matengenezo madogo na makubwa ya ndege kupitia karakana zake za JNIA na KIMAFA ili kuhakikisha karakana hizo zinatoa huduma ya matengenezo ya ndege za ATCL na mashirika mengine ya ndege yanayohitaji huduma hizo;

iv. Kununua ndege mbili za mafunzo aina ya *Cessna 172s* zenye injini moja kwa ajili ya kutoa mafunzo ya Urubani hapa nchini na hivyo kuongeza idadi ya marubani wazawa; na

v. Kujenga Kituo cha Umahiri cha Mafunzo ya Taaluma za Anga na Operesheni za Usafirishaji.

Manufaa mengine ya jumla yaliyopatikana katika eneo la usafiri wa anga ni pamoja na kuimarika kwa mnyororo wa thamani wa bidhaa zinazoharibika haraka kupitia usafiri wa anga na hivyo kurahisisha bidhaa hizo kuwafikia walaji katika masoko ya nje kwa wakati, kuwapunguzia hasara wazalishaji; Kuongeza mapato ya fedha za kigeni na mapato ya Serikali kupitia kodi, ada na tozo za kisheria ambapo mapato ya fedha za kigeni yamefikia Dola za Marekani milioni 375.23, huku jumla ya mapato

ya Serikali kupitia kodi, ada na tozo za kisheria yakifikia shilingi bilioni 221.16; kuchochea shughuli mbalimbali za ukuaji wa kiuchumi na kijamii; kuongezeka kwa fursa za kibiashara; kufungua nchi na kuvutia fursa za uwekezaji kutoka nje ya nchi.

### 5.2.2 Reli ya Kisasa ya SGR

i. Kukamilika kwa ujenzi wa Reli ya Kisasa (SGR) kipande cha Dar es Salaam – Makutupora (km. 722) ambapo huduma ya kusafirisha abiria kati ya Dar es Saalam – Morogoro – Dodoma zilianza kutolewa rasmi mwishoni mwa Juni, 2024. Tangu kuzinduliwa kwa huduma ya usafiri kwa kutumia treni ya SGR Agosti, 2024 hadi Machi 2025, zaidi ya abiria 2,054,828 wamesafiri kwa kutumia treni hiyo na kuingiza jumla ya shilingi bilioni 60.88. Uwepo wa huduma hiyo umepunguza adha ya usafiri kwa wananchi ambapo muda wa safari kati ya Dar es Salaam na Morogoro umekuwa saa 1 na dakika 45 ikilinganishwa na usafiri wa mabasi unaotumia saa 4 hadi 5. Hali kadhalika, muda wa safari kati ya Dar es Salaam na Dodoma kwa treni hiyo ni wastani wa saa 3 ikilinganishwa na usafiri wa mabasi unaotumia saa 8 hadi 9 na hivyo kuchagiza kasi ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini;

ii. Ujenzi wa vipande vingine vya kuunganisha reli ya kisasa ya SGR unaendelea ambapo kipande cha kutoka Mwanza - Isaka (km 341) umefikia asilimia 63.16; Makutupora – Tabora (km 368) asilimia 14.53; Tabora – Isaka (km 165) asilimia 6.65; na Tabora – Kigoma (km 506) asilimia 7.81. Aidha, maandalizi ya kuanza ujenzi wa kipande cha Uvinza - Malagarasi - Musongati (Km 282) yameanza ambapo Serikali za Tanzania na Burundi zilisaini mkataba wa ujenzi wa kipande hicho tarehe 29 Januari, 2025. Kutekelezwa kwa mradi huo, kumezalisha ajira 9,376

pamoja na kuwezesha kampuni zaidi ya 792 kuingia mikataba mbalimbali kwa ajili ya kandarasi na huduma za chakula, ulinzi, usafiri, bima na bidhaa za ujenzi;

iii. Kununua vitendea kazi vya Reli ya Kisasa ya SGR ambapo mabehewa 71 yamewasili nchini na yameanza kutoa huduma na mabehewa 18 yanatarajiwa kuwasili kwa nyakati tofauti mwaka 2025;

iv. Kununua vichwa vya treni vya umeme 17 na seti 10 za EMU (Mchongoko) ambavyo tayari vimewasili nchini na kuanza kutoa huduma pamoja na mabehewa ya mizigo 264 ambapo kazi ya majaribio ya mifumo inaendelea; na

v. Kutafuta fedha za ujenzi wa reli ya SGR kutoka Tabora – Kigoma (km. 506) ambayo itafungua mipaka ya biashara na nchi ya Demokrasia ya Kongo kupitia Ziwa Tanganyika (Kigoma).

### 5.2.3 Reli ya kati (MGR)

i. Kununua vichwa vya treni vitatu, mabehewa ya abiria 22 na mabehewa ya mizigo 44; na
ii. Kufanya ukarabati wa mabehewa 350 ya mizigo na 33 ya abiria ambayo yameanza kutoa huduma.

### 5.2.4 Bandari

Kwa kuzingatia ushindani wa kibiashara katika ukanda wa Bahari ya Hindi, Serikali imechukua hatua mahsusi ili kunufaika na fursa ya kijiografia ya nchi yetu kuwa lango kuu la kibiashara kwa nchi jirani. Hatua hizo ni pamoja na uboreshaji wa bandari zilizo katika bahari kuu na uwekezaji wa sekta binafsi katika kutoa baadhi ya huduma bandarini. Mafanikio yaliyopatikana katika Bandari kuu za Dar es Salaam, Tanga na Mtwara na maziwa makuu ni pamoja na:

i. Kukamilika kwa maboresho ya miundombinu ya Bandari ya Dar es Salaam ambayo yalihusu uboreshaji wa gati Na. 1 – 7, kuchimba kina cha maji kutoka mita 11 hadi mita 14.5 na upanuzi wa lango la kuingilia na kugeuzia meli, ujenzi wa gati maalumu (RoRo berth) la kuhudumia meli za magari na eneo la kuegesha magari katika Bandari ya Dar es Saalam. Maboresho hayo yamepunguza muda wa kusubiri meli, urahisi wa kupokea na kusafirisha bidhaa, uwezo wa bandari kuhudumia meli kubwa zaidi na hivyo kupunguza gharama za usafirishaji na bidhaa;

ii. Kukamilika kwa uboreshaji wa Bandari ya Tanga katika awamu ya pili kwa kufanya ukarabati wa gati namba 1 na 2 zenye urefu wa mita 300, ununuzi wa mitambo na kuongeza kina kutoka mita 3 hadi 13; Kukamilika kwa upanuzi wa eneo la kuingia meli na kutoka bandarini lenye upana wa mita 73 na eneo la kugeuzia meli na kuwa na kipenyo cha mita 800 hali ambayo imewezesha meli kuhudumiwa kwenye gati badala ya nangani na hivyo kuongeza ufanisi wa bandari kutoka tani 500,000 hadi tani 1,290,000;

iii. Kukamilika kwa ujenzi wa gati, uzio wa bandari na barabara inayounganisha gati jipya na maeneo mengine katika Bandari ya Mtwara; na

iv. Kuendelea na ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala ambapo kazi zifuatazo zimekamilika: barabara ya zege yenye urefu wa kilomita 15.5 kutoka barabara kuu ya Morogoro hadi Bandari Kavu ya Kwala; uzio wenye mzunguko wa kilomita 9; mtandao wa reli ya MGR wenye urefu wa kilomita 1.3; na yadi ya sakafu ngumu *(pavement)* yenye ukubwa wa hekta tano (5) kwa ajili ya kuhifadhi shehena za mizigo. Aidha, bandari kavu hii imeanza kutoa huduma za kupokea makasha kutoka Bandari ya Dar es Salaam kwa kutumia njia ya reli na barabara.

### 5.2.5 Usafiri wa Maziwa Makuu

i. Kukamilisha ukarabati wa meli ya MV Umoja (Wagon Ferry) katika Ziwa Victoria ambapo meli hiyo imeanza kutoa huduma ya kusafirisha mizigo kati ya Bandari ya Mwanza (Tanzania) na bandari ya Jinja (Uganda). Kukamilika kwa meli hii ya MV Umoja, kumepunguza kero kwa wafanyabiashara kwa kusafirisha shehena kubwa ya mzigo kwa wakati mmoja na hivyo kuongeza ufanisi katika shughuli za usafirishaji kwa njia ya maji;

ii. Kuendelea na ujenzi wa meli ya MV Mwanza kwa gharama ya shilingi bilioni 109 ambayo ujenzi wake umefikia asilimia 98. Ujenzi utakapokamilika, meli hiyo itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 1,200, tani 400 za mizigo, magari madogo 20 na malori matatu;

iii. Kuendelea na ukarabati wa meli katika Ziwa Tanganyika ambazo ni MT Sangara kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 3.6 ambapo ujenzi umefikia asilimia 98. Meli hiyo itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kubeba shehena ya mafuta kiasi cha lita 410,000 kwenda nchi jirani za DRC na Burundi; na MV Liemba kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 13.19 ambao umefikia asilimia 15. Meli hii itakapokamilika itakuwa na uwezo wa kubeba abiria 600 na tani 200 za mizigo; na

iv. Kuboresha bandari zilizopo katika Ziwa Victoria ambapo ujenzi wa Bandari ya Kemondo umekamilika na ujenzi wa Bandari ya Bukoba unaohusu ujenzi wa gati ya kuhudumia shehena ya magari (RO-RO), kizuia upepo, ujenzi wa eneo la maegesho ya magari na ujenzi wa jengo la abiria umefikia asilimia 94. Uboreshaji wa Bandari ya *Mwanza North* umefikia asilimia 58.

### 5.2.6 Utendaji wa Mamlaka ya Bandari

i. Kuongezeka kwa shehena za mizigo zilizohudumiwa na Mamlaka ya Bandari kutoka tani milioni 17.78 mwaka 2020/21 hadi tani milioni 27.55 mwaka 2023/24. Aidha, katika kipindi cha Novemba 2024 hadi Aprili 2025 TPA ilihudumia tani milioni 15.88 ya shehena; na

ii. Kuongezeka kwa shehena ya makasha (TEUs) kutoka makasha 728,281 mwaka 2020 hadi 1,053,174 mwaka 2024. Aidha, uwekezaji mkubwa wa mitambo ya kisasa na mifumo ya TEHAMA umewezesha ongezeko la asilimia 12.9 kwa mwaka. Kati ya Novemba 2024 hadi Aprili 2025, TPA ilihudumia makasha 582,701 ikiwa ni ongezeko la asilimia 61.7 ikilinganishwa na makasha 360,412 yaliyohudumiwa katika kipindi kama hicho kuanzia Novemba 2020 hadi Aprili 2021.

### 5.2.7 Uwekezaji wa sekta binafsi katika Bandari ya Dar es Salaam

Tarehe 22 Oktoba, 2023, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisaini mikataba ya uwekezaji na Kampuni ya DP World MEA FZE ya Falme ya Dubai. Lengo lilikuwa ni kuboresha ufanisi wa uendeshaji wa huduma za Bandari ya Dar es Salaam na kuongeza makusanyo ya mapato ya moja kwa moja na yasiyo ya moja kwa moja yatokanayo na huduma za bandari. Pamoja na umiliki wa magati hayo na bandari kwa ujumla kubaki kwa Serikali, Kampuni hiyo ilikasimiwa jukumu la kuwa mwendeshaji pekee wa gati namba 4 hadi 7 za Bandari ya Dar es Salaam na ilipewa haki ya kutumia ya gati namba 0 hadi 3 kwa muktadha wa kuipa Mamlaka ya Bandari Tanzania kuamua kuhusu matumizi ya magati hayo pindi yanapojitokeza mahitaji ya dharura ya kuhudumia meli na shehena zenye maslahi ya Taifa ikiwemo meli za matibabu kwa wananchi na meli vita..

Mkataba wa Uendeshaji umeipa DP World jukumu la kutekeleza Mpango wa Uwekezaji utakaotumia Shilingi bilioni 675 ndani ya kipindi cha miaka mitano (5). Katika kipindi kinachoanzia Januari, 2024 hadi sasa, Kampuni ya DP World imefanya uwekezaji wa awali katika maeneo mbalimbali ya uendeshaji ili kuboresha na kuongeza ufanisi wa huduma za bandari wenye thamani ya Shilingi bilioni 214.42. Maeneo yaliyowekezwa ni pamoja na:

i. Usimikaji wa mitambo nane (8) inayotambulika kama "*Rubber Tyred Gantry Crane-RTG";*

ii. Kununua mitambo miwili (2) aina ya *"Ship to Shore Gantry Cranes-SSG"*;

iii. Kununua *"terminal tractors"* ishirini na *"Generators" kubwa saba (7);* na

iv. Kufanya usanifu wa mfumo wa kisasa wa TEHAMA wa kuhudumia shehena.

Mafanikio yaliyopatikana kuanzia Mei 2024 hadi Machi 2025 kwa kulinganisha na kipindi kama hicho katika mwaka 2023/2024 ni pamoja na:

i. Kuhudumia tani milioni 16.870 ambayo ni zaidi ya asilimia 14 ya shehena ya tani milioni 14.824 iliyohudumiwa katika kipindi kama hicho kwa mwaka uliopita;

ii. Kuongezeka kwa idadi ya makasha yaliyohudumiwa na DP World kutoka makasha ya futi ishirini (TEUs) 159,807 kwa kipindi cha Mei 2022 hadi Machi 2023 hadi makasha (TEUs) 215,286 katika kipindi cha Mei 2024 hadi Machi 2025;

iii. Kupungua kwa wastani wa muda wa meli kusubiri nangani hadi wastani wa siku saba (7) kwa kipindi cha Mei 2024 hadi Machi 2025 kutoka wastani wa siku 46 kwa kipindi cha Mei 2023 hadi Machi 2024;

iv. Kwa upande wa meli za makasha, DP World imeondoa kabisa muda wa kusubiri nangani, hivyo meli za makasha hufunga moja kwa moja gatini pindi zinapowasili katika Bandari ya Dar es Salaam ikilinganishwa na wastani wa siku tano kwa mwaka 2023 kabla ya uwekezaji;

v. Uwekezaji uliofanywa na DP World umeiwezesha Mamlaka ya Bandari kukusanya jumla ya shilingi bilioni 89.165 zinazotokana na tozo ya pango na mrabaha; na Shilingi bilioni 204.961 zinazotokana na tozo ya matumizi ya miundombinu *(wharfage)*;

vi. Kuchangia kuongezeka kwa makusanyo ya mapato ya Serikali hususan yale yanayotokana na kodi kwa asilimia 18 kutoka wastani wa shilingi bilioni 850 kwa mwezi kwa mwaka 2023/24 hadi wastani wa shilingi trilioni moja (1) kwa mwezi kwa mwaka 2024/25; na

vii. Kupungua kwa gharama za matumizi ya Bandari ya Dar es Salaam kwa asilimia 37 kutoka wastani wa shilingi bilioni 262.153 kwa mwezi katika kipindi cha Mei 2023 hadi Machi 2024 hadi Shilingi bilioni 166.323 kwa mwezi katika kipindi cha Mei 2024 hadi Machi 2025.

### 5.2.8 Viwanja vya ndege

i. Kuwezesha uanzishaji wa kiwanda cha kuunganisha na kutengeneza ndege katika kiwanja cha Ndege cha Morogoro;

ii. Kukamilisha ufungaji wa taa za kuongozea ndege katika viwanja vya ndege vya Mtwara, Songea, Songwe na Dodoma uliowezesha viwanja hivyo kutoa huduma saa 24; na

iii. Kukamilisha ufungaji wa mashine 13 za ukaguzi wa mizigo na abiria katika viwanja vya ndege vya JNIA,

Kigoma, Shinyanga, Tanga, Lake Manyara na Iringa hali ambayo imewezesha kuimarika kwa ulinzi na usalama katika viwanja hivyo.

### 5.2.9 Udhibiti wa Usafiri wa Anga

i. Kukamilisha ufungaji wa mitambo ya mawasiliano ya sauti baina ya marubani na waongoza ndege (VHF Area Systems) katika viwanja vya ndege 12 vya JNIA, AAKIA, KIA, Arusha, Pemba, Mwanza, Dodoma, Kigoma, Tabora, Songwe, Mtwara na Tanga; na

ii. Kukamilisha ufungaji wa mitambo ya mawasiliano ya sauti (VHF relay stations) kwa ajili ya mawasiliano ya anga la juu katika vituo 18 vya Gairo (Morogoro), Matogoro (Songea), Michakaini (Pemba), Nambunga (Newala-Mtwara), Lolkisale (Arusha), Kwenjugo (Handeni-Tanga), Mwaseni (Rufiji-Pwani), Kitulo (Njombe), Kaluwe (Mbeya), Mwisi (Igunga-Tabora), Kasulu (Kigoma), Nyamanyama (Biharamulo - Kagera), Ndisso-Sitalike (Katavi), Muganza (Butiama-Mara), Mugumu (Serengeti), Oldean Malanja (Ngorongoro-Arusha), Lubuli (Dodoma) na Ng’holi (Dodoma).

### 5.2.10 Udhibiti wa Usafiri Ardhini

Kuunda mfumo jumuishi wa utoaji tiketi yaani SAFARI TIKETI kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Serikali Mtandao, Shirika la Reli Tanzania na Chama cha Wamiliki wa Mabasi (TABOA). Mfumo huu umerahisisha ukataji wa tiketi na kutunza taarifa za abiria na hivyo kuboresha huduma za usafiri wa umma kwa abiria kupata tiketi zao kwenye dirisha moja na kujichagulia usafiri wa daraja analomudu.

### 5.2.11 Udhibiti wa Usafiri na Usafirishaji Majini

i. Kuendelea na ujenzi wa Kituo Kikuu cha Uratibu wa Masuala ya Utafutaji na Uokozi Majini (MRCC) katika

Ziwa Victoria Mkoani Mwanza ili kuimarisha usalama wa usafiri ambapo utekelezaji umefikia asilimia 71;

ii. Kuendelea na ununuzi wa boti mbili za utafutaji na uokozi zitakazotumika katika Ziwa Victoria ambapo ujenzi umefikia asilimia 65 na unatarajiwa kukamilika Juni, 2025; na

iii. Kuendelea na ujenzi wa vituo vidogo vitatu vya utafutaji na uokoaji katika Ziwa Victoria katika maeneo ya Kanyala - Buchosa ambao umefikia asilimia 68, Nansio - Ukerewe asilimia 71 na Musoma Mjini asilimia 80.

#### 5.2.12 Huduma za Hali ya Hewa

i. Kukamilisha ununuzi na ufungaji wa rada tatu katika Mikoa ya Mtwara, Mbeya na Kigoma na kufanya Tanzania kuwa na rada tano za hali ya hewa. Kununuliwa na kufungwa kwa rada hizo, kumeimarisha shughuli za uangazi wa hali ya hewa nchini pamoja na utoaji wa tahadhari za matukio ya hali mbaya ya hewa; na

ii. Kuimarisha huduma za hali ya hewa kwa watumiaji wa Bahari ya Hindi na Maziwa Makuu ambapo kituo kipya kiliongezwa katika Bandari ya Karema, Ziwa Tanganyika na hivyo kuifanya Mamalaka ya Hali ya Hewa kuwa na jumla ya vituo tisa katika bandari zilizoko Unguja, Pemba, Dar es Salaam, Tanga, Mtwara, Mwanza, Kigoma, Karema na Itungi.

### 5.3 Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

Serikali imeendelea kupiga hatua kwenye nyanja ya mawasiliano na teknolojia ya habari kwa kuongeza wigo wa matumizi ya mtandao katika mawasiliano. Hatua zilizochukuliwa ili kuendelea kuimarisha sekta ni pamoja na kutekeleza mradi wa ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano na ujenzi wa minara ya

mawasiliano katika sehemu mbalimbali nchini. Kutokana na juhudi hizo mafanikio yafuatayo yamepatikana:

### 5.3.1 Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano

i. Kujenga Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kutoka kilomita 8,319 za mwaka 2020 hadi kilomita 13,820 mwaka 2025 ambapo vituo 111 vya kutolea huduma za mkongo vimekamilika. Ujenzi huo umewezesha Mkongo kufikishwa kwenye Wilaya 109 ikilinganishwa na Wilaya 36 zilizokuwepo mwaka 2020.

ii. Kuongeza wigo wa matumizi ya mawasiliano ya kasi *(broadband)* kutoka asilimia 45 mwaka 2020 hadi asilimia 74 mwaka 2025; na

iii. Kuwezesha ujenzi wa kiwanda cha kutengeneza nyaya za Mkongo wa Mawasiliano *(optic fibre)* kilichopo Mkuranga, Mkoa wa Pwani.

### 5.3.2 Anwani za Makazi Anwani za Makazi

i. Kutekeleza Mfumo wa Utambuzi wa Anwani za Makazi ambapo taarifa za anwani za makazi zimeongezeka kutoka 350,000 mwaka 2020 hadi 12,853,657 mwaka 2025, vibao vya namba ya nyumba vimeongezeka kutoka 300,125 mwaka 2020 hadi 7,440,812 mwaka 2025 na nguzo za majina ya barabara kutoka 9,842 mwaka 2020 hadi 229,961 mwaka 2025. Lengo ni kurahisisha utoaji, upokeaji na ufikishaji wa huduma hadi mahali stahiki na hivyo kuchochea maendeleo ya kijamii na kiuchumi pamoja na kuwezesha nchi kunufaika na fursa za uchumi wa kidijitali; na

ii. Kuboresha Mfumo wa Kidijitali wa Anwani za Makazi unaoitwa NaPA ili kuimarisha utekelezaji na matumizi yake ambapo hadi sasa mfumo huo umeunganishwa

na mifumo ya kidijitali 18 ya kutolea huduma na mingine zaidi ya 30 ipo katika hatua mbalimbali za kuunganishwa. Uunganishaji huu, unalenga kurahisisha ubadilishanaji wa taarifa na kuhakikisha mifumo ya kidijitali inasomana; Taarifa za anwani za makazi zimesaidia kuongeza ukusanyaji wa mapato, ufikishaji wa bidhaa na huduma mahali stahiki pamoja na kutumia taarifa hizo kuwatambua wahanga wa majanga, kama yaliyotokea Wilayani Hanang, Mkoani Manyara.

### 5.3.3 Mawasiliano ya Simu

i. Kuongeza minara ya mawasiliano kutoka minara 754 mwaka 2020 hadi 9,278 mwaka 2025 na hivyo kuongeza wigo wa upatikanaji wa mawasiliano kwenye maeneo yenye changamoto;

ii. Kuongeza usajili wa laini za simu kutoka 51,220,233 mwaka 2020 hadi 90,377,995 mwaka 2025. Ongezeko hili limewezesha kuongezeka kwa watumiaji wa simu na intaneti, hivyo kuwezesha watu kuwasiliana kwa urahisi pamoja na kuimarisha uchumi wa kidigitali;

iii. Kuongeza kiwango cha upatikanaji wa huduma za mawasiliano ya simu za viganjani kutoka asilimia 95 mwaka 2020 hadi asilimia 98.2 mwaka 2025; na

iv. Kupungua kwa gharama za matumizi ya huduma ya intaneti kutoka shilingi 24.28 kwa MB 1 mwaka 2020 hadi shilingi 9.3 kwa MB 1 mwaka 2025. Vilevile, gharama za kupiga simu ndani ya mtandao zimepungua kutoka shilingi 72 mwaka 2020 hadi shilingi 26 mwaka 2025 na gharama ya kupiga simu nje ya mtandao kutoka shilingi 73 mwaka 2020 hadi shilingi 28 mwaka 2025.

### 5.3.4 Ufanisi na Upatikanaji wa Huduma za Serikali

i. Kuunganisha mifumo 514 ya kutolea huduma Serikalini na Mifumo 384 ya kutolea huduma katika sekta binafsi.

Uunganishaji wa mifumo umewezesha wananchi kupata huduma kwa kutumia kitambulisho kimoja;

ii. Kuwezesha ujenzi wa mifumo mitano ya kitaifa ya kutolea huduma ya ubadilishanaji taarifa (Jamii X-change na ZanXchange) ambayo inasimamiwa na Mamlaka za Utambulisho (NIDA na ZCSRA); Mfumo wa utambuzi kidijitali (Jamii Namba); mfumo wa utambuzi wa wateja (e-KYC); Mfumo wa malipo ya kidijitali (Jamii Pay) na mfumo wa usajili na uwezeshaji wa wadau wa ikolojia ya tafiti na bunifu za TEHAMA;

iii. Kutunga Sheria ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi ya mwaka 2022 na Kanuni zake pamoja na kuanzisha Tume ya Ulinzi wa Taarifa Binafsi (PDPC);

iv. Kuandaa Mkakati wa Uchumi wa Kidijitali wa Miaka Kumi (2024 - 2034) na Mkakati wa Taifa wa Brodibandi (2021 – 2026) itakayowezesha utekelezaji wa uchumi wa kidijitali;

v. Kuendelea na ujenzi wa vituo nane vya kikanda vya ubunifu wa TEHAMA katika Mikoa ya Arusha, Mwanza, Tanga, Lindi, Dodoma, Pwani, Mtwara na Mjini Magharibi. Uwepo wa vituo hivyo utawezesha wananchi wenye ujuzi wa TEHAMA kuendeleza ujuzi wao hivyo kuwezesha ushiriki wao kwenye uchumi wa kidijitali na kuongeza ajira kupitia ujuzi huo;

vi. Kuimarisha miundombinu, kujenga na kusimamia uendeshaji wa Rasilimali Shirikishi za TEHAMA ikiwemo Mtandao wa Mawasiliano Serikalini *(GovNet)*, na vituo vya Serikali vya kuhifadhia Mifumo na Data za Masafa ya Intaneti. Hatua hii imesaidia kuondoa urudufu, kupunguza gharama na kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma pamoja na kuhakikisha uwepo wa usalama wa mawasiliano Serikalini;

vii. Kujenga Mfumo Mkuu wa kuiwezesha Mifumo ya TEHAMA Serikalini Kubadilishana Taarifa *(Government Enterprise Service Bus – GoVESB)*. Hatua hiyo imesaidia mifumo ya Serikali kuwasiliana na kubadilishana taarifa; na

viii. Tanzania *(GovTech Maturity Index)* kupanda daraja kutoka kundi B hadi kundi A na kushika nafasi ya pili (2) barani Afrika, ya kwanza Afrika Mashariki na 26 Duniani katika kuimarisha matumizi ya TEHAMA Serikalini. Hii ni kutokana na utafiti wa Benki ya Dunia kuhusu Ukomavu wa Matumizi ya Teknolojia Duniani katika Utoaji wa Huduma za Serikali na Ushirikishwaji wa Wananchi.

## 5.4 Nishati

Serikali imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha nchi inazalisha nishati ya kutosha ili kukidhi mahitaji ya ndani na kuuza ziada nje. Hatua hizo zimejumuisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji. Katika kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025, Serikali imeendelea kuhakikisha sekta ya nishati inaendelea kuimarika na kuwezesha nchi kuingia kwenye kundi la nchi zenye uchumi wa kipato cha kati. Katika kutekeleza hayo mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

### 5.4.1 Umeme

i. Kuongezeka kwa kiwango cha umeme uliounganishwa katika mfumo wa Gridi ya Taifa kutoka megawati 1,602.32 mwaka 2020 hadi megawati 4,031.71 mwaka 2025;

ii. Kukamilisha ujenzi wa miradi ya kuzalisha Umeme wa Julius Nyerere (JNHPP) – MW 2,115; Mradi wa kuzalisha umeme wa Kinyerezi I Extension MW 185 kwa kutumia Gesi Asilia; na Mradi wa Rusumo ambao umetekelezwa katika Mto Kagera kwa ushirikiano wa nchi tatu za Tanzania, Burundi na Rwanda kwa mgawanyo sawa wa umeme (MW 26.67). Ukamilishaji wa miradi hiyo

umeiwezesha nchi kuondokana na tatizo la upungufu wa umeme na kuchochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii, kukua kwa Pato la Taifa na kuimarisha mazingira ya uwekezaji na kufanya biashara nchini;

iii. Kukamilisha miradi ya usambazaji umeme ikiwemo mradi wa ujenzi wa njia za kusafirisha umeme yenye urefu wa kilomita 414 kutoka Singida - Arusha - Namanga (kilovoti 400); njia yenye urefu wa kilomita 144 kutoka Geita – Nyakanazi (kilovoti 220); njia ya kutoka Julius Nyerere hadi Chalinze (kilovoti 400/220/132); njia kutoka Nyakanazi hadi Kigoma (kilovoti 400); njia yenye urefu wa kilomita 115 kutoka Tabora - Urambo (kilovoti 132); njia yenye urefu wa kilomita 94 kutoka Rusumo-Nyakanazi (kilovoti 200); na njia ya kusafirisha umeme kwenye njia ya reli (Standard Gauge Railway – SGR - kilovoti 220);

iv. Kuendelea na ujenzi wa Mradi wa Umeme wa Jua – Megawati 50 katika Wilaya ya Kishapu, Mkoa wa Shinyanga ambao umefikia asilimia 48.6 mwaka 2025. Aidha, kukamilika kwa mradi huo kutaongeza vyanzo vya kuzalisha umeme nchini (*energy mix*) na uwezo wa mitambo ya kuzalisha umeme kwa kutumia nishati jadidifu (*nishati safi*) kufikia zaidi ya asilimia 70 na hivyo kuimarisha jitihada na mchango wa Tanzania wa kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa; na

v. Kufunga mtambo wa kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia wa MW 20 katika eneo la Hiyari – Mtwara.

### 5.4.2 Mafuta na Gesi

i. Kuongezeka kwa matumizi ya gesi asilia nchini kutoka futi za ujazo bilioni 59.83 mwaka 2020 hadi bilioni 82.91 mwaka 2025;

ii. Kuongeza ushiriki wa Shirika la Maendeleo ya Petroli (TPDC) katika Kitalu cha uzalishaji wa gesi asilia cha Mnazi Bay kutoka asilimia 20 hadi asilimia 40. Hii ni baada ya kununua asilimia 20 ya hisa za Kampuni ya Wentworth na hivyo kuongeza mapato na ushiriki katika maamuzi ya uendeshaji wa kitalu husika; na

iii. Kuimarisha miundombinu ya mtandao wa usambazaji wa gesi asilia nchini ambapo nyumba 151, taasisi 13 na viwanda 57 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi na Mtwara vimeunganishwa. Aidha, vituo vya kujaza gesi asilia (CNG filling stations) kwenye vyombo vya moto vimeongezeka kutoka vituo viwili (2) mwaka 2020 hadi tisa (9) mwaka 2025 na zaidi ya vyombo vya moto 15,000 vinatumia gesi asilia. Matumizi ya gesi asilia katika vyombo vya moto yamesaidia kupunguza mahitaji ya petroli na dizeli katika uendeshaji wa vyombo hivyo;

iv. Kuendelea na ujenzi wa mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP) lenye urefu wa kilomita 1,443 kutoka Hoima (Uganda) mpaka Tanga (Tanzania) ambapo kilomita 1,115 za bomba hilo zinapita hapa nchini. Utekelezaji wa mradi huo umefikia asilimia 55 na tayari Serikali imeshachangia mtaji wa dola za Marekani milioni 376 sawa na asilimia 15 ya hisa. Kupitia mradi huo, jumla ya ajira 6,763 zimezalishwa. Manufaa ambayo nchi yetu itapata kutokana na mradi huo ni pamoja na kutengeneza nafasi za ajira kwa watanzania, kuongeza mapato ya Taifa, kuhamisha na kuhawilisha matumizi ya teknolojia nchini na uboreshaji wa ukanda wa kati ya Uganda na Tanzania; na

v. Kuanza kutumika kwa mfumo wa kielekroniki wa “SCADA” katika usimamizi wa ushushaji wa mafuta nchini ambao

umewezesha kupunguza upotevu wa mafuta kutoka asilimia 0.5 mwaka 2020 hadi asilimia 0.1 mwaka 2025.

### 5.4.3 Nishati Safi ya Kupikia

Serikali imeendelea kutekeleza agenda ya matumizi ya nishati safi ya kupikia kwa lengo la kupunguza ongezeko la uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi pamoja na athari za kiafya zinazotokana na matumizi ya nishati isiyo safi ya kupikia katika nchi yetu. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuanza utekelezaji wa Mkakati wa Taifa wa Matumizi wa Nishati Safi ya Kupikia (2024 -2034) ambao tumelenga zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania kutumia nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2034;

ii. Kuunganisha nyumba 1,551, viwanda 57 na magari 5,000 kwenye mfumo wa gesi asilia pamoja na kusambaza majiko banifu 205,000 kwa wananchi na mitungi 452,445 ya gesi ya kupikia katika wilaya 139;

iii. Kuongezeka kwa vituo vya kujaza gesi asilia kwenye vyombo vya moto kutoka vituo viwili (2) mwaka 2020 hadi tisa (9) mwaka 2025 na zaidi ya vyombo vya moto 15,000 vinatumia gesi asilia; na

iv. Taasisi 903 zinazotoa huduma kwa umma zimeanza matumizi ya nishati safi ya kupikia.

# SURA YA SITA

## 6. UTUMISHI NA UTAWALA BORA

### 6.1 Utumishi

Serikali kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Usimamizi wa Utumishi wa Umma imehakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora. Mafanikio kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi mwaka 2025 ni pamoja na:

i. Kulipa madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi 150,647 yenye jumla ya Shilingi 252,760,066,271.61. Aidha, madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wastaafu 10,022 yenye jumla ya Shilingi 33,290,109,780.75 yalilipwa;

ii. Kupandisha vyeo watumishi wa umma 611,063, kubabadilisha kada watumishi 42,557, kupata uteuzi watumishi 3,253, kusafisha taarifa za kiutumishi 162,666, kubadilisha vyeo watumishi 10,974, kurekebisha majina watumishi 4,093, kufanya mabadiliko ya mshahara binafsi kwa watumishi 9,620, kurejesha kwenye utumishi wa umma watumishi 2,671 na kutoa ajira katika Taasisi mbalimbali za umma kwa watumishi 135,626. Aidha, jumla ya nafasi za ajira 155,008 zilitolewa na vibali vya ajira mbadala 41,673 vilitolewa ili kujaza nafasi zilizobaki wazi kwa sababu mbalimbali;

iii. Taasisi za umma 571 zimejengewa uwezo na kuwezesha utekelezaji wa Mfumo wa Usimamizi wa Utendaji Kazi

katika Utumishi wa Umma (mass rollout). Taasisi hizo zinajumuisha Wizara 27; Idara Zinazojitegemea 27; Wakala wa Serikali 27, Sekretarieti za Mikoa 26, Mamlaka za Serikali za Mitaa 184; na Taasisi na Mashirika ya Umma 280;

iv. Kupunguza kodi ya mapato (PAYEE) kutoka asilimia 9 mwaka 2020 hadi asilimia 8 mwaka 2024 na kuongeza kima cha chini cha mshahara kinachopaswa kukatwa kodi kutoka **Shilingi 170,000** hadi **270,000**. Kwa kufanya hivyo, Serikali ilisamehe kukusanya takribani shilingi bilioni 14.78 kwa mwaka kutoka kwa watumishi wa Umma na hivyo kusaidia watumishi kumudu gharama za maisha;

v. Kuongeza kima cha chini cha Mshahara kwa asilimia 35.1 mwaka 2025 kutoka asilimia 23.3 mwaka 2022 na hivyo kusababisha kima cha chini cha mshahara wa Mtumishi wa Umma kuwa shilingi 500,000 kuanzia Julai, 2025. Hatua hii imewezesha kuimarisha maisha wa wafanyakazi na kuongeza mchango wao katika maendeleo ya Taifa;

vi. Kuboresha umri wa watoto wategemezi wa mwanachama wa NHIF kwa kuongeza umri wa watoto wategemezi wa wanachama wa Mfuko huo kutoka miaka 18 hadi miaka 21 ambapo watoto 65,353 wamenufaika na jumla ya Shilingi 3,702,636,040 zimetumika katika matibabu yao;

vii. Kufuta tozo (retention fee) ya asilimia 6 iliyokuwa ikitozwa kutoka katika mishahara ya watumishi wa Umma walionufaika na Mikopo ya Elimu ya Juu. Kufutwa kwa tozo hiyo kumewezesha shilingi trilioni 1.1 kubaki kwa watumishi;

viii. Kuunda Mfumo wa Tathmini ya Watumishi wa Umma (*HR Assessment System*) ambao umesaidia kuandaa mahitaji ya watumishi;

ix. Kushughulikia masuala ya kiutendaji ambapo malalamiko 1,142 yalishughulikiwa kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi mwaka 2025. Kati ya hao, malalamiko 94 yalikubaliwa, 325 yalikataliwa, 64 yaliwasilishwa nje ya muda na 288 yalihitimishwa kwa kutolewa ufafanuzi;

x. Kuanzisha mfumo wa Kupima Uelewa na Ufahamu wa Wasailiwa kwa njia ya mtandao ***'Online Aptitude Testing System' (OATS).*** Mfumo huo umepunguza gharama za michakato ya ajira kwa waombaji kazi na kufanya usaili wa kuandika/mchujo kwa njia ya kielektroniki kupitia kwenye vituo vilivyo karibu na maeneo wanayotoka; kupunguza gharama za kudurufu maswali ya usaili, usahihishaji wa maswali na uhakiki wa maswali; na kupunguza siku za kuendesha michakato ya ajira kutoka zaidi ya 120 hadi pungufu ya 50;

xi. Kufanya marekebisho ya Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Sura 366, Sheria ya Taasisi za Kazi Sura 300, na Sheria ya Usimamizi wa Ajira za Wageni Sura 436 ili kukidhi mahitaji ya sasa. Hatua hii imeimarisha ustawi wa wafanyakazi;

xii. Kuongeza ufanisi wa utoaji wa vibali vya kazi kutoka miezi miwili (2) hadi siku 14 au chini ya muda huo uliopo kisheria kupitia mfumo wa *Online Work Permit Application and Issuance System –OWAIS.* Hatua hii imeongeza ufanisi kwa kuvutia wawekezaji wengi nchini*;* na

xiii. Kongeza ufanisi katika utoaji wa leseni za usajili kutoka siku 14 hadi siku moja (1) na upatikanaji wa ithibati kutoka siku 28 hadi siku moja (1) hadi tatu (3) kupitia Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Mahali pa Kazi (WIMS). Hatua hii imewezesha wananchi kupunguza matumizi ya rasilimali fedha na muda wa ufuatiliaji.

### 6.2 Utawala Bora na Mapambano Dhidi ya Rushwa

Mafanikio yaliyopatikana katika eneo la utawala bora na mapambano dhidi ya rushwa ni pamoja na

i. Kupungua kwa malalamiko ya ukiukwaji wa maadili kutoka 919 mwaka 2020 hadi 852 mwaka 2025. Kupungua huko kunaashiria kuongezeka kwa uadilifu miongoni mwa Viongozi na hivyo kuongeza imani ya Wananchi kwa Serikali yao katika kutoa huduma;

ii. Kufanya vizuri katika mapambano dhidi ya rushwa kwa kupata alama 41 na kushika nafasi ya 82 kati ya nchi 180 zilizofanyiwa utafiti, ikiwa imepanda kwa nafasi tano kutoka nafasi 175 ya mwaka 2023 ambapo ilipata alama 40. Aidha, Tanzania imeendelea kuimarika kwa mapambano dhidi ya rushwa ambapo imeshika nafasi ya pili katika kwa Ukanda wa Afrika Mashariki na nafasi ya 14 kwa nchi za Afrika kwa mujibu wa taarifa ya utafiti uliofanywa na Taasisi ya *Transparency International* mwaka 2024 na matokeo yake kutangazwa Februari, 2025;

iii. Kukamilika kwa ujenzi wa majengo ya ofisi za Mikoa ya Kilimanjaro, Simiyu na Iringa na Wilaya za Kilolo (Iringa), Kongwa (Dodoma), Kiteto (Manyara), Mvomero (Morogoro), Liwale (Lindi), Nyasa (Ruvuma), Momba (Songwe), Nzega (Tabora), Kishapu (Shinyanga), Rombo (Kilimanjaro), Monduli (Arusha) na Nkasi (Rukwa). Vilevile, ujenzi wa ofisi ya TAKUKURU kituo maalum Chalinze (Pwani) umekamilika ; na

iv. Kudhibiti na kuokoa kiasi cha Shilingi bilioni 211.95 na kurejeshwa Serikalini kupitia operesheni mbalimbali za uchunguzi wa tuhuma za rushwa. Aidha, mali zenye thamani ya Shilingi bilioni 35.688 zikijumuisha nyumba,

viwanja, magari na fedha taslimu Shilingi bilioni 1.17 zilitaifishwa. Sehemu ya fedha hizo ilitumika kutekeleza miradi ya maendeleo kama vile ujenzi wa vituo vya afya, ununuzi wa dawa na vifaa tiba, ujenzi wa shule na barabara ili kuleta ustawi wa wananchi na maendeleo endelevu ya Taifa.

### 6.3 Utawala wa Sheria

Sekta ya katiba na sheria ni mhimili mkuu katika kutoa haki kwa wananchi. Kutokana na umuhimu huo, Serikali imetekeleza mikakati mbalimbali iliyowezesha kupata mafanikio katika maeneo tofauti. Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuimarisha upatikanaji haki kwa watu wote kupitia huduma ya msaada wa kisheria na kampeni ya Msaada wa Kisheria ya *Mama Samia Legal Aid Campaign* – MSLAC ambayo imetolewa katika Mikoa 25 ya Tanzania Bara na Mikoa mitatu ya Zanzibar;

ii. Kuendelea kutoa elimu ya huduma ya Msaada wa Kisheria kwa jamii ambapo wananchi 2,698,908 katika Halmashauri 180, kata 1,907 na Vijiji/Mitaa 5,702 walifikiwa na huduma hiyo. Upatikanaji wa huduma hiyo umewasaidia wananchi kujua masuala ya haki na wajibu; umiliki na utatuzi wa migogoro ya ardhi; matunzo ya watoto; utatuzi wa migogoro ya ajira na mahusiano kazini; ukatili wa kijinsia; wosia, mirathi, ndoa na familia; usajili wa matukio muhimu ya binadamu; na haki za binadamu;

iii. Kuongezeka kwa mashirika yanayotoa msaada wa kisheria kutoka 84 mwaka 2020 hadi 377 mwaka 2025; na wasaidizi wa msaada wa kisheria kutoka 617 mwaka 2020 hadi 2,205 mwaka 2025. Ongezeko hilo linatokana na uboreshaji na uendelevu wa huduma ya msaada wa Kisheria;

iv. Kuanzisha madawati ya msaada wa kisheria katika mamlaka za Serikali za Mitaa 184. Madawati hayo yametoa ajira 449 na kutoa huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi 6,427,738. Aidha huduma imesajili migogoro 16,041 ambapo 7,889 ilipatiwa ufumbuzi na migogoro 8,152 inaendelea kufanyiwa kazi;

v. Kukamilisha ujenzi wa mfumo wa kielektoniki wa kutoa huduma za msaada wa kisheria. Mfumo huo unawezesha upokeaji wa taarifa za utekelezaji wa huduma za msaada wa kisheria kutoka kwa Mashirika ya Msaada wa Kisheria na kuhifadhi taarifa za utekelezaji wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia. Mfumo huo unalenga kurahisisha upatikanaji wa takwimu zinazotokana na utoaji wa huduma za msaada wa kisheria;

vi. Kukamilisha uhakiki wa sheria kuu 300 kati ya 446 zilizotafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili. Lengo ni kutumia lugha ya Kiswahili kwenye utoaji wa haki na kuwezesha wananchi kuelewa sheria za nchi;

vii. Kuimarisha Mifumo ya Utoaji Haki ili ipatikane kwa wote na kwa wakati kwa:

  a) Kuanzisha Kituo cha Huduma kwa wateja kwa ajili ya kurahisisha utoaji wa malalamiko kupitia namba 0262160360 na *Whatsapp* 0739101910;

  b) Kuongeza idadi ya Majaji na Mahakimu ili kuongeza kasi ya utendaji kazi ambapo Majaji ni 146 na Mahakimu ni 1,426;

  c) Kupungua mrundikano wa mashauri mahakamani ambapo hadi Aprili 2025 kulikuwa na mashauri 238,154. Kati ya hayo, mashauri 174,581 yalihitimishwa na 63,573 yako katika hatua

mbalimbali. Hii imefanya Tanzania kuwa nchi yenye mashauri machache mahakamani duniani;

d) Kukamilisha ujenzi wa jengo la Makao Makuu ya Mahakama, nyumba za Majaji, na kuendelea na ujenzi wa nyumba ya Jaji Mkuu Jijini Dodoma;

e) Kukamilisha ujenzi wa vituo jumuishi 6 vya utoaji haki vilivyopo Dodoma, Morogoro, Mwanza, Arusha, Kinondoni na Temeke, na kuendelea na ujenzi vituo 9 vilivyopo Katavi, Songea, Songwe, Njombe, Simiyu, Lindi, Singida, Tunduru, Korogwe, Ulanga, Pemba, Geita na Chamwimo – Dodoma;

f) Kukamilisha Ujenzi wa majengo ya Mahakama za Wilaya za Korogwe, Ulanga na Ubungo na kuendelea na ujenzi wa Mahakama za Wilaya za Kibiti, Ubungo, Nachingwea, Simanjiro, Hanang, Mbulu na Mkalama;

g) Kukamilisha ujenzi wa majengo ya mahakama za mwanzo katika maeneo ya Mtae (Tanga), Mkunya (Newala), Msanzi (Rukwa), Uyole (Mbeya), Mlimba (Morogoro), Mang'ula (Morogoro), Mtowisa (Rukwa), Laela (Rukwa), Haydom (Manyara), Ngerengere (Morogoro), Kimbe (Tanga), Nyakibimbili (Kagera), Matiri (Ruvuma), Kabanga (Kagera), Chanika (Dar es Salaam), Mahenge (Kilolo Iringa), Mahenge (Morogoro), Luilo (Ludewa Njombe), Kinesi (Rorya Mara), Newala (Mtwara), Usevya (Katavi), Madale (Dar es Salaam), Usevya (Mlele), Nyakibimbili (Bukoba), na Mahenge (Kilolo); na

h) Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa majengo 72 ya mahakama za mwanzo;

viii. Kuongeza Ofisi za Mashtaka kwenye Wilaya kutoka ofisi za mashtaka 50 mwaka 2020 hadi 108 mwaka 2025.

# SURA YA SABA

## 7. ULINZI NA USALAMA

Ulinzi na usalama katika Taifa ni nguzo na mhimili muhimu katika kuleta amani, maendeleo na ustawi wa Taifa. Kwa kutambua umuhimu huo, Serikali imeendelea kuweka mifumo ili kuhakikisha wananchi na Taifa linaendelea kuwa salama na lenye amani dhidi ya vitisho vya ndani na nje ya nchi. Jitihada hizo zimeendelea kuipa nchi sifa ya kuwa kisiwa cha amani barani Afrika na hivyo kuchangia katika kuimarisha uwekezaji, utalii, na maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na:

### 7.1 Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania na Jeshi la Kujenga Taifa

i. Jeshi la Ulinzi wa Wananchi wa Tanzania limeendelea kuwezeshwa kwa vifaa na mafunzo kwa askari ili kutekeleza majukumu yake ya msingi ikiwemo ulinzi wa Taifa na mipaka ya nchi; miradi ya kimkakati; na kusaidia katika ulinzi wa amani katika maeneo ya kikanda na kimataifa, uokoaji wa maafa yanapotokea, usambazaji wa chakula na dawa na usaidizi wa kijamii;

ii. Kuendelea kutumia njia za kidiplomasia na mazungumzo na nchi jirani ikiwemo Rwanda, Kenya, Uganda, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC), Malawi, Msumbiji na Zambia ili kuimarisha na kutatua changamoto za mipaka baina ya Tanzania na nchi hizo;

iii. Kufanya tafiti na uzalishaji wa vifaa mbalimbali vya kijeshi ikiwemo magari ya Nyumbu, bomu la kufukuza tembo kwa ushirikiano na taasisi za utafiti kama COSTECH, TIRDO na TAWIRI;

iv. Kutoa mafunzo ya uzalendo na uwezo wa kujitegemea kwa Jeshi la Akiba ambapo wananchi 213,790 walinufaika;

v. Kuboresha viwanda vya TATC (Nyumbu) na Mzinga ili kuimarisha uzalishaji wa vifaa vya kijeshi na kiraia;

vi. Kujenga nyumba 6,064 za askari ili kuboresha mazingira ya kazi kwa askari;

vii. Kutekeleza kilimo cha umwagiliaji katika maeneo ya JKT zikiwemo kambi za Chita na Mtabila kwa lengo la kuimarisha usalama wa chakula na kupunguza gharama za malezi ya vijana wawapo makambini; na

viii. Kujenga mahanga matatu (3) ya vijana wanaonufaika na mafunzo ya kijeshi na uzalendo katika vikosi vya Bulombola, Mtabila na Rwamkoma pamoja na maghala ya chakula katika vikosi vya Mlale na Itaka. Vilevile, kuboresha kambi ya JKT Kibiti Pwani, ambapo mahanga mapya yamejengwa. Aidha, vituo viteule vya JKT Misenyi na Chenene vimeboreshwa kwa kuchimba visima vya maji, kujenga minara ya kuweka matenki pamoja na kituo cha Afya.

### 7.2 Jeshi la Polisi

i. Kuongeza bajeti ya Jeshi la Polisi kutoka shilingi bilioni 564.53 mwaka 2020/2021 hadi shilingi trilioni 1.13 mwaka 2024/2025. Ongezeko hilo limeimarisha ufanisi wa Jeshi la Polisi katika kulinda usalama wa raia na mali zao;

ii. Kujenga miundombinu ya vituo vya polisi 472; kununua magari 431 na pikipiki 331; kupandisha vyeo Maofisa, Wakaguzi na Askari 10,363; na kuajiri askari wapya 16,009 kwa ajili ya kuimarisha usalama;

iii. Kujenga vituo sita (6) vya Polisi vya Daraja A kwa gharama ya shilingi 5,944,636,386.00 katika maeneo ya Gezaulole

na Mburahati Dar es salaam, Lindi, Ikungi (Singida), Mtumba (Dodoma), na Wanging'ombe (Njombe); vituo nane (8) vya Daraja B vyenye thamani ya shilingi 367,581,815,076.00 vilivyopo Lushoto (Tanga), Mkalama (Singida), Mkoani Kusini Pemba, Makunduchi (Kusini Unguja), Ludewa (Njombe), Ruangwa (Lindi); na vituo 18 vya Daraja C vyenye thamani ya shilingi 2,079,761,615.00 ikiwa ni pamoja na Malya (Mwanza), Uwanja wa ndege Dodoma, Mpasa (Rukwa), Songambele (Tabora), Shirati Tarime (Mara) na Shehia ya Matangatuani Kaskazini Pemba;

iv. Kupanga askari katika kata 3,961 na shehia 388 kwa ajili ya kusogeza huduma za Polisi na kulinda usalama wa raia na mali zao;

v. Kukamata watuhumiwa 443 waliojihusisha na makosa ya kupatikana na silaha 2,498 na risasi 479 ambao walifikishwa mahakamani;

vi. Kupungua kwa kesi za jinai zilizoripotiwa katika vituo vya Polisi kutoka kesi 54,233 mwaka 2020 hadi kesi 51,875 mwaka 2025; na

vii. Kukamata nyara za Serikali 6,492 zenye uzito wa tani 4,981, kilogramu 842 na gramu 339 pamoja na watuhumiwa 10,790 kutokana na operesheni mbalimbali zilizofanyika nchini

### 7.3 Jeshi la Magereza

i. Kuendelea na ujenzi wa Hospitali Kuu ya Kanda ya Jeshi la Magereza Dodoma ambayo ikikamilika itatoa huduma za watumishi wa Jeshi la Magereza, wafungwa, mahabusu na jamii inayozunguka eneo hilo;

ii. Kupandisha vyeo maafisa waandamizi na askari 14,733, kuajiri askari wapya 3,404 na kununua magari 38 yenye thamani ya shilingi bilioni 7.46. Maboresho hayo yamechangia kupunguza uhaba wa rasilimali watu, usafirishaji wa mahabusu na kuboresha utendaji kazi wa Jeshi la Magereza;

iii. Kulipa madeni ya watumishi 2,676 na wastaafu 155 yenye thamani ya shilingi bilioni 2.58. Malipo hayo yameongeza ari na morali ya kazi kwa watumishi wa Jeshi la Magereza nchini;

iv. Jeshi la Magereza kuanza matumizi ya TEHAMA ya Mahakama Mtandao ambapo jumla ya magereza 66 yanatumia mfumo huo. Hatua hiyo, inarahisisha usikilizaji wa kesi bila wafungwa kusafirishwa hadi mahakamani; na

v. Kununua zana za kilimo ikiwemo trekta mbili zenye thamani ya shilingi milioni 100 na kujenga majosho mawili yenye thamani ya shilingi milioni 53 katika Magereza ya Wami Vijana na Bariadi ili kupunguza utegemezi wa chakula.

### 7.4 Jeshi la Zimamoto na Uokoaji

i. Kununua magari 50 ya zimamoto na utawala yakiwemo mawili yenye ngazi kwa majengo marefu, boti mbili za uokoaji, magari 6 ya kubeba maji na kujenga vituo vipya 11 ili kuongeza uwezo wa kukabiliana na majanga;

ii. Kukamilika kwa vituo vipya vya Zimamoto na Uokoaji vya Nzuguni, Dodoma kilichogharimu shilingi bilioni 1.25, Kituo cha Zimamoto Chamwino kilichogharimu shilingi bilioni 1.19, Kituo Kikuu cha Zimamoto Mchicha, Dar es Salaam kimegharimu shilingi bilioni 2.39 pamoja na ukarabati wa Kituo cha Zimamoto na Uokoaji cha Ilala,

Dar es Salaam kilichogharimu Shilingi milioni 273.7. Vituo hivyo, vimeongeza uwezo wa Jeshi kufikia maeneo ya dharura kwa wakati na kuboresha huduma kwa wananchi;

iii. Kuendelea na ujenzi wa vituo vya Zimamoto na Uokoaji vya Mji wa Serikali Mtumba, Dodoma ambao ujenzi umefikia asilimia 50.53; vituo vipya saba (7) katika Mikoa ya Manyara, Njombe, Kagera, Katavi, Geita, Simiyu na Songwe ambapo ujenzi ni kati ya asilimia 38 hadi 71; na ghorofa nane (8) za makazi ya askari Kikombo, Dodoma. Kukamilika kwa makazi hayo, kutaboresha maisha ya askari na kuongeza ari ya kazi; na

iv. Kupandisha vyeo Maafisa na Askari 1,505, kuajiri askari wapya 723 na kutoa mafunzo ya ndani na nje ya nchi kwa maafisa na askari 2,475 na hivyo kuendelea kuboresha utendaji kazi katika Jeshi hilo.

**7.5 Idara ya Uhamiaji**

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuimarisha doria, misako na operesheni katika maeneo mbalimbali nchini na hivyo kukamata watu 97,538 kwa makosa ya kiuhamiaji ambapo wamechukuliwa hatua mbalimbali za kisheria na wengine kuondoshwa nchini;

ii. Kupandisha vyeo Makamishna watano (5); Naibu Makamishna 17; Makamishna Wasaidizi Waandamizi 31; Maafisa, Wakaguzi, Askari 3,115; na Watumishi wa Kada ya Kiraia 213; na kuajiri askari 2,251 kwa ajili ya kuimarisha nguvu ya utendaji;

iii. Kulipa shilingi bilioni 11,903,984,041.15 pamoja na kiasi cha Dola za Marekani 23,483 kwa ajili ya malipo ya madeni ya watumishi na wazabuni waliotoa huduma

mbalimbali. Vilevile, kulipa shilingi 1,796,921,829.69 kwa ajili ya malipo ya stahiki za malimbikizo ya mishahara kwa maafisa, askari na watumishi wa kada za kiraia 971;

iv. Kuendelea na ujenzi wa Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Geita, Mtwara na Lindi pamoja na mradi wa Chuo cha Mafunzo cha Uhamiaji cha Raphael Kubaga kilichopo Boma Kichakamiba Wilaya ya Mkinga Mkoani Tanga; na

v. Kukarabati Ofisi za Uhamiaji katika Mikoa ya Mara, Dar es Salaam (Kurasini) na Morogoro pamoja na nyumba za makazi ya askari katika Mikoa ya Tabora na Pwani.

### 7.6 Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA)

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kusajili watu 3,581,830 na kufanya watu waliosajiliwa kufikia 25,634,890 sawa na asilimia 81.4 ya watu 31,477,938 wenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea. Mafanikio hayo, yametokana na kusogeza huduma za usajili na utambuzi karibu na makazi ya watu kwa kuanzisha Ofisi za usajili za wilaya na vituo vya usajili 142 Tanzania Bara na 11 Zanzibar;

ii. Kuzalisha vitambulisho 14,987,162 na hivyo kufanya vitambulisho vilivyozalishwa kufikia 21,266,895 tangu kuanza kwa usajili mwaka 2012. Mafanikio ya uzalishaji na usambazaji wa vitambulisho yametokana na kutoa fedha jumla ya shillingi 60,078,313,987.78 kwa ajili ya kuimarisha uzalishaji wa vitambulisho;

iii. Kuunganisha Ofisi za usajili za wilaya 22 na Kituo cha Uchakataji wa Taarifa na kufanya ofisi za usajili zilizounganishwa kufikia 153. Lengo ni kuwezesha mawasiliano kati ya ofisi za usajili, na kuhakikisha

maombi ya watu wote waliosajiliwa yanasafirishwa kutoka Ofisi za Usajili za Wilaya kwenda Kituo cha Kuchakata Taarifa *(Data Center)* kwa ajili ya uchakataji na uzalishaji vitambulisho kwa wakati;

iv. Kuunganisha Taasisi 68 za Umma na Binafsi katika mfumo wa Usajili na Utambuzi hivyo, kufanya Taasisi zilizounganishwa kufikia 124. Lengo ni kuwezesha uhakiki wa taarifa za wananchi wanaohitaji huduma katika taasisi hizo, kuongeza ufanisi wa utendaji ili kuleta maendeleo ya kiuchumi na kijamii katika ulinzi na usalama wa nchi; na

v. Kununua magari 30 yaliyogharimu shilingi 4,366,649,600 kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za usajili na utambuzi wa watu katika Ofisi za usajili za wilaya Tanzania Bara na Zanzibar.

# SURA YA NANE

## 8. USHIRIKIANO WA KIKANDA NA KIMATAIFA

Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kutilia mkazo utekelezaji wa diplomasia ya uchumi kwa vitendo ili kuhakikisha Taifa linaendelea kunufaika na fursa zipatikanazo katika maeneo ya kiuchumi, kijamii na kisiasa. Aidha, imeendelea kushiriki katika majadiliano ya kimataifa na jumuiya za kikanda na kuratibu ziara za kikazi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa nje ya nchi na viongozi wakuu wa mataifa mengine pamoja na wawakilishi wa mashirika ya kimataifa hapa nchini. Mafanikio yaliyopatikana kutokana na hatua hizo ni pamoja na:

i. Kukamilisha Sera ya Mambo ya Nje ya Mwaka 2001 Toleo la Mwaka 2024 itakayosaidia kuimarisha ushirikiano wa kidiplomasia na kiuchumi ili kutumia fursa zilizopo;

ii. Kuimarika kwa ushirikiano wa kimataifa ambapo Tanzania ilishiriki katika mikutano 312 ya kikanda na kimataifa ikiwemo Mkutano wa G20 ulioazimia kuunga mkono upatikanaji wa nishati safi na kuimarisha uwekezaji kwenye kilimo,

iii. Kushika Uenyekiti wa Asasi ya Siasa, Ulinzi na Usalama ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika, yenye jukumu la kusimamia masuala ya ulinzi na usalama katika Kanda hiyo, ambapo mbali na masuala mengine tumeweza kusimamia uangalizi wa chaguzi kwenye Nchi za Botswana, Mauritius, Msumbiji na Namibia;

iv. Kushiriki kwenye maonesho na makongamano muhimu ya biashara na uwekezaji nje ya nchi ikiwemo maonesho ya Dubai Expo 2020 nchini UAE, Maonesho ya Wajasiriamali

wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (JuaKali/NguvuKazi), Kongamano na Maonesho ya Petroli ya Afrika Mashariki pamoja na maonesho ya kimataifa ya China, Shanghai Guangzhou na *Japan Speciality Coffee Conference and Exhibition 2022*;

v. Kufanya ziara katika nchi mbalimbali ikiwemo China kwa lengo la kuimarisha uchumi, kuimarisha uhusiano wa kidplomasia na kufungua milango ya masoko ya bidhaa mbalimbali ikiwemo mihogo mikavu, soya, mazao ya baharini, asali, pilipili na mashudu ya alizeti. Aidha, ziara nchini Korea iliwezesha upatikanaji wa fedha zenye masharti nafuu kiasi cha Dola za kimarekani bilioni 2.5. kwa ajili ya miradi ya maendeleo;

vi. Tanzania kuwa mwenyeji wa mikutano mikubwa ya kimataifa ikiwemo Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Matumizi ya Nishati Safi ya Kupikia Barani Afrika, na Tanzania kuwa mwenyekiti mwenza wa mkutano huo iliyochangia upatikana kwa fursa za ajira na ujuzi, kuimarika kwa diplomasia ya mikutano, na kuwa na fursa za masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi;

vii. Kuhamasisha matumizi ya Kiswahili kama lugha ya diplomasia katika jumuiya za kikanda na kimataifa ikiwa ni pamoja na kuwezesha Shirika la Umoja wa Mataifa la Elimu na Sayansi (UNESCO) kuitangaza tarehe 7 Julai ya kila mwaka kuwa Siku ya Kiswahili Duniani. Hii ni hatua nzuri ya kufikia lengo la kukifanya Kiswahili kuwa miongoni mwa lugha zitakazotumika na Umoja wa Mataifa;

viii. Kuandaa ushiriki wa Watanzania 5,754 katika vikosi vya kulinda amani;

ix. Kuwawezesha wafanyabiashara wa Tanzania kufikia soko kubwa la Afrika lenye idadi ya watu wapatao bilioni 1.3 baada ya nchi kuridhia Mkataba wa Uanzishwaji wa

Eneo Huru la Biashara la Afrika. Aidha, biashara kati ya Tanzania na nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki iliongezeka kwa asilimia 61.1;

x. Kuongezeka kwa upatikanaji wa masoko ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi kutoka Dola za Marekani milioni 6,371.7 mwaka 2020 hadi Dola za Marekani milioni 7,696.6 mwaka 2023 sawa na ongezeko la asilimia 82.8;

xi. Kuongezeka kwa mchango wa diaspora kutoka Dola za Marekani Milioni 569.3 mwaka 2021 hadi Dola za Marekani milioni 751.6 mwaka 2023. Sambamba na hilo, kumekuwa na mwamko wa diaspora kuwekeza katika sekta za uchumi na jamii ikiwemo kilimo, elimu, afya, milki (real estate) na sekta ya fedha;

xii. Kuwezesha ufunguzi wa Balozi mpya mbili (2) za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambazo ni Uwakilishi wa Kudumu wa Tanzania Vienna-Austria na Ubalozi wa Jakarta-Indonesia. Aidha, ufunguzi wa Konseli Kuu mbili (2) katika Jiji la Lubumbashi, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Jiji la Guangzhou, Jamhuri ya Watu wa China ili kusogeza huduma karibu na kuimarisha mahusiano na nchi hizo. Hatua hii imeifanya Tanzania kuwa na jumla ya Balozi 45 na Konseli Kuu tano (5). Vilevile, maandalizi ya kufungua tena ubalozi wa Tanzania Luanda – Angola yamekamilika; na

xiii. Kushawishi nchi tano (5) kufungua ofisi za Konseli Kuu Zanzibar ambazo ni Umoja wa Falme za Kiarabu, Msumbiji, China, India na Oman. Aidha, nchi saba (7) zimefungua ofisi za Ubalozi wa Heshima ambazo ni Ufaransa, Uingereza, Italia, Ujerumani, Hispania, Uswidi na Brazil. Hatua hii inarahisisha upatikanaji wa huduma za kikonseli, viza na kuchagiza ukuaji wa biashara, utalii na uwekezaji kati ya Tanzania na nchi hizo.

# SURA YA TISA

## 9. URATIBU WA MASUALA MBALIMBALI

### 9.1 Muungano

Serikali imeendelea kulinda, kuthamini, na kudumisha Muungano ili kuimarisha amani, umoja na usalama, pamoja na kuleta maendeleo na hivyo kuwezesha wananchi kufurahia matunda yake. Kwa kuzingatia umuhimu huo, hatua mbalimbali zimechukuliwa na kuleta mafanikio yafuatayo:

(i) Kuondolewa kwa hoja 15 kati ya 18 kwenye orodha ya hoja za Muungano;

(ii) Kufanya vikao 69 vya ushirikiano vya kujadili mambo yasiyo ya Muungano baina ya Taasisi na Idara zisizo za Muungano za SJMT na SMZ ili kuleta ufanisi na uwiano wa maendeleo kwa pande zote mbili za Muungano; na

(iii) Kutoa fedha kiasi cha shilingi bilioni 6.234 kwa ajili ya Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya majimbo ya uchaguzi Zanzibar.

### 9.2 Mazingira

Serikali imeendelea kutekeleza mikakati na kampeni za kukabiliana na uharibifu wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi kwa kutekeleza miradi na programu mbalimbali zilizoshirikisha wadau katika kulinda na kuhifadhi mazingira. Mafanikio yaliyopatikana katika sekta hii ni pamoja na:

i. Kutekeleza Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022 – 2032) ambao

umeainisha hatua za kimkakati zinazopaswa kuchukuliwa ili kukabiliana na changamoto za Mazingira kwa kuzingatia jiografia na mifumo ya ikolojia ya maeneo husika nchini;

ii. Kurejeshwa kwa ardhi iliyoharibika kutokana na uharibifu wa mazingira ambapo hekta 28,706 zimetengwa kuwa hifadhi ya misitu ya jamii na hekta 106,199.65 kati ya hekta 110,000 zimewekwa kwenye mkakati wa urejeshwaji;

iii. Kuimarisha Miundombinu ya Fukwe ili kuhimili athari za mabadiliko ya Tabianchi zitokanazo na ongezeko la kina cha Bahari katika Fukwe za Sipwese–Pemba na Mikindani – Mtwara kwa kujenga miundombinu 13 kuzuia maji kujaa kwenye bahari na kuingia kwenye maeneo ya uzalishaji yenye urefu wa mita 70 hadi 65; ukuta wa zege wenye urefu wa mita 190 eneo 15 la Mikindani, Mtwara; matuta makubwa mawili (2) ya kuzuia maji ya bahari kuingia sehemu za mashamba katika maeneo ya Sipwese, Pemba na Mikindani;

iv. Kuandaa Kanuni na Mwongozo wa Taifa wa Usimamizi wa Biashara ya Kaboni ili kuweka utaratibu na masharti yanayopaswa kuzingatiwa kwa wadau na wajasiriamali wakati wa utekelezaji wa miradi ya biashara ya kaboni. Aidha, miradi 73 inatekelezwa katika maeneo mbalimbali na hivyo kuwezesha wananchi kupata gawio la mauzo ya kaboni la Shilingi milioni 45; na

v. Kutekeleza kampeni ya upandaji miti kitaifa ambapo jumla ya miti 691,523,763 ilipandwa na kustawi katika Mikoa 26 na Halmashauri 184.

### 9.3 Shughuli za Vyama vya Siasa

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: -

i. Kufanya marekebisho ya Sheria ya Vyama vya Siasa ya Sura Na. 258 na Sheria ya Gharama za Uchaguzi Sura Na. 278 kwa lengo la kuimarisha utawala wa demokrasia nchini;

ii. Kuondoa zuio la mikutano ya hadhara ya Vyama vya Siasa kwa kupitisha Kanuni ya kuratibu mikutano ya hadhara hivyo kuwezesha vyama vya siasa kuendesha shughuli za kisiasa ikiwemo kunadi sera zao;

iii. Kufanya mikutano maalum sita ya Baraza la Vyama vya Siasa na wadau wa demokrasia ya vyama vingi vya siasa nchini ambayo imewezesha mawazo na ushauri mbalimbali kutolewa na kuwasilishwa Serikalini; na

iv. Kutoa ruzuku ya Shilingi bilioni 87.81 kwa vyama vya siasa vyenye sifa ya kupata ruzuku kwa lengo la kuendesha shughuli za vyama.

### 9.4 Uratibu wa Maandalizi ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: -

i. Kutunga Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani Na. 1 ya Mwaka 2024 pamoja na Sheria ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi Na. 2 ya Mwaka 2024. Aidha, kutunga Kanuni za Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura za Mwaka 2024, Kanuni za Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025, na Kanuni za Maadili ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani za Mwaka 2025. Sheria na kanuni hizi zitasaidia kurahisisha usimamizi na uendeshaji wa uchaguzi nchini;

ii. Kuendesha chaguzi ndogo 10 ambazo zilihusisha nafasi za ubunge katika Majimbo tisa (9) na udiwani katika Kata 97. Chaguzi hizi ziliratibiwa vizuri na kufanyika kwa amani na utulivu;

iii. Kuongeza vituo vipya vya kuandikisha wapiga kura kutoka 37,814 mwaka 2020 hadi vituo 40,170 mwaka 2025. Ongezeko hili limesogeza karibu vituo vya kuandikisha wapiga kura kwa lengo la kurahisisha ushiriki wa wananchi katika shughuli za uchaguzi;

iv. Kuboresha Mifumo ya Uchaguzi ikiwa ni pamoja na Mfumo wa Uandikishaji Wapiga Kura (VRS); Mfumo wa Kuanzisha Mchakato wa Kuboresha Taarifa za Mpiga Kura kwa Njia ya Mtandao (OVRS); Mfumo wa Usajili wa Waangalizi, Asasi za Kiraia na Vyombo vya Habari(AMS); Mfumo wa Daftari la Wapiga Kura( PNVRS); Mfumo wa Menejimenti ya Logistiki na Ugavi (WLMIS); Mfumo wa Ramani za Kijiografia (GIS); Mfumo wa Menejimenti ya Matokeo (RMS); Mfumo wa Menejimeti za Wagombea (CMS); na Mfumo unaomwezesha Mpiga Kura kuhamisha taarifa zake na Kupiga Kura tofauti na kituo alichojiandikisha (KRP); na

v. Kukamilisha uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza ambao ulihusisha mizunguko 13 kwa mikoa yote ya Tanzania bara na Zanzibar. Kazi inayoendelea katika awamu ya pili ni uandikishaji wa wafungwa waliopo magerezani na wanafunzi waliopo vyuo vya mafunzo wenye kifungo kisichozidi miezi sita.

## 9.5 Uratibu wa Shughuli za Maafa

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na**;**

i. Kuendelea na ujenzi wa Kituo cha Taifa cha Usimamizi wa Maafa Jijini Dodoma kwa lengo la kuimarisha na

kuendeleza mbinu jumuishi katika uratibu na usimamizi wa maafa nchini;

ii. Kuboresha Mfumo wa Usimamizi wa Maafa ambao umezingatia mifumo ya Serikali iliyopo katika ngazi zote, mahitaji ya sasa na baadaye. Maboresho hayo yanalenga kuimarisha uwajibikaji wa pamoja wa wadau wote ndani na nje ya Serikali na kuimarisha uwezo wa kitaifa katika kuzuia na kupunguza madhara ya maafa, kujiandaa na kukabiliana na maafa, pamoja na kurejesha hali pindi maafa yanapotokea;

iii. Kuanzisha Kituo cha Taifa cha Operesheni na Mawasiliano ya Dharura na Chumba cha Ufuatiliaji wa Mwenendo wa Majanga na Tahadhari ya Mapema. Kituo hicho kimeunganishwa na vituo vya kisekta ili kufuatilia mwenendo wa majanga, kupokea na kuchambua taarifa za tahadhari na dharura kwa ajili ya usimamizi wa maafa nchini;

iv. Kuanzisha Mfuko wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa kwa ajili ya ugharamiaji wa maafa wakati wa dharura na hivyo kuwezesha utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa maafa kabla, wakati na baada ya maafa kutokea; na Kurejesha hali iliyosababishwa na Maafa ya maporomoko ya tope Wilaya ya Hanang' Mkoani Manyara, ambapo Serikali ilijenga nyumba 109 za kudumu kwa ajili ya waathirika maporomoko ya ya tope ya Wilayani Hanang'.

### 9.6 Masuala ya VVU na UKIMWI

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na;

i. Kuandaa Mkakati wa Tano wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI *(National Multi Sectoral HIV and AIDS Framework, Five - NMSF V 2021/22 – 2025/26)*. Mwongozo huu umeainisha

majukumu ya kila sekta katika udhibiti wa UKIMWI nchini;

ii. Kufanyika kwa utafiti wa viashiria na matokeo ya VVU na UKIMWI *(Tanzania AIDS Impact Survey - THIS)* mwaka 2022/2023. Utafiti huu ulipima matokeo ya juhudi za mapambano dhidi ya UKIMWI na kuonesha kuwa kiwango cha ushamiri wa VVU kimepungua kutoka asilimia 4.7 mwaka 2016/17 hadi asilimia 4.4 mwaka 2022/23. Vilevile, mwelekeo mzuri wa kufikia shabaha za kitaifa na kimataifa za 95-95-95 ifikapo 2026, ambapo utafiti umeonesha kuwa Taifa limefanikiwa kuvuka lengo kwenye utekelezaji wa shabaha ya asilimia 95 ya pili inayohusu Tiba kwa WAVIU waliotambua hali zao ambapo asilimia 98 ya WAVIU wapo kwenye Tiba. Pia, utafiti katika shabaha ya asilimilia 95 ya Tatu inayohusu kufubaza Virusi kwa WAVIU wanaoendelea na tiba, asilimia 94 ya WAVIU ambao wapo kwenye tiba wamefubaza VVU. Aidha, katika kufikia shabaha ya asilimia 95 ya kwanza inayohusu watu wote wanoishi na VVU kupima na kujua hali zao za maambukizi, asilimia 82.7 ya watu wanoishi na VVU nchini wanaojua hali zao za maambukizi ya VVU;

iii. Kupungua kwa maambukizi mapya kutoka watu 72,000 mwaka 2016/17 hadi watu 60,000 mwaka 2022/23;

iv. Kupungua kwa kiwango cha maambukizi ya VVU kwa watu wazima kutoka asilimia 4.7 mwaka 2016/17 hadi asilimia 4.4 mwaka 2022/23; na

v. Kupungua kwa vifo vitokanavyo na UKIMWI kutoka 64,000 mwaka 2010 hadi 23,215 mwaka 2024.

### 9.7 Uratibu wa Shughuli za Afua za Lishe

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na;

i. Kutekeleza mpango wa utoaji chakula shuleni ambapo

hadi sasa zaidi ya asilimia 60 ya shule zote nchini zinatoa chakula kwa wanafunzi shuleni;

ii. Tanzania kuwa nchi pekee katika nchi za Afrika zilizo ukanda wa Mashariki, Kati na Kusini ambayo inatumia maabara yake ya Taifa kufanya uchambuzi wa sampuli zote zinazohusu masuala ya chakula na lishe zilizokusanywa katika Utafiti wa Kitaifa wa Demografia na Afya wa Mwaka 2022 *(Tanzania Demographic and Health Survey – TDHS 2022)*;

iii. Kujengwa kwa kiwanda cha virutubishi kupitia Kampuni ya SANKU kwa ajili ya urutubishaji wa vyakula nchini na barani Afrika; na

iv. Kuanzisha mashine vinyunyizi (disiefire) kupitia shirika la Viwanda Vidogo Vidogo SIDO kwa ajili ya kuchanganya virutubishi kwenye chakula.

## 9.8 Mapambano Dhidi ya Dawa za Kulevya

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kukamilisha na kuanza utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya ya Mwaka 2024 ili kuimarisha uwezo wa nchi katika kudhibiti na kupambana na biashara na matumizi ya dawa za kulevya;

ii. Kupunguza uingiaji, uzalishaji na usambazaji wa dawa za kulevya kwa kubaini na kudhoofisha mitandao ya wafanyabiashara wa dawa za kulevya pamoja na kukamata jumla ya Kilogramu 4,697,511.35 za dawa za kulevya zikihusisha watuhumiwa 25,715;

iii. Kuanzisha ofisi tano za Kanda katika Mikoa ya Arusha (Kanda ya Kaskazini), Mwanza (Kanda ya Ziwa), Mtwara (Kanda ya Pwani), Mbeya (Kanda ya Nyanda

za Juu Kusini) na Dodoma (Kanda ya Kati) ili kuimarisha mapambano dhidi ya biashara na matumizi ya dawa za kulevya kutoka Ofisi mbili za Kanda zilizokuwepo kuanzia mwaka 2020;

iv. Kuongeza vituo vya utoaji huduma za tiba kwa waraibu wa dawa za kulevya kutoka vituo tisa mwaka 2020 hadi 18 mwaka 2025 katika Mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Tanga, Morogoro, Songwe, Mbeya, Dodoma, Mwanza na Arusha. Hivyo, kuongeza waraibu waliosajiliwa kutoka 9,188 mwaka 2020 hadi 18,170 mwaka 2025; na

v. Kuanzisha Maabara ya Uchunguzi na Sayansi Jinai ili kuokoa gharama kubwa zinazotumika katika uchunguzi wa sampuli ambapo sampuli moja (1) hugharimu Dola za Marekani 100.

### 9.9 Serikali Kuhamia Dodoma

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuendelea na ujenzi wa majengo ya ofisi za Wizara na Taasisi katika Mji wa Serikali, Mtumba Awamu ya Pili ambapo hadi Aprili, 2025 wastani wa ukamilishaji wa majengo umefikia asilimia 90.1. Aidha, kati ya majengo 34 yaliyo katika Mji wa Serikali, majengo sita (6) yamekamilika;

ii. Ujenzi wa miundombinu ya kudumu katika Mji wa Serikali ambapo:

    a) Ujenzi wa Barabara za lami zenye urefu wa Kilomita 59.1 umekamilika; na upembuzi yakinifu wa barabara inayounganisha Mji wa Serikali na Ikulu yenye urefu wa kilomita 9.9 pia umekamilika;

    b) Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya kudumu ya umeme inayopita chini ya ardhi yenye urefu

wa Kilomita 42 ya msongo wa kilovoti 33 ambao umefikia asilimia 55;

c) Kukamilika kwa usambazaji na usimikaji wa miundombinu ya mtandao wa mawasiliano; na

d) Kuendelea na ufungaji wa mifumo ya kamera za usalama (CCTV) ambao umefikia asilimia 47.

iii. Kukamilika kwa awamu ya kwanza ya ujenzi wa Uwanja wa Mashujaa iliyohusisha ujenzi wa uwanja wa gwaride.

### 9.10 Sera na Uratibu wa Shughuli za Serikali

i. Kuandaa Mwongozo wa Uratibu na Usimamizi wa Utekelezaji wa Sera ambao unalenga kuimarisha mfumo wa uratibu wa uandaaji na usimamizi wa utekelezaji wa sera kwa kuweka utaratibu wa kutunga, kurekebisha na kusimamia utekelezaji wa sera; kuandaa mkakati wa utekelezaji wa sera; kufanya tathmini ya utekelezaji wa sera; kuondoa muingiliano baina ya sera; na kutoa taarifa za utekelezaji wa sera;

ii. Kuwezesha sera mpya kutungwa na baadhi ya sera za sekta kupitiwa na matoleo mapya ya sera hizo kutolewa ili kuwezesha sera na mikakati ya sekta kuendana na wakati na mahitaji ya kitaifa na kimataifa; na

iii. Kuboresha mfumo wa Kielektroniki wa Uratibu wa Shughuli za Serikali ambao umejumuisha Moduli za Sera, Maagizo ya Viongozi wakiwa nje ya nchi pamoja na kuongeza wigo wa matumizi ya mfumo huo hadi ngazi ya Taasisi za Serikali na Halmashauri kwa ajili ya kuwezesha upatikanaji wa taarifa za utekelezaji Sera, Ahadi na Maagizo ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa.

## 9.11 Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu

Mafanikio yaliyopatikana katika utoaji wa Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ni pamoja na:

i. Kuandaa Mpango Kazi wa Taifa wa Haki na Ustawi kwa Watu Wenye Ualbino 2024/2025 – 2028/2029 (MTHUWWU) ambao umelenga kuimarisha ustawi, ulinzi na usalama kwa Watu Wenye Ualibino nchini. Mpango umeweka Mikakati mahsusi kuhusu Ulinzi; Kinga; Usawa na kutobaguliwa; na Uwajibikaji katika kutekeleza afua mbalimbali za Watu Wenye Ualibino;

ii. Kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Teknolojia Saidizi 2024 – 2027 *(National Assistive Technology Strategy – NATS).* Mkakati umeweka mazingira wezeshi ili kuhakikisha kila Mtanzania mwenye uhitaji wa vifaa saidizi avipate kwa wakati kupitia watoa huduma wenye weledi na kwa gharama nafuu; na

iii. Kuanzisha mfumo wa Kielektroniki wa Taarifa na takwimu kwa Watu Wenye Ulemavu – *(Persons with Disability Management Information System - PD-MIS)* mwaka 2023. Hatua hii imeongeza ufanisi wa upatikanaji wa taarifa sahihi za Watu Wenye Ulemavu zitakazowezesha upangaji wa mipango ya maendeleo kwa kundi hili.

## 9.12 Ukuzaji wa Fursa za Ajira, Ujuzi na Huduma za Ajira

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuzalisha ajira 8,084,204 kwa kushirikiana na sekta binafsi kupitia utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ikiwemo ujenzi wa bomba la mafuta ghafi la Afrika Mashariki, reli ya kisasa, Bwawa la Kufua Umeme la Julius Nyerere na Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa

Msalato;

ii. Kuongezeka kwa vijana waliopata mafunzo kupitia Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi kutoka vijana 30,873 mwaka 2021 hadi vijana 77,228 mwaka 2025. Mafunzo hayo yameboresha upatikanaji wa nguvukazi yenye ujuzi stahiki katika soko la ajira ili kuchochea uwekezaji, biashara na kukuza kipato cha watanzania;

iii. Kuongezeka kwa vijana waliopata mafunzo ya uzoefu wa kazi katika taasisi za umma na binafsi kutoka vijana 4,136 mwaka 2020 hadi vijana 23,384 mwaka 2025. Mafunzo hayo yameongeza uzoefu unaotokana na kujifunza kwa vitendo na hatimaye kuweza kujiajiri na kuajiri wengine;

iv. Kuanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Taarifa za Soko la Ajira nchini ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za soko la ajira kwa wakati. Taarifa hizi zimewezesha Watu binafsi na waajiri kupata fursa ya kuchagua waajiriwa bora, hivyo kuongeza ufanisi na tija; na

v. Kuunganisha Watanzania 7,019 na fursa za ajira nje ya nchi. Fursa hizo zimechangia kuongeza kipato kwa watanzania na kuchangia Pato la Taifa.

### 9.13 Hifadhi ya Jamii

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuandaa Sera ya Taifa ya Kinga ya Jamii ya Mwaka 2023 pamoja na Mkakati wa utekelezaji wa mwaka 2023 hadi 2033 ambayo umeweka uratibu madhubuti na kuimarisha utekelezaji wa afua stahiki za kinga ya jamii;

ii. Kuanzisha mifumo ya kielektroniki ikiwemo mfumo wa PSSSF PAMOJA kwa upande wa Mfuko wa Hifadhi ya

Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF) na mfumo wa NSSF KIGANJANI kwa upande wa Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) ambapo wanachama wanajisajili, kuhakiki na kuwasilisha madai ya Mafao yao kwa njia ya mtandao;

iii. Kuongeza ulipaji wa mafao ambapo Mfuko wa NSSF ulilipa Shilingi bilioni 3,520 na malipo kwa mwaka kutoka Shilingi bilioni 537.08 mwaka 2021 hadi kufikia Shilingi bilioni 704.94 kwa mwaka 2025. Aidha, Mfuko wa PSSSF ulilipa mafao ya Shilingi bilioni 5,218. 64 na malipo ya mafao kwa mwaka yalifikia wastani wa shilingi bilioni 1,482.18 kutoka shilingi bilioni 2,390.47 mwaka 2021. Vilevile, Mfuko wa WCF ulilipa mafao ya Shilingi bilioni 84.62 kati ya Juni, 2021 hadi Machi 2025 na malipo ya mafao ya mwaka kutoka Shilingi bilioni 13.19 mwaka 2021 hadi Shilingi bilioni 28.02 mwaka 2025;

iv. Kuongeza idadi ya wanachama wachangiaji kutoka 849,886 mwaka 2021 hadi 1,758,018 mwaka 2025. Kati yao wanachama 1,320,699 waliandikishwa kutoka sekta rasmi na wanachama 437,319 ni wananchi waliojiajiri;

v. Kuboresha ulipaji wa mafao kwa wastaafu kwa kufanya mabadiliko ya Kikokotoo kwa watumishi nchini. Maboresho hayo ya malipo ya mkupuo kutoka asilimia 33 hadi asilimia 40 kwa waliokuwa wanalipwa asilimia 50, na kutoka asilimia 33 hadi 35 kwa waliokuwa wanapata asilimia 25 kabla ya kuunganisha Mifuko mwaka 2018; na

vi. Kuongeza kima cha chini cha pensheni kutoka shilingi 100,000 hadi shilingi 150,000 kwa mwezi na kuhuisha pensheni ya kila mwezi kwa kiwango cha asilimia mbili (2) kwa kuzingatia sheria na Kanuni zilizopo.

### 9.14 Maendeleo ya Vijana

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na:

i. Kuandaa Sera ya Taifa ya Maendeleo ya Vijana (2007), Toleo la Mwaka 2024 na Mkakati wa utekelezaji wa Mwaka 2024 - 2034 ambayo imeimarisha ustawi na maendeleo ya vijana kwa kutoa mwongozo wa kuwezesha ushiriki wa Vijana kwenye shughuli za kijamii, kisiasa na kiuchumi; na

ii. Kufanya maboresho ya Sheria ya Ununuzi wa Umma Sura Na. 410 yaliyowezesha kutenga asilimia 30 ya ununuzi wa Umma kwa ajili ya Makundi maalum (Wanawake, Vijana, Wazee na Wenye Ulemavu) ambayo imewezesha jumla ya Kampuni 299 zinazomilikiwa na vijana kuunganishwa na Mamlaka ya Ununuzi Serikalini (PPRA) na kunufaika na zabuni za umma zenye thamani ya shilingi bilioni 10.8 na hivyo kujiongezea mitaji.

### 9.15 Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo

Sekta ya Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo imeendelea kukua kwa kiwango kikubwa na kuleta tija kwa maisha ya Watanzania pamoja na kutoa ajira kwa vijana wengi na kuongeza kipato cha mtu mmoja mmoja na Taifa kwa ujumla. Ukuaji wa sekta hiyo ulitokana na kuimarishwa kwa uhuru wa vyombo vya habari, kutekeleza mikakati thabiti ya kukuza lugha ya Kiswahili duniani, kuweka mazingira wezeshi ya kuendeleza wasanii na kazi za sanaa pamoja na kuboresha miundombinu ya michezo ili kuhamasisha wananchi wengi kushiriki katika michezo.

Mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na;

i. Kuongeza usajili na utoaji wa leseni kwa vyombo vya habari kutoka 788 mwaka 2020 hadi 1,042 mwaka 2025. Kati

ya vyombo hivyo, Magazeti ni 372, Radio 247, Television 68 na Radio za Mtandaoni na Televisheni Mtandao 355. Usajili na utoaji wa leseni kwa vyombo hivyo umeendelea kuimarisha uhuru wa vyombo vya habari na kuwezesha wananchi kupata habari kwa wakati;

ii. Kuongeza usikivu wa matangazo ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC) kutoka Wilaya 102 mwaka 2020 hadi Wilaya 139 mwaka 2025;

iii. Kufikisha matangazo ya TBC katika mataifa yote ya ukanda wa SADC na ulimwenguni kupitia majukwaa ya teknolojia ya TEHAMA. Pamoja na masuala mengine matangazo hayo, yamewezesha kuitangaza Tanzania kimataifa katika masuala mbalimbali ikiwemo kuonesha vivutio vya utalii vilivyopo nchini;

iv. Kuongeza idadi ya maneno yaliyoingizwa katika Kongoo la Kiswahili kutoka 200,000 mwaka 2020 hadi 39,000,000 mwaka 2025 pamoja na misamiati ya lugha ya Kiswahili kutoka 216 mwaka 2020 hadi 1,964 mwaka 2025. Aidha, misamiati hiyo imewezesha kuongezeka kwa wigo mpana wa mawasiliano katika jamii;

v. Kuongeza vituo vilivyosajiliwa vya kufundisha kiswahili kwa wageni kutoka vituo 5 hadi vituo 33; Balozi/Vituo vya kitamaduni vinavyofundisha kiswahili nje ya nchi kutoka 4 hadi 19; Watanzania wanaofundisha kiswahili nje ya nchi kutoka 73 hadi 495; na wakalimani wa kiswahili waliopo nchini kutoka 23 hadi 214. Huduma za kufundisha kiswahili na ukalimani kwa wageni zimesaidia kusimamia matumizi ya kiswahili fasaha na sanifu ndani na nje ya nchi na kutumia lugha ya Kiswahili kama ajira na chanzo cha mapato;

vi. Kuongezeka kwa idadi ya watu wanaotumia lugha ya Kiswahili duniani kutoka watu 190,000,000 mwaka 2020 hadi wati 500,000,000 mwaka 2025;

vii. Kupata ridhaa ya kiswahili kutumika kama lugha rasmi na lugha ya kazi katika jumuiya mbalimbali Afrika ikiwemo Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini Mwa Afrika (SADC) Mwaka 2019 na Umoja wa Afrika (AU) mwaka 2022. Aidha, Jumuiya ya Wazalishaji Almasi Afrika (ADPA) nao wameridhia matumizi ya Kiswahili katika mikutano yake;

viii. Kuongeza utambuzi wa maeneo ya urithi (Heritage Sites) yenye amali za kiukombozi kutoka 14 mwaka 2020 hadi 266 mwaka 2025. Utambuzi wa maeneo hayo umesaidia kuhifadhi kumbukumbu kuhusu mchango wa Tanzania katika harakati za ukombozi wa Umoja wa Afrika;

ix. Kuongeza mitaji ya mikopo iliyotolewa kwa wasanii kupitia Mfuko wa Utamaduni na Sanaa kutoka shilingi 1,077,000,000 kwa wasanii 45 hadi shilingi 5,250,070,500.89 kwa wasanii 359. Mikopo hiyo imewezesha wasanii kuzalisha kazi zenye ubora zinazokidhi viwango vya kitaifa na kimataifa;

x. Kuongezeka kwa vibali vya wasanii wa ndani kwenda nje ya nchi kufanya shughuli za Sanaa kutoka vibali 122 hadi vibali 1,492 na vibali vilivyotolewa kwa wadau kuingiza wasanii nchini kufanya shughuli za Sanaa kutoka vibali 75 hadi 623. Vibali vilivyotolewa vimewezesha wasanii kujifunza kutoka kwa wasanii wengine ndani na nje ya nchi, kuongeza ubora wa kazi za sanaa na kujiongezea kipato;

xi. Kuongeza kiasi cha mirabaha kilichogawiwa kwa wasanii waliosajiliwa COSOTA kutoka shilingi 245,000,000 hadi

shilingi 687,705,259 na hivyo kuwezesha wasanii kupata fedha na kunufaika na kazi zao za sanaa;

xii. Kuongezeka kwa ushiriki wa timu za Tanzania za michezo katika mashindano mbalimbali kutoka mashindano 68 hadi 402. Ushiriki wa timu za Tanzania katika mashindano hayo umesaidia wanamichezo kujifunza na kuitangaza nchi Kimataifa;

xiii. Tanzania kwa mara ya kwanza kuwa wenyeji wa mashindano ya Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON 2027) na Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji Wanaocheza Ligi za Ndani (CHAN 2025);

xiv. Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa viwanja vitakavyotumika kwa ajili ya michuano ya AFCON 2027 ambapo Uwanja wa Arusha umefikia asilimia 40.8; Uwanja wa Dodoma mkataba wa ujenzi ulisainiwa tarehe 13 Februari, 2025 na Mkandarasi amekabidhiwa eneo la ujenzi; ukarabati wa Uwanja wa Benjamin Mkapa umefikia asilimia 85; na kukamilika kwa ukarabati wa Uwanja wa Amaan Zanzibar;

xv. Kukarabati na kujenga viwanja vitano vya mazoezi vitakavyotumika wakati wa michuano ya AFCON 2027. Viwanja hivyo ni uwanja wa Mej. Gen. Isamuhyo, Uwanja wa Leaders Club, Uwanja wa Gymkhana, Uwanja wa Shule ya Sheria *“Law school”* na uwanja wa Farasi; na

xvi. Kupanda kwa nafasi ya Viwango vya FIFA kwa nchi ya Tanzania kutoka nafasi 137 hadi 107.

# HITIMISHO

Mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita ni matokeo ya uongozi mahiri na wenye maono ya Mheshimiwa *Dkt.* Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, nia yake ya kweli iliyowezesha kuwa na mshikamano wa kitaifa na uhuru wa kujieleza, utawala bora, maridhiano ya kisiasa, pamoja na ushirikiano ambao kwa kipindi chote cha utekelezaji umewezesha wananchi kuendelea kuiunga mkono Serikali.

Katika kipindi kilichobaki cha utekelezaji wa Ilani na kuwa madarakani, Serikali itaweka kipaumbele katika kukamilisha utekelezaji wa Ilani hiyo, mipango na mikakati ya maendeleo, pamoja na kuendelea kutoa huduma bora za kijamii na kiuchumi kwa wananchi. Vilevile, kukamilisha maandalizi ya Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050 na kuanza utekelezaji ili kuliwezesha Taifa kufikia malengo ya kuwa nchi ya kipato cha kati ngazi ya juu yenye uchumi mseto, stahimilivu, imara na jumuishi, usiokuwa na aina yeyote ya umaskini. Aidha, itaendelea kuweka msisitizo wa kuwa na mfumo jumuishi wa utawala, wenye uwazi ili kudumisha amani, uhuru na usalama wa watu, na kuzingatia masuala yanayohusu mabadiliko ya tabianchi ili kuwa na uchumi endelevu.

